# Nipashe

Jumatatu Julai 15, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579970

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



## Adaiwa kuua dada kumkuta na mpenzi wake nyumbani

UKURASA 3




UKURASA 13

# Makamba, Kinana waibuka na mazito

UK. 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### KIBANO CHA BOT KWA BENKI CHAUNGWA MKONO

BAADA ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kueleza kuwa inaendelea kuandaa kanuni za sheria ndogo za fedha ya mwaka 2018 na kuanza kutumika pamoja na...

UKURASA WA 3


### WAMILIKI SHULE BINAFSI WATAKA UCHUNGUZI

WAMIKILI wa shule binafsi nchini wameiomba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kuchunguza programu zinazoanzishwa mara kwa mara na kuingia gharama ya...

UKURASA WA 5

### W'BIASHARA WAWEKEWA MAFUMO KUONDOA KERO

SIKU chache baada ya Rais John Magufuli kuonyesha kukerwa na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushindwa kushughulikia ipasavyo masuala yanayowahusu...



MAKAMBA



KINANA

## Mkurugenzi Mtendaji wa Benki TIB atumbuliwa

UKURASA 3



## Msongamano wa wafungwa, mahabusi wamtisha waziri

UKURASA 2

MICHEZO MAGORI: SIMBA SC TUMEJIPANGA UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

# Makamba, Kinana waibuka na mazito

**Na Salome Kitomari**

MAKATIBU wakuu wastaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Yusuph Makamba na Abdulrahman Kinana, wameeleza kusikitishwa na kauli za kuwachafua na kuwadhalilisha zinazotolewa dhidi yao.

Vilevile, walidai wameandika barua kwa viongozi wa Baraza la Ushauri la Viongozi Wakuu wastaafu, kuwasihi watumie busara katika kushughulikia jambo hilo linaloelekea kuhatarisha umoja, mshikamano na utulivu wa chama hicho.

Taarifa hiyo iliyosainiwa na viongozi hao na kusambazwa kwenye vyombo vya habari nchini jana, walidai wameamua kutokwenda mahakamani kwa sababu kuu mbili.

"Jambo hili lina taswira ya kimkakati na lina mtandao wenye malengo ya kisiasa, kwa hiyo linapaswa kushughulikiwa kisiasa, pili unapochafuliwa unachokwenda kudai mahakamani ni fidia, kwetu sisi heshima yetu haiwezi kuthaminishwa na fidia," taarifa yao ilieleza.

Walisema kauli zinazotolewa na mwanaharakati mmoja, zinaonyesha anatumika kama kipaza sauti na mamluki anayetumika kuivuruga CCM na nchi kwa ujumla.

"Baada ya kupata ushauri kutoka kwa watu mbalimbali wakiwamo viongozi wakuu wastaafu wa CCM, viongozi wa dini, wanataaluma, wanahabari, wana-CCM na wananchi kadhaa tumeamua kutoa tamko hili," ilisema taarifa hiyo.

Katika taarifa yao hiyo, wamedai, kauli ya mwanaharakati huyo ya kwanza ilidai viongozi hao wanamkwamisha Rais, hata hivyo walipuuza kwa kuwa walijua ni uzushi na wanajua hawawezi kuihujumu serikali na chama walichokitumikia kwa maisha yao yote na wakiwa wastaafu hawawezi kufanya hivyo.

Vile vile walidai kuwa mwanaharakati huyo kwa mara nyingine alidai kuwa wao (Makamba na Kinana) wana mhujumu Rais asipitishwe muhula wa pili wa urais wa 2020.

Walieleza katika taarifa yao hiyo kuwa kwa uzoefu wao wa kusimamia mchakato wa mgombea urais na nafasi nyingine, kauli hiyo ni uzushi na uzandiki uliosukwa kwa malengo maalum.

"Kwa bahati mbaya viongozi wetu hawakuchukua hatua yoyote na zaidi ameendelea kuwadhalilisha na kuwavunjia heshima viongozi wastaafu na watu wengine katika jamii," taarifa yao hiyo ilieleza na kuongeza:

"Mtu huyu amefikia hatua ya kuthubutu kuwatuhumu viongozi

INAENDELEA UK. 8



Wakazi wa Kijiji cha Buraga, Kata ya Bukumi, Musoma Vijijini mkoani Mara, wakipanga matofali juzi, ambayo wamefyatua kwa ajili ya ujenzi wa shule shikizi kijijini mwao. **NA MPIGA PICHA WETU**

# Msongamano wafungwa, mahabusi wamtisha waziri

**Na Rose Jacob,** MWANZA

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Yusuf Masauni, amewaagiza wakuu wa Magereza nchini kuhakikisha wanaondoa changamoto ya msongamano wa mahabusi katika magereza kwa kufanya ziara za mara kwa mara.

Agizo hilo alilitoa mwishoni mwa wiki alipofanya ziara katika Gereza la Butimba mkoani hapa.

Alisema endapo wakuu wa magereza watakuwa na utaratibu wa kuwatembelea mahabusi mara kwa mara, watabaini mambo mengi ambayo kwa namna moja au nyingine yatapunguza msongamano wa mahabusi.

"Katika hili la msongamano wa wafungwa na mahabusi, nawaagiza wakuu wote wa magereza nchini wafanye ziara za mara kwa mara magerezani. Wasisubiri mpaka sisi viongozi wa wizara tuje kwenye magereza kuzungumza na mahabusi na wafungwa," alisema na kuendelea:

"Kusikiliza changamoto mbalimbali, waanze wenyewe kuzungumza nao, na nina uhakika watabaini changamoto nyingi kama ambavyo sisi tunaziona."

Alisema msongamano wa mahabusi katika magereza mengi unasababishwa na uwapo wa mahabusi ambao makosa waliyotenda yanadhaminika, hivyo wangeweza kuwa nje kwa dhamana hadi hukumu zitakapotoka.

"Haya ndiyo maelekezo yangu. Kuna kesi nyingi ambazo hazieleweki, kuna mahabusi wengine wapo gerezani bila hatia, naomba mchukue hatua na kufuatilia. Wale ambao wanastahili kubaki magerezani wabaki ila tusiwaonee raia ambao hawastahili kuwamo magerezani," alisema.

Awali akitoa taarifa kwa Naibu Waziri, Mkuu wa Magereza Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi SACP Rajabu Hamza, alisema siku hiyo ya ziara ya Naibu Waziri, magereza yote matano ya mkoa huo yalikuwa na idadi kubwa ya wafungwa na mahabusi kuliko uwezo wake.

"Magereza ya Butimba, Kasungamile, Ukerewe, Magu na Ngudu yote kwa pamoja uwezo wake ni kupokea wahalifu 1,249, lakini kwa siku hii ya leo kuna wahalifu 2,633. Hii ina maana kwamba wahalifu 1,384 wameongezeka, hivyo kuleta msongamano," alisema SACP Hamza.

Wakati huo huo, Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza imezindua mahakama inayotembea (mobile court') itakayosaidia kupunguza msongamano wa mahabusi kwa kuwa itakuwa ikisikiliza mashauri mengi kwa muda mfupi na kuyatolea uamuzi.

Jaji Mfawidhi Kanda ya Mwanza, Sam Rumanyika, aliwataka mahakimu watakaokaa kwenye mahakama hiyo kusikiliza mashauri kwa wakati na kutenda haki, pia waepuke kuahirisha mashauri bila sababu za msingi.

"Mahakama hii ya kidijitali haitafanya kazi mithili ya daladala bali kutakuwa na vituo maalum vilivyowekwa ambavyo ni karibu na wananchi ili kuwapunguzia gharama na muda wa kupata haki mahakamani," alisema Jaji Rimanyika.

# Benki zaunga mkono BoT kibano wasumbufu kwa wakopaji

**Na Elizabeth Zaya**

BAADA ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kueleza kuwa inaendelea kuandaa kanuni za sheria ndogo za fedha ya mwaka 2018 na kuanza kutumika pamoja na mambo mengine, kuzibana benki zinazoumiza wateja waliokopa, Chama cha Benki Tanzania (TBA) kimesema kinakubaliana na uamuzi huo.

Ofisa wa Dawati la Malalamiko ya Wateja wa huduma za kibenki wa BoT, Ramadhani Myonga, aliiambia Nipashe wiki iliyopita kuwa kibano hicho kitaanza hivi karibuni, baada ya kumalizika kwa uandaaji wa kanuni za sheria ndogo za fedha ya mwaka 2018 na kuanza kutumika.

Akizungumza na Nipashe Mkurugenzi Mtendaji wa TBA, Tusekelege Joune, alisema TBA wanasapoti kwa mikono miwili ujio wa sheria hiyo kwa kuwa wanaamini itaendelea kuimarisha ushirikiano na wateja wao.

Pia alisema itaongeza uwazi, kupunguza malalamiko na itaweka usawa katika huduma zinazotolewa baina ya benki moja na nyingine.

"Ni kweli tunajua kwamba sheria hiyo inakuja, lakini sisi tuko positive (chanya) nayo, na tunaisubiri kwa sababu itamsaidia pia mteja kufahamu nini anatakiwa kufanya anapokopa," alisema.

Wiki iliyopita Myonga alisema kibano kinaandaliwa kwa benki ambazo zimekuwa zikitengeneza mikataba na masharti ya mikopo, kwa lengo la kuumiza wakopaji kwa kuwawekea masharti magumu ambayo hawawezi kuyatekeleza.

BoT inasema kwamba lengo la benki hizo kuandaa mikataba na masharti magumu kwa wakopaji ni kupiga mnada mali zao pale wanaposhindwa kulipa kwa wakati mikopo wanayokopa.

Myonga, alisema kibano hicho kitaanza hivi karibuni, baada ya kumalizika kwa uandaaji wa kanuni za sheria ndogo za fedha ya mwaka 2018 na kuanza kutumika.

Myonga alisema wamebaini kwamba benki nyingi zimekuwa zikiweka masharti magumu ambayo siyo rafiki kwa wakopaji ambayo pia hayampi ahueni mkopaji kumwongeza muda mkopaji huyo kulipa mkopo wake pale anapopata mtikisiko kiuchumi.

"Kwa mfano, unaweza kukuta mteja anayekopa anaambiwa atarejesha kiasi fulani cha fedha kumbe wakati huo huo rejesho lake halijajumuishwa na fidia ya mkopo wa mwezi... mteja anapaswa ajue hata na sehemu ya marejesho, lakini hata zile document (nyaraka) za mikopo yao huwa hata hawapewi,"

INAENDELEA UK. 8



Daktari wa Mifugo kutoka Shirika la Haki na Ustawi wa Wanyama Tanzania (TAPO), Master George, akitoa elimu ya namna ya kutambua mifugo inayoumwa kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Bulige Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga. **PICHA NA SHABAN NJIA**

# Wamiliki shule binafsi wataka uchunguzi programu za mafunzo

**Na Salome Kitomari**

WAMIKILI wa shule binafsi nchini wameiomba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kuchunguza programu zinazoanzishwa mara kwa mara na kuingia gharama ya kutozwa fedha.

Kauli hiyo imekuja baada ya shule hizo kupokea maelekezo kutoka wizara kwenda kwa madereva wa magari ya wanafunzi wa shule zao kupewa mafunzo ya usalama barabarani.

Katika barua ya Mei 28, mwaka huu, kutoka kwa Katibu Mkuu wa Tamisemi, yenye kumbukumbu namba Na. HA.193/222.01/71, ilieleza kuridhia mafunzo hayo kufanyika kwa shule zote binafsi nchini.

Barua hiyo ilielekezwa kwa Mwenyekiti wa Umoja wa wamiliki wa shule na vyuo binafsi nchini (Tamongsco), Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kikristo ya Huduma za Kijamii (Christian Social Service Commission), Katibu Mtendaji Baraza Kuu la Waislamu Tanzania na Mwenyekiti wa Umoja wa wawekezaji binafsi kwenye elimu.

Barua hiyo iliyosainiwa na Kaimu Katibu Mkuu, Prof. James Mdoe, alieleza kuwa wamepokea barua kutoka taasisi isiyo ya kiserikali ya Anti-Poverty and Environment Care (Apec) wakiomba kibali cha wizara kuendesha mafunzo ya usalama barabarani kwa lengo kuimarisha usalama.

"Kwa kuwa Apec wana kibali cha kuendesha mafunzo kutoka kwa Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Tanzania, wizara haina pingamizi, unaombwa kutoa ushirikiano kwa mkurugenzi wa taasisi hiyo kuhusu kutoa mafunzo husika," alisema.

Kwa mujibu wa barua ya taasisi hiyo yenye kumbukumbu namba APEC/NGO/T/01/52/19 kwenda kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Aprili 16, mwaka huu, ina kichwa cha habari kuanza utekelezaji wa mafunzo ya salama barabarani kwa madereva wa mabasi ya shule na wanafunzi Tanzania.

Vile vile, shirika hilo limejitambulisha kuwa linajihusisha na kupambana na umaskini, ajali za barabarani na kutunza mazingira Tanzania Bara, linamiliki shule ya madereva na wamepata kibali cha kutoa mafunzo kwa madereva ngazi zote nchini.

Barua hiyo iliyosainiwa na Mkurugenzi Mtendaji, Respicius Timanywa, alisema wameamua kutoa mafunzo kwa madereva hao ili kuwajengea uelewa wa taratibu za usalama barabarani na majukumu yao kuhakikisha wanatii sheria kwa usalama wa wanafunzi.

"Hii ni kwa sababu ajali nyingi zinazosababishwa na madereva wasio na mafunzo sahihi wanaosababisha vifo vya wanafunzi wasio na hatia na wakati mwingine kusababisha misukosuko mingi barabarani inayowafanya wanafunzi kunusurika mara kwa mara," alisema.

Alisema wameamua kuwapa mafunzo madereva hao kutokana na umuhimu wao na majukumu mengi kuliko madereva wa daladala, lakini wamiliki wa shule hawakumbuki kuwapa mafunzo wala semina mpaka majanga yanapotokea.

"Zamani dereva alikuwa mtu mwenye dhamana ya kubeba watoto kutoka nyumbani mpaka shuleni na kuwarejesha kwa sasa wanatakiwa kutambua kazi yao ni zaidi ya kuendesha gari," alisema.

Walitaja baadhi ya wajibu wa dereva kuwa ni mlinzi wa mwanafunzi, kuwa na lugha nzuri na rafiki kwa wanafunzi, kuwa na heshima, kujua tabia za wanafunzi, kuwazuia wanafunzi wasije na vitu vya hatari shuleni, kutoa huduma ya kwanza, kuwa jicho la shule awapo barabarani na mwenye tabia njema.

Barua hiyo ilieleza kuwa utafiti waliofanya wamebaini umuhimu na majukumu ya dereva wa basi la shule ni zaidi ya kuendesha, lakini wengi wana leseni bila mafunzo sahihi, hawana mafunzo ya usimamizi na ulinzi wala huduma ya kwanza.

INAENDELEA UK. 8

## Sababu za bosi wa TIB kutumbuliwa

**Na Salome Kitomari**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imesitisha uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya TIB Corporate, Frank Nyabungege, kwa kile kilichoelezwa ni mwenendo usioridhisha wa benki hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na BoT, imebainisha kuwa uamuzi huo umesukumwa na mwenendo usioridhisha wa benki hiyo katika kuleta mabadiliko.

Aidha, kutokana na uamuzi huo, BoT kwa mamlaka iliyopewa na sheria ya benki na taasisi za fedha mwaka 2006 imemteua Fred Luvanda, kuwa Kaimu Mkurugenzi.

Kabla ya uteuzi huo, Luvanda alikuwa Kurugenzi ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha, na kwa nafasi ya sasa atasimamia shughuli zote za kiutendaji za benki ya TIB Corporate.

Taarifa hiyo ya Idara ya Uhusiano na Itifaki, ilieleza kuwa hatua hizo zimechukuliwa kwa lengo la kuboresha usimamizi na utendaji wa benki zinazomilikiwa na serikali.

"Benki Kuu ya Tanzania inauhakikishia umma kuwa benki ya TIB Corporate itaendelea kutoa huduma na madai yote yaliyoiva yatalipwa kama kawaida. Itaendelea kulinda maslahi ya wenye amana katika benki ili kuhakikisha sekta ya fedha inakuwa stahimilivu," alibainisha.

# Adaiwa kuua dada kumkuta na mpenzi wake nyumbani

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linamtafuta Daudi Bundala kwa tuhuma za kumshambulia dada yake, Suzana Bundala (21), kwa kumpiga kitu kizito kichwani na kumsababishia kifo, baada ya kumkuta akiwa amelala na mpenzi wake nyumbani kwao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Richard Abwao, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema lilitokea Ijumaa usiku katika Kijiji cha Bugoshi, Kata ya Uyogo Wilaya ya Kipolisi Ushetu.

Alisema kuwa, chanzo cha tukio hilo ni Suzana kukutwa akiwa na mpenzi wake, Eddy Nkimbila, nyumbani kwao kitendo kilichomchukiza mtuhumiwa na kumshambulia dada yake na kumsababishia kifo.

"Ilikuwa saa tano kamili usiku katika Kijiji cha Bugoshi ambapo Daudi Bundala alimkuta dada yake akiwa amelala na mpenzi wake Eddy Nkimbila nyumbani kwao kisha kumshambulia na kitu kizito kichwani na kumsababishia kifo," alisema Kamanda Abwao.

Kamanda Abwao alisema hata hivyo, mtuhumiwa akimbia baada ya tukio hilo na juhudi za kumtafuta na kumkamata zinaendelea, na kuongeza kuwa mwili wa marehemu umekabidhiwa kwa ndugu zake kwa ajili ya taratibu za mazishi.

Aliwataka wananchi mkoani Shinyanga kuacha tabia ya kuendelea kujichukulia sheria mkononi, ili kuepisha matukio ya kikatili na uvunjaji wa sheria.

# Nachingwea yapunguza magonjwa mabusha, matende

**Na Said Hamdani,** LINDI

SERIKALI imefanikiwa kupunguza maambukizi ya magonjwa ya mabusha na matende katika Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi kutoka watu 600 waliokuwa wakiugua hadi 300.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema hayo wakati wa uzinduzi wa huduma za kliniki tembezi, katika kambi ya upasuaji wa ugonjwa wa mabusha Mkoa wa Lindi, Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea.

Akisoma hotuba kwa niaba ya Waziri Ummy, Mkurugenzi wa Huduma za Kinga, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subbi, alisema katika kipindi cha miaka minne, kuanzia mwaka 2014 sasa wilaya 96 kati ya 120 zimepunguza maambukizi kwa kiwango kikubwa hadi kufikia kusimamisha uwezeshaji wa kingatiba kwa ngazi ya jamii.

Kwa ugonjwa wa trakoma au vikope, Dk. Subbi alisema wilaya 71 zilizokuwa na maambukizi ya ugonjwa huo, 65 zimefaulu kuutokomeza na kufikia kiwango ambacho kimefanya kusimamisha umezeshaji dawa ya Zthromax@ kwa wananchi.

Dk. Subbi alipongeza viongozi wakiwamo watoa huduma za afya na wananchi walioitikia wito wa kumeza dawa za kingatiba na kuondoa maradhi hayo.

Vile vile, aliwataka wananchi wa Mkoa wa Lindi, hasa wilaya ambazo bado hazijapunguza kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa matende na mabusha, kuzitumia dawa zinazotumika kutibu ugonjwa huo ni salama na zimethibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Katika zoezi hilo linaloendeshwa na wataalamu kutoka Hospitali ya Rufani ya Muhimbili, wagonjwa zaidi ya 300 kati ya 600 waliolengwa kupatiwa huduma ya upasuaji wamefanikiwa kuondoa mabusha wilayani Nachingwea.



Mratibu mwenza wa Mradi wa Sahiwal kutoka Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) Makao Makuu Dodoma, Neema Urassa, akizungumza na wafugaji wa Transmara nchini Kenya wakati wa ziara ya mafunzo ya wafugaji kutoka Tanzania waliotembelea wenzao wa Kenya kwenye mradi unaofadhiliwa na Shirika la Kimataifa la AU-IBAR.

# Kiwanda mbolea bil. 14/- sasa kukamilika Februari

**Novatus Makunga,** ARUSHA

KIWANDA cha mbolea itakayozalishwa kutegemeana na aina ya udongo na mahitaji ya mazao shambani kinatarajiwa kukamilika mwezi Februari mwakani katika eneo la Vikawe wilayani Kibaha mkoani Pwani kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 14.1.

Mbolea ya kiwanda hicho itatokana na matokeo ya upimaji wa udongo katika mashamba ya wakulima kwa kutegemeana na mahitaji ya rutuba katika ardhi.

Akizungumza na Nipashe, mtendaji mkuu wa kampuni inayojenga kiwanda hicho ya Live Support System ya mjini hapa, Dk. Edmond Matafu, alisema mradi huo umewezeshwa kwa mkopo nafuu kutoka Uholanzi.

Alisema mkopo huo kutoka Taasisi ya Uwekezaji wa Sekta Binafsi (PSI) ya Uholanzi ambayo imetoa Dola za Marekani milioni 5.3 (zaidi ya shilingi bilioni 12.1) na Euro milioni 5.3 (zaidi ya shilingi bilioni 1.9).

Dk. Matafu alisema kiwanda hicho kitakapokamilika kitatoa ajira kwa Watanzania zaidi ya 200, huku kikiwa na uwezo wa kuzalisha tani 40 kwa saa. Alisema sambamba na kiwanda hicho, pia wameanza kutoa huduma ya upimaji wa udongo kwa kutumia maabara zilizofungwa ndani ya magari pamoja na vifaa vingine vidogo vinavofahamika kama skana.

Alisema wakulima baada ya kupata matokeo ya upimaji wa udongo watatengenezewa mbolea, huku kiasi cha chini kikiwa kilo 200.

"Aina hii ya teknolojia inapunguza matumizi ya mbolea shambani kwa asilimia 40, lakini inampa mkulima ongezeko la mazao atakayovuna kwa zaidi ya theluthi mbili," alisema.

Dk. Matafu alifafanua zaidi kwamba mbolea itakayozalishwa kiwandani hapo itakuwa katika muundo wa kidonge ambacho kitazamishwa katika udongo shambani na kifaa kinachofanana na pampu ya kujazia upepo katika baiskeli. Akifafanua kuhusiana na huduma ya upimaji wa udongo (LSSL), Dk. Matafu alisema wameshapima sampuli za udongo zaidi ya 60,000 na kutoa majibu, huku nyingine 15,000 za mikoa ya Nyanda za Juu Kusini zikiwa katika mchakato wa mwisho wa kutolewa majibu na ushauri.

Alisema maabara iliyofungwa katika magari ina uwezo wa kupima sampuli za udongo kwa mazao zaidi ya kumi, huku kwa vifaa vidogo vya upimaji vinavyofahamika kama skana vikipima mazao yasiyozidi mawili.

"Kwa upande wa magari ambayo yana maabara, tutakuwanayo manne tukianza na hilo ambalo lilizinduliwa mapema wiki hii hapa Arusha, huku hivyo vifaa vidogo vya upimaji udongo tukiwa navyo 100," alifafanua.

Dk.Matafu alisema gharama za upimaji huo wa udongo ni za kawaida dola za Marekani 12.5 (sawa na shilingi 28,712), ukilinganisha na za nchi za Afrika Mashariki ambazo ni dola za Marekani 50 (sawa na shilingi 114,849).

Wiki iliyopita akizindua moja ya gari lenye maabara ya kipimia udogo, Waziri wa Kilimo, Maliasili na Chakula wa Uholanzi, Majolijn Sonema, alieleza kuvutiwa na huduma hizo alizoeleza zinampa uhakika mkulima wa kupata mavuno ya mazao ya uhakika.

Alisema wakulima katika nchi nyingi za Afrika wanakosa huduma za upimaji wa udongo ambapo matokeo yake ni muhimu katika kufahamu aina ya mbolea inayohitaji katika udongo.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, aliwataka wakulima kutumia teknolojia ya upimaji wa udongo katika kujihakikishia mavuno ya kutosha.

# Tanapa yabadili muundo wake kisa kukabili ujangili

**Na Salome Kitomari**

MABADILIKO ya mbinu za ujangili duniani yamelifanya Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), kubadili muundo na mfumo wa utendaji kazi kwa kuwa jeshi la uhifadhi na misitu (Usu).

Kamishna Uhifadhi wa Tanapa, Dk. Allan Kijazi, akiwasilisha mada ya mabadiliko ya kimuundo na kiutendaji wa shirika hilo, kwenye mkutano wa wahariri na waandishi waandamizi, alisema mabadiliko hayo yamejumuisha kuhama kutoka mfumo wa kiraia na kuwa jeshi Usu.

Alisema Tanapa inasimamia hifadhi 19 kwa sasa, na kwamba majangili wanatumia mbinu za kisasa ambazo mamlaka zinazolinda rasilimali hazikuwa nazo.

"Miaka ya nyuma tulilazimika kutumia Polisi na Jeshi la Wananchi ambao wengi hawana uelewa wa umuhimu wa wanyamapori kwamba wapambane na ujangili na wakati huo huo walinde wanyama, kwa sisi kuwa jeshi Usu tutaweza kutumia silaha nzito na kupambana na ujangili," alisema.

Kwa mujibu wa Kijazi, ulinzi na usalama kwa sasa umeimarishwa ndani na nje ya hifadhi kuhakikisha shughuli za utalii zinafanyika kwa utulivu na kuendelea kuvutia watalii wengi zaidi.

"Haikuwa rahisi kupambana na majangili kwa kufanya operesheni za muda mfupi, walijua kwa kuwa kipindi cha operesheni waliweka silaha chini na baada ya kwisha waliendelea na ujangili lakini kwa sasa ni ulinzi endelevu wa raslimali zetu," alibainisha.

Kamishna huyo alisema kuwa mafunzo maalum kwa watumishi wa Tanapa yanatolewa katika kituo cha Mlele, Katavi na kwamba watakaopata mafunzo hayo ni ambao tayari wana elimu za shahada na uzamili.

Aidha, alisema vyuo cha wanyamapori Pasiansi na Mweka vitaendelea kutoa mafunzo kwa maofisa wa ngazi za kati.

Naye, Niabu Kamishna wa Uhifadhi na Maendeleo ya Biashara, Willium Mwakalema, akiwasilisha mada juu ya mpango wa Tanapa kumaliza migogoro kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi, alisema wameandaa mpango wa matumizi bora kwa vijiji vinavyozunguka hifadhi ili kumaliza au kuondoa migogoro iliyopo.

Alisema utekelezaji utaanzia kwenye hifadhi za Tarangire, Ziwa Manyara na Serengeti kwa wilaya zinazozunguka na baadaye watakwenda kwenye hifadhi nyingine.

Mwakalema alisema wamefikia vijiji 74 na vimebakia 21 na fedha zitakazotumika ni Sh. bilioni 1.7, na kwamba wananchi watatambua mahali pa kilimo, vyanzo vya maji, malisho na maeneo ya wazi.

"Kuwezesha mpangowa vijiji vilivyopo kando mwa hifadhi kutapunguza migogoro kati ya uhifadhi na jamii, lengo hasa ni kutunza bayonuai iliyopo nje ya hifadhi," alisema.

Alisema umuhimu wa mpango huo ulisukumwa na matukio ya kuweka sumu kwenye mizoga ya wanyama wafugwao ili wanyamapori wafe na kuna tukio la simba tisa na ndege kufa baada ya kula mzoga uliowekwa sumu na wananchi.

## HABARI KITAIFA




Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam akipita karibu ya meza za wafanyabiashara wa matunda waliojipanga pembeni mwa Barabara ya Msimbazi jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajasiriamali waliofanya vizuri watafutiwa fursa

**Na Beatrice Philemon**

JUMLA ya wajasiriamali 15 wanaofanya biashara ndogo ndogo na kati ambao wamefanya vizuri katika biashara kutoka mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Lindi, Mtwara, Iringa na Njombe wamefadhiliwa na Mradi wa Tanzania Local Enterprise Development (TLED) ili kushiriki maonyesho ya Sabasaba mwaka.

Akizungumza na waandishi wa habari, Ofisa Mawasiliano wa Mradi wa TLED, Jemima Michael, alisema lengo kuu ni kuwapa fursa wajasiriamali kujifunza kwa kuona wenzao wanafanya nini, kuzitangaza biashara zao kimataifa kupitia jukwaa la maonyesho ya Sabasaba na pia kuwasaidia kupata soko ikiwamo kujifunza teknolojia tofauti ili kuboresha bidhaa zao.

Alisema mradi wa TLED ni maalumu kwa wajasiriamali wa biashara ndogo na ulianzishwa kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali katika kukabiliana na vikwazo vya biashara vinavyowakabili hasa upatikanaji na ukuaji wa masoko katika sekta ya biashara ya kilimo kwa kuzingatia changamoto za ziada zinazowakabili wanawake wajasiriamali.

"Huu ni mradi wa miaka mitano (Aprili 2015 - Machi 2020) unaofadhiliwa na Global Affairs Canada (GAC) wenye lengo la kutoa rasirimali muhimu za biashara kwa wajasiriamali wa ndani ili kuongeza ajira endelevu kwa wanawake na wanaume katika sekta ya biashara ndogo na ya kati na kuboresha

INAENDELEA UK. 8

# W'biashara wawekewa mfumo kuondoa kero

**Novatus Makunga,** ARUSHA

SIKU chache baada ya Rais John Magufuli kuonyesha kukerwa na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushindwa kushughulikia ipasavyo masuala yanayowahusu wafanyabiashara, wizara hiyo imeanzisha mfumo wa kliniki.

Mfumo huo unaziweka pamoja taasisi zote zilizopo chini yake kwa lengo la kuondoa kero na kuhudumia bila usumbufu.

Rais Magufuli alionyesha kukerwa kwa kutoshughulikiwa kwa kero mbalimbali alipokutana na wafanyabiashara wakubwa watano kutoka kila wilaya nchini jijini Dar es Salaam Juni 7, mwaka huu na baadaye alipokuwa akimwapisha waziri wa sasa wa wizara hiyo, Innocent Bashungwa Juni 10, mwaka huu.

Kuundwa kwa kliniki hizo za kutoa huduma kulibainishwa na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, mwishoni mwa wiki jijini hapa alipokutana na wanyabiashara na wajasiriamali wanaofanyakazi na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) katika Mkoa wa Arusha.

Alisema kuwa kliniki hiyo imeanzishwa mjini Dar es Salaam, na kwamba ni matarajio ya wizara hiyo utaratibu huo utaanzishwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

"Kliniki inafanyakazi kwa kutoa huduma kwa wafanyabiashara kuanzia zoezi la usajili wa biashara, utafutaji wa masoko na uuzaji wa bidhaa zao," alisema.

Manyanya aliwaambia wajasiriamali kwamba utaratibu wa kufanya kazi serikalini umebadilika na hivi sasa taasisi zake zote zimeanza kufanyakazi kwa pamoja ili kumaliza changamoto mbalimbali zinazowakabili wafanyabiashara na wajasiriamali.

"Tunatambua kwamba wafanyabiashara na wajasirimali ndiyo msingi wa mapato ya kuiwezesha kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwamo ujenzi wa miradi,

INAENDELEA UK. 8

## Bei ya pamba yakwamisha kampuni kununua

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KUSUASUA kwa soko la zao la pamba wilayani Kahama mkoani Shinyanga, kumedaiwa kutokana na kushuka kwa bei ya soko la dunia na kusababisha kampuni ya ununuzi kushindwa kununua kwa kuogopa kupata hasara.

Akizungumza jana na vyombo vya habari, Meneja wa shughuli wa zao la pamba kutoka Chama Kikuu cha Ushirika (KACU), Amri Mwinyimkuu, alisema mpaka sasa kati ya kampuni nne zilizopatiwa leseni ya ununuzi wa zao hilo ni mbili zilizoanza kununua pamba.

Alisema, bei iliyopitishwa kwa ajili ya kununua zao hilo ilikuwa ni Sh. 1,200, lakini kabla hawajaanza kununua ikaporomoka na kufikia Dola la Kimarekani 63 kwa pamba nyuzi, sawa na Sh. 1,449.

Pia alisema, kwa mkulima bei ya pamba bado haijashuka isipokuwa kampuni zinalalamika bei ya pamba nyuzi inazidi kushuka katika soko la dunia, nakuongeza endapo watanunua kwa bei Sh. 1,200 serikali iwapatie fidia ya hasara watakayoipata.

Hata hivyo, alisema bei ya pamba nyuzi katika soko la dunia imeporomoka kutoka Dola 1.53 hadi kufikia 1.39 kwa kilo moja, na kuongeza hali hiyo ndiyo inayosababisha kampuni nyingi kushindwa kupeleka fedha kwenye vyama vya msingi kununua.

Vile vile, Mwinyimkuu alisema, kati ya asilimia 33 hadi 35 huwa ni pamba nyuzi kwenye pamba mbegu, huku asilimia 62 hadi 65 huwa ni mbegu na kuongeza asilimia mbili inayobaki huwa ni uchafu ambao huwa unatupwa.

Kadhalika alisema kwa mwaka huu wanatarajia kupata zaidi ya kilo milioni 4.7 ikilinganishwa na mwaka jana walipata kilo milioni 2.3 na kuongeza zaidi ya wakulima 13,559 kutoka katika Halmashauri ya Ushetu, Kahama mjini na Msalala wamelima zao hilo.

Mkagunzi wa pamba wilayani hapa, Emmanuel Kileo, alisema, kati ya kampuni nne zilizopewa leseni ya ununuzi wa zao hilo, ni mbili tu zimejitokeza kununua zao hilo ambazo ni Fresho na Kaham Oil Mill.



# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Nidhamu iboreshwe kwa wachezaji nchini

**WAKATI** tayari Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), likiwa limeshatangaza kuwa msimu mpya wa Ligi Kuu Bara utafanyika kuanzia Agosti 23, mwaka huu, klabu zinatakiwa pia ziwaandae wachezaji wao kujitambua.

Ligi hiyo ndiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Kwa mara nyingine tena, msimu ujao, ligi hiyo inatarajiwa kushirikisha timu 20, ambazo zitacheza mechi 38 kila mmoja, kwa maana ya mfumo wa nyumbani na ugenini.

Klabu zimekuwa zikiwaandaa zaidi wachezaji wake katika kujiimarisha ndani ya uwanja, ili ziweze kuvuna matokeo mazuri kwenye mechi zote wanazocheza.

Lakini, klabu nyingine zimekuwa zikisahau kuwajenga wachezaji wake kisaikolojia, na hapa ndipo "haiba" ya mchezaji huonekana anapokuwa ndani na nje ya uwanja.

Nipashe zinawakumbusha viongozi wa klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara na zile za Ligi Daraja la Kwanza, kuwapa wachezaji wao, mafunzo maalumu ya kujitambua, ambayo pia yatachangia uwezo wa nyota hao wanapokuwa uwanjani.

Tumeshuhudia wachezaji mbalimbali wenye vipaji, wakishindwa kufanya vema na baadhi yao kuacha kuendelea kucheza kandanda kwa sababu ya kujiunga kwenye makundi ambayo si mazuri katika kukuza na kuimarisha taaluma zao.

Wachezaji wanapokosa mwongozo sahihi, vipaji vyao hupokea na hapo hupelekea klabu iliyomsajili inashindwa kufikia malengo yake na baadhi hushuka daraja wakati nyingine hushindwa kuendelea na ligi au mashindano ambayo ilikuwa inashiriki.

Jukumu hili lisiachwe kwa klabu peke yake, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kwa kushirikiana na TFF, wanaweza kuandaa madarasa maalumu kwa ajili ya kuwaongezea uelewa wachezaji, kwa sababu zinafahamu uwezo halisi wa vilabu vyake.

Tunaamini kuwa, kwa kufanya hivi, sio tu, Ligi Kuu Tanzania Bara itakuwa yenye wachezaji wanaojitambua, pia serikali itakuwa imewaandaa wachezaji "waliokamilika" ambao wataitumikia Timu ya Taifa (Taifa Stars).


Ni ukweli kuwa, idadi kubwa ya wachezaji wanaounda Kikosi cha Taifa Stars wanatoka kwenye Ligi Kuu (ukiangalia takwimu za Kundi C kwenye Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon), Tanzania ilikuwa na wachezaji wa ndani 14, Kenya wachezaji 9, Algeria ilitoa nyota mmoja wakati Senegal yenyewe haikuwa na hata mchezaji mmoja anayecheza nyumbani, hivyo jitihada zinahitajika kuwaandaa vema wachezaji wanaoshiriki ligi hiyo.

Mafanikio yoyote yanahitaji uwekezaji uliokamilika, endapo wachezaji wanaoshiriki Ligi Kuu Bara wataandaliwa vema, tuna hakika Tanzania itakuwa na wachezaji wenye viwango vizuri ambavyo vitasaidia kuifanya Taifa Stars iwe na uwezo wa kushindana na si kushiriki kwenye mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Kama tutabadilika na kuwekeza vema, Afcon ijayo Tanzania itakwenda ikiwa imara na yenye kuogopewa na timu za mataifa mengine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mashabiki wanapopenda wachezaji kuliko klabu

Na Adam Fungamwango

**KATIKA** miaka ya hivi karibuni, kumezuka kizazi cha baadhi ya mashabiki wa soka kupenda zaidi wachezaji kuliko klabu zao.

Haijulikani kwa nini, lakini baadhi ya mashabiki kwa sasa wameonekana wakiumia mno baadhi ya wachezaji wakiondoka kwenye klabu zao kwenda kutafuta malisho sehemu nyingine.

Kwa kawaida mchezaji ni kama mfanyakazi ambaye analetwa kwenye kampuni kuitumikia kwa muda ambao wamekubaliana na mwajiri wake, na mkataba ukimalizika, wanaweza kukaa na kuamua kuendelea au kutoendelea.

Na hapa inawezekana mwajiri asiridhishwe na huduma ya mfanyakazi wake akaamua kumuacha, au mfanyakazi asitake tena kuendelea hapo, ama kuamua kubadilisha upepo na kwenda sehemu nyingine.

Hiyo ndiyo ipo hata kwenye soka. Lakini kwa Tanzania sasa eti linaanza kuonekana jambo la ajabu na baadhi ya mashabiki kuanza kuwalaumu na kuwashutumu wachezaji wanaoondoka, kuhama, pia wapo wanaowalaumu viongozi wa klabu eti kwa nini wamewaacha wachezaji.

Nitoe mifano ya hili. Ibrahim Ajibu na Gadiel Michael wameondoka Yanga baada ya kumaliza mikataba yao, na wakajiunga na klabu ya Simba.

Kuna baadhi ya mashabiki wamekuwa wakitoa maneno ya kejeli, shutuma kisa kwa nini nyota hao wamehama.

Hii ikasababisha mpaka Gadiel aandike waraka wa kuwaomba radhi baadhi ya mashabiki wa Yanga wenye 'nongwa'. Sidhani kama mchezaji huyo alipaswa kufanya hivyo kwa sababu hakuna lolote baya ambalo amelifanya.

Ni kwamba mkataba na klabu umekwisha na yeye binafsi hakuwa na mpango wa kuongeza, akili yake tayari ilikuwa kwingine.

Tunakwenda kwenye klabu ya Simba. Emmanuel Okwi ameamua kuondoka. Baadhi ya mashabiki wamekuwa akimwandikia waraka mkali kuwa hajaitendea haki klabu ya Simba kwa sababu ndiyo iliyompa jina na kwa nini ameiacha kwa staili hiyo?

Ni kwamba amemaliza mkataba na Simba na ameamua kufuata malisho sehemu nyingine.

James Kotei na Haruna Niyonzima wameondoka baada ya kumaliza mikataba yao, lakini baadhi ya mashabiki wanawashutumu viongozi kwa nini wamewaacha.

Ukiangalia haya yote, sababu yake ni moja tu. Imefikia wakati mashabiki wanawapenda zaidi wachezaji kuliko klabu. Ndiyo maana wakiondoka wanaumia. Wanatoa maneno ambayo hayastahili.

Yeyote anayependa klabu, anajua kuwa watakuja wachezaji wazuri, wenye vipaji, wanaoweza kuwa tegemeo kwa timu, lakini mwisho wa siku wataondoka na kuiacha klabu ikiwa pale pale, ikisajili wachezaji wengine na maisha yanaendelea.

Ndiyo maana leo Yanga haina kina Mbuyu Twite, Vicent Bossou ambao walikuwa tegemeo kubwa, lakini kwa sasa hata kuna baadhi ya mashabiki wameshaanza kuwasahau.

Walikuwapo kina Ben Mwalala na Boniface Ambani, mastraika hatari sana ambao Yanga iliwahi kuwa nao miaka ya hivi karibuni tu, lakini wamesahaulika, hivyo kuondoka kwa Heritier Makambo na Ajibu hakuwezi kuiathiri, Yanga, itaendelea kuwapo.

Mashabiki wa Simba wakumbuke kuwa timu yao ilishawahi kuifunga Yanga mabao 3-1, Okwi akiichezea Yanga, hivyo sidhani kama kuondoka kwake kunaweza kuwa pengo kubwa na haiwezi kufanya chochote bila yeye.

Niyonzima hakucheza kipindi kirefu kwenye mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu na Simba ilipata matokeo, alianza kuonekana kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita, leo hii baadhi yao wanaona kama hakuna maisha ya Simba bila mchezaji huyo.

Hata kwenye miaka ya '70, '80 hata '90 kumetokea wachezaji bora kabisa wa klabu hizo na kuzipa sifa kubwa zilizonazo kwa sasa, lakini kwa sasa hawapo, lakini zenyewe zipo na zinaendelea kupata wachezaji bora kila kukicha.

Kikubwa ni kuzisapoti klabu na kuachana na tabia ya kupenda zaidi wachezaji, kwani wao wanaingia na kutoka, lakini zenyewe zinabaki vile vile.

# MJADALA/BARUA

## Uchafuzi huu Tandale haukubaliki

**Mhariri habari**

*NINAJITOKEZA kwa mara ya kwanza katika gazeti letu hili lilolo na kurasa iliyo mahsusi kwa lengo la kutuwezesha tueleze kero na dukuduku mbalimbali tulizo nazo ili ziwafikie wahusika kwa minajili ya kutatuliwa.*

*Mimi ni mkazi wa Tandale jijini Dar es Salaam. Ninakerwa kwa kweli na tabia iliyoenea katika eneo letu inayofanywa na baadhi ya wakazi wenzetu ya kujisaidia ovyo haja ndogo kwenye chupa za maji. Mbaya zaidi wakishajisaidia kwenye chupa hizo za maji huzitupa ovyo kwenye barabara za mitaa mbalimbali na kuziacha bila hata ya kufikiria madhara yake katika suala zima la uchafuzi wa mazingira, lakini pia kwa kuhatarisha afya za wakazi wenzao.*

*Tatizo hili limekuwa ni la muda mrefu na inaonekana kama vile halijapatiwa ufumbuzi pengine kutokana na kufanyika kwa kificho na hasa nyakati za usiku na hivyo kusababisha ugumu kwa sisi wananchi kuwaona wahalifu hao.*

*Ninaomba kupitia kwako Mhariri watu hawa wasio wastaarabu waache tabia zao hizo. Vilevile naziomba mamlaka za kiserikali zilizo katika eneo letu zilishughulikie suala hili kwa ukamilifu kwani linatuathiri kiafya.*

**Muathirika-Tandale**

## Walezi tusifuge tabia zisizokubalika

**Mhariri**

*KWA kweli kuna tabia ambayo inanishangaza sana mimi ya baadhi ya wazazi na walezi katika jamii yetu hii ya Kitanzania ambao kwa kiasi kikubwa hawako tayari kusikiliza ushauri wanaopewa na majirani zao juu ya tabia za watoto wao.*

*Katika mtaa ninaoishi hapa Mbalizi mkoani Mbeya, kuna jirani yangu aliye na mtoto mwenye tabia zisizokubalika katika jamii ya wastaarabu na hata katika mwenendo wa kawaida wa maisha ya watu. Mtoto wake huyu ana tabia ya kukwapua mali za watu na hata kukaba hasa nyakati za usiku na mchana kwenye maeneo yasiyo na watu. Anafanya uhalifu huu kwa kushirikiana na vijana wanaotoka maeneo mengine ya jiji hili la Mbeya.*

*Lakini cha kusitikisha zaidi ni kuwa kwa majirani ambao wameshawahi kwenda kuwaeleza wazazi wake juu ya uhalifu anaoufanya kijana wao, mara nyingi wamekuwa wakikataa kuwa kijana wao hana tabia hiyo.*


*Kwamba wanaoenda kulalamika kwao wanamuonea gere kijana wao kutokana na maendeleo anayoyafanya. Naomba serikali ya mtaa wetu ichukue hatua ya kumkanya kijana huyo ili aachane na tabia hiyo kwani inaweza ikamhatarishia maisha yake siku moja na hasa pale wananchi watakapojichukulia sheria mkononi.*

**Jason Mandyanga- Mbalizi**


### WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz


# Ndayiragije anakwenda kupoteza sifa yake Stars?




**Na Adam Fungamwango**

HAKUNA shabiki yeyote wa soka la Tanzania anayepinga kuwa kocha raia wa Burundi, Etienne Ndayiragije ni mmoja wa makocha wenye sifa kubwa kwa sasa.

Sifa yake ilianza alipoiwezesha timu ya Mbao FC kuwa moja ya timu tishio kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mara tu baada ya kupandishwa na Shirikisho la Soka nchini (TFF) kuchukua nafasi ya Geita Gold Mine FC ambayo ni moja kati ya timu zilizobainika kupanga matokeo.

Mbao FC ikiwa imeshtukizwa tu, ilianza kucheza Ligi Kuu msimu wa 2016/17, kila mmoja akiipa nafasi ndogo ya kubaki.

Kilichotokea ni kwamba, mbali na kwamba haikuteremka daraja, lakini ilikuwa ni mwiba mchungu kwa timu kongwe za Simba na Yanga.

Nyuma ya timu hiyo, ilibainika kuwa kuna mtu anaitwa Ndayiragije, ambaye alikuwa na wachezaji wasio na majina, lakini aliwageuza na kuwa bidhaa adimu kiasi cha kugombaniwa na klabu mbalimbali nchini.

Hata walipoondoka msimu wa pili, Mbao FC ilibaki vile vile kuwa timu ngumu, ikiendelea kufanya maajabu.

Hilo liliwashtua viongozi wa KMC ambao timu yao ilikuwa imepanda daraja, ikaamua kumchukua.

Tangu alipoondoka Mbao FC, msimu uliopita haikuwa kama ile iliyozoeleka na iliponea chupuchupu kushuka daraja, huku upande wa pili KMC kwa msimu mmoja tu nayo ikawa kama Mbao FC mpya.

Na haikushangaza kushika nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu na kupata nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Ndayiragije alikuwa nyuma ya yote hayo. Azam FC nayo ikaamua kumng'oa kutoka KMC na kumpeleka Chamazi. Bado hajaonyesha chochote japo timu ipo kwenye michuano ya Kombe la Kagame, lakini mashabiki wengi wanamwamini mno.

Na hilo ndilo lililosababisha hata TFF kumteua kuwa Kocha Mkuu wa muda wa Taifa Stars akiiongoza kwenye michuano ya kufuzu Kombe la Afrika kwa wachezaji wa ndani (CHAN).

Binafsi sina wasiwasi na uwezo wa kocha huyo, lakini tatizo ni kwamba soka la Tanzania hasa katika kikosi cha Stars linatawaliwa mno na siasa kuliko uhalisia.

Linatawaliwa na siasa za kila aina zikiwamo za U-simba na U-yanga. Hofu yangu ni kwamba, kama Ndayiragije mwenyewe kama hakukaa vizuri basi kuna anguko la umaarufu wake mbele ya safari.

Tatizo ni kwamba kuna aina fulani ya kutaka kuridhisha watu kwenye kuchagua wachezaji wa Stars. Kuna wachezaji vipenzi vya mashabiki ambavyo kama kocha huyo hakuwachagua tatizo litaanzia hapo hapo. Ni lawama kuanzia mwanzo hadi mwisho. Na wanakuwa wanaiombea mabaya timu.

Kingine ni uwiano wa wachezaji wa Simba na Yanga. Huyu huyu Ndayiragije anaweza kuwa "mbaya" kama atachagua wachezaji wengi kutoka Simba au Yanga. Timu yenye wachezaji wachache kwa jinsi ninavyowafahamu mashabiki wa Kibongo wataanza kuhoji, maswali kibao, kununa na hata kuisusa timu.

Hapo sasa ndipo linapokuja suala ya uchaguzi wa wachezaji kisiasa na si kwa uwezo wa wachezaji.

Na ikizingatiwa kuwa safari hii ni wachezaji wa ndani tu na kina Mbwana Samatta na Simon Msuva hawahusiki.

Wakati mwingine kuteua wachezaji kwenye timu ya taifa kwa kufuata uwezo wa mchezaji kunaweza kuleta mgawanyiko wa mashabiki wa soka nchini.

Kwa haya yote niliyoyaorodhesha hapa ndiyo yanayofanya Ndayiragije awe na wakati mgumu mno kwenye kikosi cha Taifa Stars.

Stars si Mbao FC, KMC wala Azam FC, huku aliko sasa kuna "siasa" zaidi kuliko kutafuta wachezaji wa kweli wanaliofanya vema kwenye klabu zao na ambao viwango vya viko juu bila shaka yoyote.

Anaweza kuteua wachezaji anaowataka yeye bila kujali chochote kitakachotokea, wala kuteua wachezaji vipenzi vya mashabiki, lakini timu itakapofanya vibaya, atazikoga lawama kama ilivyokuwa kwa Emmanuel Amunike.

Lakini kama ataingia kwenye siasa inaweza kumsaidia kwa muda mashabiki wengi wakaridhishwa naye, lakini kwa bahati mbaya timu ikifanya vibaya ikiwa na wachezaji wao vipenzi ndani, hao hao mashabiki watamgeuka yeye na kusema tatizo si wachezaji ila ni kocha kwa sababu amezoea kuzifundisha timu kama Mbao FC na KMC tu na si Taifa Stars.

## KABWELA — NA FADHILI MOHAMMED



# W'biashara wawekewa mfumo kuondoa kero

INATOKA UK. 5

barabara, elimu, afya, maji na shughuli nyingine nyingi," aliongeza.

Hata hivyo, alisema mazingira ya kufanyia biashara bado siyo mazuri, hivyo serikali inaendelea kuyafanyia marekebisho ili kujenga mazingira rafiki na mazuri zaidi.

Alisema katika hatua ya awali serikali imefuta tozo zipatazo 54 ambazo zilikuwa ni kero kubwa kwa wafanyabiashara kuanzia bajeti ya mwaka wa fedha wa 2019/2020. Alifafanua kuwa kulikuwa na kodi nyingi ambazo zilikuwa kero na mzigo kwa wafanyabiashara ambapo alisema ilifikia bidhaa moja kutozwa kodi na taasisi zaidi ya moja. Aidha, Manyanya aliwataka wafanyabiashara na wajasiriamali kutokatishwa tamaa na vikwazo vinavyojitokeza hususan vinavyosababishwa na baadhi ya watendaji serikalini. Katika hatua nyingine, Manyanya aliwaagiza viongozi wa serikali katika mikoa yote kuhakikisha wale wote waliochukua mikopo kutoka Sido wanairejesha mara moja ili fedha hizo ziwanufaishe wakopaji wengine.

Alisema kwamba fedha walizokopa siyo zawadi bali ni mtaji kwa ajili ya kuwawezesha kukuza zao.

Akitoa ufafanuzi wa malalamiko mbalimbali ya wafanyabiashara na wajasiriamali yakiwamo ya usumbufu wa kukata leseni, Meneja wa Sido mkoa wa Arusha, Nina Nchimbi, alisema kila biashara ina mfumo wake wa kupata leseni kutoka mamlaka zinazohusika.

Alisema Sido siku zote imekuwa ikifanya kazi zake na taasisi mbalimbali za serikali zikiwamo halmashauri za wilaya, manispaa na majiji, Mamlaka ya Mapato Tanzania (Tra), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA).

Nchimbi alisema Sido itaendelea kuendesha mafunzo kwa wajasiriamali kabla ya kuanza mradi ama kupata mkopo kwa lengo la kuwajengea uwezo kibiashara. Alivitaka viwanda vinavyotengeneza vifungashio nchini kuhakikisha vinatenga dirisha kwa ajili ya kuwahudumia wajasiriamali wadogo bila vikwazo.

Baadhi ya wafanyabiashara na wajasiriamali walilalamika kwamba baadhi ya watendaji katika taasisi za umma wamekuwa wakitoa maelekezo kwa vitisho.

Walisema wapo baadhi ya wanasiasa na watendaji serikalini wamekuwa kikwazo kikubwa katika kuwawezesha wajasirimali kufanyabiashara zao kwa ufanisi na tija zaidi kutokana na kuwapo sheria na kodi nyingi ambazo zimekuwa kikwazo bila kujali mapato yao halisi.



Muuguzi Mkuu Hospitali ya Rufani ya Mkoa-Amana, Beauty Mwambebule, akitoa maelezo kwa wageni kutoka nchi ya Bangladesh namna mfumo wa Kaizen unavyofanya kazi katika hospitali hiyo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA**

# Wajasiriamali waliofanya vizuri watafutiwa fursa

INATOKA UK. 5

utoaji wa ajira kutokana na maendeleo na huduma za kifedha kwa wajasiriamali katika mikoa sita nchini," alisema. Mikoa iliyofaidika na mradi wa TLED ni Shinyanga, Mwanza, Lindi, Mtwara, Iringa na Njombe, huku malengo mahsusi ni kuhakikisha mnufaikaji wa mradi huo anapatiwa elimu na ushauri kutoka kwa timu ya washauri wakuu (wanaojitolea) na wafanyakazi wa mradi. Aidha, aliongeza kuwa TLED uhakikisha wanufaikaji wa mradi huu wanaunganishwa na soko la biashara zao, upatikanaji wa teknolojia na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuendeshea biashara hizo.

Awali ofisa huyo alielezea malengo ya mradi huo ni kufikia wajasiriamali 1,760 mpaka ukomo wa mradi huo, ambapo kwa sasa mradi huo umeweza kuwafikia watu 1,361 sawa na asilimia 77 ya walengwa wote wa mradi.

Kupitia maonyesho haya ya Sabasaba tumeyatumia kuwapa fursa wajasiriamali kujifunza kwa kuona wenzao wanafanya nini na kuzitangaza biashara zao kimataifa kupitia jukwaa hili la maonesho ya Sabasaba, aliongeza Jemima Michael. Careen Charles, mjasiriamali wa kutengeneza mikoba asili kutokea Shinyanga ameushukuru mradi wa TLED kwa kumpa fursa ya kushiriki katika maonyesho ya Sabasaba, na kumsaidia kupata soko la biashara zake la uhakika.

# Benki zaunga mkono BoT kibano kwa wasumbufu

INATOKA UK. 2

alisema Myonga.

Alisema sehemu nyingine ya matatizo ya mikopo ni pale mteja anapotaka kuhama kutoka benki moja kwenda nyingine, kwa ajili ya kutafuta ahueni ya mkopo wake.

"Kwa hiyo huwa inafika mahali mkopaji akitaka kuhamia katika benki nyingine kwa ajili ya kutafuta ahueni ya mkopo wake, benki husika ambayo amekopa humwekea masharti magumu ilimradi tu ashindwe, na mwisho wa siku ndiyo kutengeneza mazingira ya kukimbilia kupiga mnada mali zake," alisema Myonga.

"Benki nyingi hazitoi fursa kwa wakopaji 'kurestructure' mikopo yao baada ya kuyumba kiuchumi, badala yake yanakimbilia kupiga mnada mali na hiyo pia inachangia na namna ambavyo mikataba ilivyoandikwa, haitoi fursa hiyo."

Alisema tatizo jingine linalochangia migogoro ya mikopo ni wakopaji wenyewe kukimbilia kutia saini mikataba ya mikopo yao bila kusoma vilivyoandikwa katika mikataba hiyo, hivyo mwisho wa siku hujikuta wanaingia katika matatizo husussan wanapobaini kwamba walichokisaini hawawezi kukitekeleza.

"Tatizo wakopaji wengi huwa wanakimbilia kusaini kitu ambacho hawakijui, wakikimbilia kupatiwa pesa harakaharaka bila kusoma kilichoandikwa kwa hiyo baadaye inawaletea matatizo," alisema Myonga.

Tatizo jingine ambalo alisema linachangia migogoro ya mikopo katika benki nyingi ni lugha inayotumika katika kuandika mikataba ya mikopo, kutokuwa na elimu ya mikopo kwa wakopaji na maandishi madogo yanayoandikwa katika mikataba hiyo.

"Kwa hiyo BoT imetengeneza sheria mpya ya 2018 ambayo inasubiri kanuni ambazo wakati wowote zitakamilika na kuanza kufanya kazi, hizi zitakuwa suluhisho la kumlinda mteja na huduma za kibenki," alisema Myonga.

Alisema pia itatoa fursa kwa mkopaji kuwa na nafasi ya kujiridhisha na kile kilichoandikwa kwenye mkataba wa mkopo kwa muda wa saa 24 hadi siku tatu na kufanya uamuzi wa kukubali au kukataa.

"Pia kutakuwa na mfumo wa kurestructure mkopo kwa ajili ya kumsaidia mkopaji anapopata mtikisiko wa kiuchumi," alisema.

Pia alisema sheria hiyo itatoa fursa kwa BoT kutembelea taasisi za fedha kuangalia au kukagua na kujiridhisha kama zinatekeleza kanuni za kuwalinda wateja na mwongozo wa BoT.

Kwa takribani miaka mitatu kumekuwapo na kasi kubwa ya wateja wengi wa benki kujikuta katika wakati mgumu kiuchumi, hivyo benki walizokopa kuuza kwa mnada mali zao zikiwamo nyumba, magari, mashamba na viwanja.

# Makamba, Kinana waibuka na mazito

INATOKA UK. 2

wakuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuwa wanamhujumu Rais na amefanya hivyo bila kujali athari ya kauli zake kwa Muungano wetu."

Taarifa hiyo ilisema viongozi hao hawahusiki kwa namna yoyote na shutuma zilizotolewa na mwanaharakati huyo na kudai zimeandaliwa kwa malengo maalum ya kuwadhalilisha, kuwavunjia heshima, kuwajengea chuki na kuwachafulia majina ndani na nje ya chama.

"Tunawasihi Watanzania kuzipuuza, kuzidharau na kuzinyanyapaa, ikiwamo kuwa makini na yanayoandaliwa na wanaomtuma kwa kuwa wanaipeleka nchi mahali pabaya kwa mwavuli wa kumsaidia Rais," walibainisha.

"Tunasikitika kwamba licha ya kuwatuhumu na kuwakashifu Watanzania wenzake, viongozi na watendaji kwenye serikali, taasisi za umma, za kijamii na sekta binafsi, ameachwa akitamba, hata anapotumia lugha za vitisho na za kuhatarisha usalama wa raia hakuna hatua zinachukuliwa dhidi yake," taarifa hiyo ilieleza.

Wastaafu hao katika taarifa yao wanauliza mwanaharakati huyo anatumwa na nani, anakingiwa kifua na nani, anatumika kwa malengo gani.

Walisema tafakuri yao ni kwamba kuna ushahidi wa kimazingira mwanaharakati huyo anatumwa na mtu mwenye uwezo wa kumlinda na kumkingia kifua bila kuhojiwa na taasisi yoyote wala mtu yeyote.

Vile vile, walidai zipo ishara kwamba wanaomkingia kifua wana mamlaka, baraka na kinga ambazo wamepewa ili kutekeleza majukumu maalum.

"Anatumika kwa malengo ya kuwazushia, kuwakejeli, kuwavunjia heshima, kuwatia hofu na kuwanyamazisha viongozi, taasisi na watu ambao ni walengwa waliokusudiwa," walisema na kuongeza:

"Kuna kila dalili lengo na hatima ya mkakati huu ni

# Wamiliki shule binafsi wataka uchunguzi

INATOKA UK. 3

Aidha, wamiliki wa shule wanashindwa kutimiza wajibu wa kuwapa mafunzo madereva jambo linalosababisha ajali kuongezeka, mmomonyoko wa maadili na kuharibu saikolojia za watoto.

Taasisi hiyo ilipendekeza kuwa endapo dereva ataendesha gari la shule bila cheti cha Apec Driving School, baada ya ukaguzi wa maofisa elimu kata wasiruhusiwe kuendesha wanafunzi.

Kwa mujibu wa barua hiyo mafunzo hayo yalianza Mei mwaka huu katika majiji ya Dar es Salaam, Arusha na mkoa wa Kilimanjaro.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Mtendaji Mkuu Taasisi ya Ubunifu Tanzania (EIT), Benjamin Nkonya, alisema inashangaza kwa uchaguzi wa shule za kutoa mafunzo hayo kusahau kuwa wanafunzi wengi wako kwenye shule za umma.

"Hatuelewi kwamba nia ni kutoa mafunzo au kuna jambo jingine, wamefanya utafiti gani na wapi na matokeo ni yapi ambayo yamewafanya waone shule binafsi ndiyo zinastahili kupewa mafunzo hayo, wanafunzi wa shule za umma wanaopanda daladala wanaathirika kisaikolojia sana," alisema na kuongeza:

"Sio mara ya kwanza kwa taasisi kama hizi kuja kutoa mafunzo na wanatutoza fedha nyingi sana, mfano miaka ya nyuma kuna taasisi ilikuwa inatoza Sh. 300,000 kwa dereva mmoja na mafunzo yenyewe hatuonyeshwi mitaala na hatuoni umuhimu wake."

Naye, Mwenyekiti wa Tomongsco, Jeremia Gwejeneza, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu alisema wamepokea barua hiyo, lakini wanaomba serikali kuliangalia upya suala hilo.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Fortunatus Musilimu, alipotafutwa kujua kama wametoa kibali cha mafunzo hayo, simu yake iliita bila kupokelewa na ujumbe mfupi wa maandishi haukujibiwa.

# Wakurugenzi, wakuu wa idara waonywa kukaimisha

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Everist Ndikilo, amewataka wakurugenzi na wakuu wa idara katika wilaya za mkoa huo kuacha tabia ya kuwakaimisha watumishi kuingia katika mikutano ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,(CAG) kwa ajili ya kujibu hoja ambazo zinatakiwa kujibiwa na wakuu wa idara na wakurugenzi.

Ndikilo aliyasema hayo katika kikao maalumu cha Baraza la Madiwani, Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, ambacho kiliandaliwa kwa ajili ya kujibu hoja 32 za nje za CAG.

"Hoja zinatakiwa kujibiwa na wakuu wa idara na wakurugenzi na sio katika mikutano ya kujibu hoja wanakaimishwa watu kujibu badala ya kuwapo wakuu wa idara na wakurugenzi," alisema.

Aliongeza kuwa mtu kama sio mtaalamu hawezi kujibu hoja na hali hiyo inachangia halmashauri kupata hati chafu.

Ndikilo aliipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga kwa kupata hati safi mara tatu mfululizo.

Alisema kupata hati safi kunaonyesha jinsi ushirikiano uliopo ni mzuri baina ya mkurugenzi, wakuu wa idara na madiwani kwa kusimamia fedha za maendeleo kiufasaha.

Alisema halmashauri za wilaya zote za mkoa wake zimefanikiwa kupata hati safi.

Alisema kupata hati safi kunaonyesha jinsi ilani ya chama tawala inavyotekelezwa katika kusimamia masuala ya maendeleo.

Alizitaka halmashauri zote za mkoa huo ziepuke kuingia mikataba na mawakala wasio waaminifu ambao wanaweza kukusanya mapato na kutokomea na fedha.

Pia Ndikilo aliziangiza halmashauri za mkoa huo, ziendelee kutoa ushirikiano pale wakaguzi wanapofika katika ofisi zao kuanzia kuingia hadi kutoka.




Ofisa Mkuu wa Wateja Wadogo na Wakati wa NMB, Filbert Mponzi, akizungumza na wachimbaji wadogo wa madini wa Geita katika Jukwaa la Mtaji wa Maendeleo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri: Uhifadhi vyanzo vya maji Mto Rufiji wa kudumu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema imejipanga kuhakikisha vyanzo vyote vya maji vinavyotiririsha maji kuelekea Mto Rufiji, vinatunzwa na kulindwa wakati wote sambamba na ujenzi wa mradi mkubwa wa umeme wa Stiggler's Gorge.

Akizungumza baada ya kutembelea eneo la mradi huo mwishoni mwa wiki akiwa ameambatana na maofisa waandamizi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), January Makamba, alisema vyanzo ya maji vya Mto Rufiji ni muhimu, hivyo lazima vilindwe wakati wote.

"Utunzwaji na ulinzi wa vyanzo vya maji vinavyotiririka kuelekea Mto Rufiji ni muhimu kwa ustawi endelevu wa ujenzi wa mradi mkubwa wa kuzalisha umeme ambao utakuwa na manufaa makubwa kwa nchi," alisema Makamba.

Makamba alisema NEMC imeshafungua ofisi yake eneo la ujenzi wa mradi wa uzalishaji umeme eneo hilo la Stiegler's Gorge ili kuhakikisha ujenzi wa mradi huo haukwami wala kusababisha athari zozote za kimazingira.

"Kuwapo kwa wataalamu wa mazingira katika eneo la mradi kutasaidia kurahisisha hupatikanaji wa huduma za haraka pale zitapohitajika na kufanya ufuatiliaji wa karibu wa hatua za maendeleo ya mradi na hali ya mazingira kwa ujumla," alisema.

Makamba aliwataka wananchi wanaoishi kandokando ya mito inayotiririsha maji kwenye Mto Rufiji kuzingatia hifadhi ya mazingira katika matumizi ya maji pamoja na kuyatumia kwa namna endelevu kwani mahitaji ya maji ni makubwa.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema kama Baraza litaendelea kuhamasisha pamoja na utoaji wa elimu juu ya utunzaji wa mazingira ili kutimiza azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Tumejipanga kutoa elimu na kuhamasisha Watanzania kuhusu namna bora ya utunzaji wa mazingira na kuyafanya kuwa endelevu kwa ustawi wa watu wote na nchi kwa ujumla wake," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema kuwa mradi utaleta faida kubwa kwa maendeleo ya Tanzania siyo kwa uzalishaji umeme pekee bali pia kuimarisha sekta na utalii na kuwaomba Watanzania kuendelea kumuunga mkono Rais John Magufuli.

Naye Meneja wa Pori la Akiba la Selous, Henock Msoche, alisema wamejipanga kuhakikisha kuwa watumishi wote katika eneo hilo wanalindwa wakati wote wa utekelezaji wa mradi.

Mradi wa umeme wa Stiegler's Gorge unategemewa kuzalisha megawati 2,100 za umeme mara utakapokamilika na hivyo kuondoa kabisa tatizo la umeme nchini na kufanikisha azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati kupitia viwanda ifikapo mwaka 2025.

## NHIF yabaini udanganyifu wa mil. 65/-

**Na Dege Masoli,** KOROGWE

ZAIDI ya Sh. milioni 65 zilizokuwa zilipwe katika vituo vya kutoa huduma ya Bima ya Taifa ya Afya (NHIF) mkoani Tanga kwa kipindi cha mwaka 2018/2019 zimeokolewa baada ya kubainika kuwa madai hayo ni ya udanganyifu.

Akizungumza kwenye ufunguzi wa kikao kazi cha waratibu wa bima mkoa, Meneja wa Mfuko wa NHIF, Mkoa wa Tanga, Ally Mwakababu, alieleza jumla ya shilingi 65,155,468 ambazo zilikuwa zilipwe na vituo vya kutolea huduma kwenye mwaka huu zimeokolewa baada ya kubainika kuwapo na udanganyifu.

Katika kikao hicho kilichofanyika jana Mjini Korogwe, Mwakababu alisema mwaka wa fedha 2018/2019 waliokoa fedha hizo ambazo zingeweza kuhujumiwa kutokana na madai ya kughushi ambayo vituo vilitaka kuyalipa baada ya kufanya ukaguzi wa kushtukiza wa madai hayo na kubaini kuwapo kwa udanganyifu huo.

Alisema vituo ambavyo vilifanyiwa ukaguzi ni 28 kati ya hivyo 20 ni vya serikali na nane ni vya madhehebu ya dini, hivyo alivitahadharisha vituo hivyo kufuata miongozo na taratibu zilizowekwa za tiba kabla havijachukuliwa hatua ya ukiukwaji wa kanuni, taratibu na sheria zilizopo.

"Mfuko huo umefanya juhudi kubwa kwa kushirikiana na wadau wengine kwenye vituo vinavyotoa huduma ambapo kwa mwaka 2018/2019 mfuko huo umelipa vituo vya serikali shilingi bilioni 3.7 sawa na ongezeko la milioni 427.7 asilimia 11, hivyo kuna maendeleo makubwa huku huduma zikizidi kuboreka mkoani Tanga," alieleza Makababu.

Awali akizungumza wakati akiwasilisha mada ya majukumu ya waratibu wa mfuko huo, Ofisa Udhibiti Ubora, Dk. Mussa Sendama, alielezea umuhimu wa kutambua makundi yenye uhitaji kwani kufanya hivyo ni kutaka kusaidia na kuwezesha mfuko huo kusonga mbele.

# Hospitali ya wilaya yakosa X-ray kwa miaka mitatu

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

HOSPITALI ya Mkomaindo iliyopo Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara haina huduma ya mashine ya X-ray kwa zaidi ya miaka mitatu, hali inayosababisha wagonjwa kusafiri umbali mrefu kwenda hospitali ya misheni Ndanda kufuata huduma hiyo.

Mganga Mkuu wa hospitali hiyo, Dk. Musa Rashidi, aliyasema hayo juzi na kufafanua kuwa hali hiyo imetokana na ya mashine iliyokuwapo kupata itilafu ya vipuri na haijatengenezwa.

Alisema kutokana na changamoto hiyo, hivi sasa wagonjwa wote wanaokwenda kwa ajili ya kupatiwa huduma hiyo katika Hospitali ya Mkomaindo wanalazimika kuwaeleza waende katika hospitali binafsi kwa ajili ya kupata huduma ya X-ray.

Dk. Rashidi alisema mashine hiyo ni ya muda mrefu na haiendani na teknolojia ya sasa kama mashine zilizopo kwenye hospitali zingine nchini, ambazo kwa teknolojia ya sasa ndizo zinahitajika kutoa huduma kwa wagonjwa.

"Wastani wa wagonjwa wanaofika katika hospitali yetu kwa ajili ya kufuata huduma ya X-ray inategemea, lakini wanafika kati ya 25 hadi 30 kwa siku na tunawaeleza waende kwenye hospitali binafsi ili wakapate huduma hii kwa kuwa hapa hatuna huduma hii," alisema Dk. Rashidi. Alisema Hospitali ya Mkomaindo kwa sasa inapokea wagonjwa wengi kutoka maeneo mbalimbali ikiwamo wilaya za Nanyumbu, Newala, Nachingwea na baadhi yao kutoka Msumbiji, na kwamba uwezo wa baadhi ya vifaa tiba huhudumia wagonjwa wengi kwa siku ni mdogo.

Dk. Rashidi alisema kufuatia changamoto hiyo uongozi wa hospitali hiyo umeamua kuomba mashine nyingine ya kisasa kwa kuomba mkopo kupitia Mfuko wa Bima ya Afya, lakini hadi sasa hawajaletewa mashine hiyo.

Mmoja wa wagonjwa aliyefika kupata huduma hiyo, Ayubu Yazidu, alisema kukosekana kwa huduma hiyo imekuwa ni changamoto kwa wananchi.

Alisema wanalazimika kwenda katika hospitali binafsi ya misheni Ndanda kufuata huduma hiyo ambapo ghalama za matibabu ni kubwa zaidi, hivyo kuiomba serikali kuwasaidia. Alipofuatwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji Masasi, Gimbana Ntavyo, hakuwapo ofisini kwa maelezo kuwa alikuwa nje kwa majukumu mengine.



Ofisa Mawasiliano Mwandamizi wa Tanzania Breweries Limited, Amanda Walter, akitoa mada katika semina kuhusu unywaji kistaarabu kwa askari wa Jeshi la Polisi kutoka Kikosi cha Mbwa na Farasi iliyofanyika katika kiwanda cha Ilala mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkakati wa LATRA wagusa wanawake madereva

**Na Enock Charles**

MADEREVA wanawake wanaoendesha mabasi yaendayo haraka maarufu kama mwendokasi wameupongeza mkakati wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, kuamua kutoa mafunzo kwa wanawake 100 ili waendeshe mabasi ya mwendokasi na mengine.

Akizungumza na gazeti hili, dereva wa mabasi hayo yaendayo Kimara-Kivukoni, Mary Kumalija, amesema yeye kama mojawapo ya madereva waliobahatika kuendesha mabasi hayo, aliupongeza mkakati huo kwa kuwa utasaidia kuongeza idadi ya madereva wanawake na kuwajengea uwezo wa kujiamini.

"Huo mpango unadhihirisha ni jinsi gani wanawake tunaaminika unajua kazi ya udereva inahusisha kubeba roho za watu na kwa hiyo umakini unahitajika... mimi kwa mfano sijawahi kupata ajali tangu nimeanza kazi hii, mafunzo yatasaidia kuongeza idadi ya madereva wanawake na kuwajengea uwezo wa kujiamini," Mary alisema.

Dereva mwingine wa mabasi hayo aliyejitambulisha kwa jina la Catherine, alisema mkakati huo utasaidia kuondoa dhana kuwa kazi ya udereva wa nabasi ya abiria ni ya wanaume pekee, huku wanawake wakijitenga mbali na kazi hiyo. "Hapo nyuma haukuwapo, mimi nilisoma kwa gharama zangu, lakini naupongeza mkakati huu maana tulizoea kazi hizi za kuendesha vyombo vya usafiri wa umma ni ya wanaume huku wanawake wakibaki kuendesha vyombo binafsi," Catherine alisema.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na LATRA mwanzoni mwa mwezi huu, mafunzo hayo yatatolewa kwa madereva wanawake kwa miezi miwili ili waweze kuwa na sifa za kuendesha magari ya abiria.

"Lengo mahususi la mradi huu ni kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo ili kuwajengea uwezo wanawake 100 ambao hivi sasa wana uwezo wa kuendesha magari madogo," ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa madereva watakaofuzu wataweza kuendesha magari ya abiria ikiwa ni pamoja na mabasi ya mradi wa mabasi yaendayo haraka.

Mafunzo hayo kwa mujibu wa taarifa hiyo ya LATRA yanatarajiwa kutolewa katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kilichopo Dar es Salaam, ambapo waombaji wametakiwa kutuma maombi yao kufikia mwishoni mwa mwezi huu.

# Malisho yatishia uhai wa ng'ombe

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAFUGAJI wa Kijiji na Kata ya Bulige katika Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama Mkoa wa Shinyanga, wamesema mifugo yao iko hatarini kutoweka kutokana na kukosekana kwa maeneo ya malisho.

Kukosekana wka malisho kunatajwa pia kuchangia migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Daudi Yona, mwenyekiti wa wafugaji katika kijiji hicho, aliyabainisha hayo walipotembelewa na Shirika la Haki na Ustawi wa Wanyama Tanzania (TAPO) ambalo limekuwa likiwasaidia wafugaji chakula cha mifugo, dawa za vidonda, minyoo na dawa za kulinda ngozi kwa wanyama.

Alisema ukosefu wa maeneo ya malisho katika kijiji chao imesababisha kuibuka mgogoro kati yao na wamiliki wa mashamba ambayo mara nyingi wamekuwa wakiyatumia kulishia mifungo yao baada ya kuvunwa kwa mazao.

Aidha, Yona alisema mifugo imeanza kuathirika kwa kukosa chakula na maji ya kunywa ya kutosha, na kwamba wakati mwingine wamekuwa wakitumia maji ya kwenye madimbwi ambayo yametuama kwa muda mrefu na mifugo inapoyatumia hupata ugonjwa wa minyoo.

Naye Ndilanha Misobi alisema Tapo kwa kushirikiana na serikali wamekuwa wakiwasaidia kuipatia tiba mifugo yao ili kuinusuru na magonjwa ambayo yamekuwa yakitokana na kunywa maji machafu.

Pia alisema wamekuwa wakisaidia kuwapatia chakula cha mifugo kwa kila mfugaji aliyoko katika kijiji hicho sambamba na elimu namna ya kufuga kisasa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi nchini hasa kwa kipindi hiki cha kiangazi.

Ofisa Mifugo wa kata hiyo, Devid Chiloleth, alikili kuwapo kwa changamoto ya ukosefu wa maeneo ya malisho, majosho ya kunyoshea mifugo wakati wakitoka malishoni na kusababisha wafugaji wengi kuwa wa kuhamahama.

# IAA, TPDF wakubaliana shahada ya sayansi ya kijeshi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

CHUO cha Uhasibu Arusha (IAA) na Jeshi la Wananchi Tanzania (TPDF) kupitia Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli (TMA), mwishoni mwa wiki walitia saini mkataba wa pili wa makubaliano wa utekelezaji utoaji wa shahada ya sayansi ya kijeshi (Bachelor of Militry Science).

Akizungumza mwishoni mwa wiki katika Chuo cha Uhasibu Arusha, kwenye hafla fupi ya utiaji saini, Mkuu wa Chuo cha Uhasibu Arusha, Prof. Eliamani Sedoyeka, alisema hayo ni matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya chuo ya kutoa mafunzo kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Bunge iliyoanzishwa na chuo hicho.

Alisema ushirikiano wao na TPDF umekuwa wa muda mrefu tangu lilipopatikana wazo la kuanzishwa kwa ushirikiano baina ya taasisi hizo mbili, Desemba, 2015 waliposaini mkataba wao wa kwanza wa ushirikiano na Novemba 20, 2017 kuzindua rasmi shahada ya sayansi ya kijeshi.

"Shahada hii ina wanafunzi 208 kati yao waliopo mwaka wa pili ni 146 na mwaka wa kwanza 62, lakini mwakani tunategemea kuwa na wahitimu wetu wa kwanza katika shahada hii ya sayansi ya kijeshi," alisema.

Prof. Sedoyeka alisema ushirikiano huo una malengo ya muda mrefu na wanategemea kuongeza kozi mbalimbali katika kuendeleza ushirika huo kwenye utoaji elimu bora kwa jeshi nchini.

Vile vile, alisema IAA kinatoa elimu bora na katika mazingira rafiki kwa kijana, kutokana na kufundisha mitaala mahiri inayozingatia ufundishaji wa vitendo zaidi kuliko nadharia na mitaala hiyo imepata ithibati katika bodi ya kitaaluma.

"Chuo kinahakikisha vijana wanapata elimu bora kwa kuwaboreshea mazingira ya usomaji ili wasaidie serikali kupeleka nchi katika kima cha kati ifikapo mwaka 2025 na kufikia lengo lake la kufanya Tanzania ya viwanda," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa IAA, Juma Kaniki, alisema ushirikiano huo kwao umekuwa na manufaa mengi katika nyanja mbalimbali yakiwamo kuwaletea uhusiano mzuri na jeshi nchini na vyuo vya kijeshi ndani na nje ya nchi.

Pia alitaja manufaa mengine ni kutangaza chuo na kuwapa heshima chuo hicho na kuwawezesha kupokea wanafunzi 208 ambao wapo darasani na wanatarajia kuchukua wengine.

Alitaja manufaa mengine waliyopata ni kuwawezesha kuwajengea uwezo wanafunzi wa TMA watatu ambao wanasoma shahada ya pili chuoni IAA.



Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally (katikati), akimsikiliza Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Manyara, Martha Umbullah (kushoto), aliyeiwezesha shamba kwa kuipa Sh. milioni 2 jumuiya ya UWT Kiteto na kuvuna mahindi Kijiji cha Engusero juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanawake Wakatoliki waanzisha kiwanda cha sabuni

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANAWAKE Wakatoliki Tanzania Jimbo Kuu la Arusha (Wawata), wameamua kuunga mkono juhudi za serikali kwa kuanzisha kiwanda cha kuzalisha sabuni za aina mbalimbali, ili kukuza kipato kwa wasichana waliopata elimu ya shule za msingi na sekondari, pamoja na wanawake wanaolewa katika umri mdogo.

Akizungumza juzi wakati akizindua kiwanda hicho kilichopo eneo la Nanenane Njiro, Mhashamu Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Arusha, Isaack Amani, alipongeza Wawata kwa jududi za kuunganisha nguvu zao na kuanzisha kiwanda hicho.

Alisema uanzishwaji wa kiwanda hicho ni uwajibikaji ambao Rais John Magufuli amekuwa akiimba kila siku, sababu bila kuwajibika kwa kufanya kazi maisha hayawezi kubadilika.

"Ni lazima tuwajibike watu wakubali kubadilika na kufanya kazi ili kuleta mabadiliko katika jamii, hivyo niwapongeze kwa kuwa na fikra za kuunga mkono juhudi za serikali za kupeleka nchi katika uchumi wa kati kwa kuanzisha viwanda," alisema.

Alisema serikali wanachofanya kuhimiza watu kuwajibika ni jambo zuri na kuwajibika ni kubadilisha maisha na inaanza katika fikra na kuamua kuwanaunga mkono serikali, ili watu wajue katika kufanya kazi ndio maisha yanabadilika.

Aidha, aligusia umuhimu wa watu kulinda amani ya Tanzania ambayo ipo na amani hiyo ambayo ipo ni vema ikalindwa ili isipotee kirahisi.

"Ili kulinda amani hii lazima watu waepukane na kuchukizana, kubaguana, kuchokozana na kutotendeana haki na mizozo mirefu na watu wapatane wanapokoseana, tusikae muda mrefu wa kuzozana na kuweka kisasi, kwa kuwa kwa kufanya hivyo inahatarisha amani na tuombee watu wawajibike na tujenge mazingira ya kuhakikisha inakuwa salama kwa kila mtu," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Wanawake Wakatoliki Jimbo Kuu la Arusha, Sara Kessy, alisema wanawasaidia kinamama katika utume wao wa kanisa na wameona bado wanahitaji kutiwa moyo na hasa katika kuitikia wito wa Rais John Magufuli wa uanzishwaji viwanda.

"Tukaona kuna uhitaji wa kufundisha vijana wa darasa la saba, kidato cha nne na wanawake wanaoolewa wakiwa na umri mdogo mafunzo ya utengenezaji sabuni kwa kuanzisha kiwanda hiki ili wajifunze, wajiajiri na kuzalisha viwanda vyao vidogo vidogo au wajizalishe bidhaa zao na kupunguza gharama za matumizi nyumbani mwao," alisema.

Alisema sabuni wanazotengeneza ni za kuondoa madoa, kufulia, za miche, za maji, za kuogea na kufulia na wanaamini kwa kuwafundisha kutengeneza bidhaa hizo watatengeneza ajira na kuwapatia kipato kwa wale waliokwama kupata ajira.

Alisema kwa sasa wanazalisha miche 440 ndani ya siku tatu na sabuni ya maji wanazalisha kwa siku lita 600 hadi 700.

# Malaigwanani walalamikia migogoro hifadhini

**Na Zanura Mollel,** NGORONGORO

VIONGOZI wa kimila jamii ya Kimasai malaigwanani zaidi ya 40, Tarafa ya Ngorongoro, Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha, wamemwomba Rais John Magufuli kubadilisha uongozi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kutokana na kutokuwapo kwa uhusiano mzuri na jamii na kusababisha migogoro ndani ya hifadhi hiyo.

"Awali viongozi wa mamlaka waliokuwapo walikuwa wakikutana na malaigwanani pamoja na viongozi wa baraza la wafugaji na kujadili kuhusu maisha ya wakazi na wanyama na kushauriana namna ya kuendeleza uhusiano mzuri katika hifadhi hiyo," alisema.

Akisoma taarifa fupi iliyoandaliwa na malaigwanani hao jana, Jamse Moringe, laigwanani kutoka Kata ya Alaitole mbele ya Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Arusha, Loatha Sanare, alisema kutokuwapo kwa uhusiano mzuri kumeanza mwaka 2016, baada ya mabadiliko ya uongozi katika mamlaka hiyo.

"Kulikuwa kuna uhusiano mzuri tangu mwaka 1992 hadi 2015, lakini kwa sasa hakuna uhusiano kati ya wahifadhi na wananchi," alisema Moringe.


Alisema malaigwanani wamelaani kuwapo kwa katazo la kujenga nyumba za kisasa na za asili, kuwapo kwa katazo la kujenga shule ambayo ni taasisi za serikali, kunyimwa kutumia vyombo vya moto katika maeneo ya hifadhi ikiwamo gari na pikipiki huku mazingira hayo yakiwa magumu kwa wananchi.

"Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inazungumzia elimu bure, lakini hapa tunanyimwa kujenga shule kwa maana hiyo hakuna wawakilishi wa mheshimiwa rais ngazi ya wilaya hadi mkoa, tunataka kujua hatima yetu watu wa Tarafa ya Ngorongoro," alieleza Moringe na kuongeza:

"Tarafa hii ni miongoni mwa tatu zinazounda Wilaya ya Ngorongoro, ambayo ni Loliondo, Sale na tarafa hii ina vijiji 25 na kata 11 pamoja na wakazi 93,136," alisema Moringe.

Vile vile, alizungumzia kuwapo kwa vijana waliofukuzwa kazi kwenye mamlaka hiyo, huku wakinyimwa ajira wazawa katika tarafa hiyo iliyopo ndani ya mamlaka na kuitaka serikali kutoka tamko rasmi kuhusu vijana wasomi waliopo katika eneo hilo na wale wa darasa la saba waliofukuzwa kazi.

Maria Gutumuhoga, mkazi wa Kijiji cha Olpiro, Kata ya Easi, alikemea kuwapo kwa taarifa zinazosambaa kuwa wanapewa chakula cha bure (mahindi) na huku mahindi hayo yakiwa ni ya bei nafuu.





# Waiomba TIC mwekezaji wa kiwanda cha maziwa

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WAKAZI wa Kijiji cha Manio-Kashashi katika Wilaya ya Siha, wamekitaka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kuwatafutia mwekezaji atakayewekeza katika sekta ya maziwa kwa kujenga kiwanda cha kisasa kitakachochukua kiasi kikubwa cha maziwa yanayoharibika kwa kukosa soko.

Mwenyekiti wa Chama cha Akiba na Mikopo cha Manio Saccos, Edri Kileo, alisema pia wameshaiandikia serikali kuhusu kusudio hilo la kutaka kutafutwa mwekezaji atakayewanusuru wananchi wa eneo hilo na hasara ya kupoteza maziwa kutokana na kukosa soko la uhakika.

"Tunatoa ombi kwa serikali ama wawekezaji kujitokeza na kuwekeza katika kijiji chetu kiwanda cha kusindika maziwa, kwa kuwa wafugaji wengi wanapata hasara kubwa na kupoteza fedha zao kutokana na kutokuwa na kiwanda cha kusindika maziwa," alisema.

Mei 14, mwaka huu, Ofisa Mwandamizi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Maendeleo ya Sekta Binafsi na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi anayeshughulikia mazingira ya biashara, Christopher Mramba, alipokuwa anazungumza na wafugaji wa Mkoa wa Kilimanjaro alisema serikali hivi sasa, imeondoa vikwazo na urasimu usio wa lazima kwa wasindikaji na wazalishaji wa sekta ya maziwa.

Alisema serikali ina nia njema ya kusimamia sekta hiyo kutokana na udhibiti usioridhisha wa biashara.

Mramba alisema: "Serikali inataka mzalishe vizuri na mfanye biashara vizuri bila vikwazo, bila urasimu sio wa lazima. Kwa wale ambao mmezoea kusikia neno urasimu pengine ni neno ambalo sio baya, isipokuwa wanataka kukulazimisha ufuate taratibu hizi na zile."

Vile vile, serikali imeeleza kuwa nia yake ya kusimamia na kutengeneza mazingira mazuri ya kufanya biashara na usindikaji wa maziwa ni pamoja na kutatua kero ambazo wazalishaji wanakutana nazo hasa wasindikaji, wazalishaji wa maziwa.

Mpango huo wa serikali unatokana na udhibiti usioridhisha wa biashara.

"Udhibiti hauna maana ya kuzuia biashara isifanyike, una lengo la kuhakikisha uzalishaji, biashara zinafanyika kwa kufuata kanuni ambazo ni rahisi kuzifuata, hazina mwingiliano wa majukumu," alisisitiza.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni (aliyevaa mavazi ya kiraia), akiangalia moja ya bidhaa zinazotengenezwa na wafungwa katika Gereza la Butimba, jijini Mwanza, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Dk. John Magufuli la kutaka wafungwa watumike katika shughuli za uzalishaji. **PICHA: MPIGAPICHA**

# Wapania kumpelekea PM mgogoro wa ardhi

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WANANCHI wa Kijiji cha Namwai, Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, wanajipanga kumpelekea malalamiko ya mgogoro wa ardhi Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ili aushughulikie kati ya kijiji chao na mwekezaji wa shamba la Kafoi.

Habari zilizopatikana jana na kuthibitishwa na mwenyekiti wa kamati ya kufuatilia utatuzi wa mgogoro wa ardhi wa Kitongoji cha Esimbosi, kilichopo katika kijiji hicho, Daniel Nahumu, alisema wananchi hao watakwenda kumweleza Waziri Mkuu wiki ijayo atakapowasili mkoani Kilimanjaro.

Waziri Mkuu Majaliwa anatarajiwa kuwasili mkoani humo Julai 17, kwa ajili ya kuzindua zoezi la uboreshaji wa daftari la wapigakura.

Pia, kamati hiyo imedai kusikitishwa na kitendo cha Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Dk. Bashiru Ally, kusomewa na kupewa taarifa ya uongo kuhusu kumalizika kwa mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa Kitongoji cha Esimbosi na mwekezaji wa shamba la Kafoi Estate, jambo ambalo si kweli.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Danieli Nahumu, alisema kwa miaka 15 mgogoro huo haujapatiwa ufumbuzi kuanzia ngazi ya wilaya hadi mkoa na kwamba umekuwa ukichangiwa na baadhi ya viongozi wa ardhi Wilaya ya Siha kwa kushirikiana na mwekezaji kupuuza madai ya wananchi.

"Tunakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassimu Majaliwa unapokuja kuzindua zoezi la uboreshaji wa daftari la mpiga kura uingilie kati mgogoro huu wa mpaka kati ya wananchi wa kitongoji chetu na mwekezaji wa shamba la Kafoi Estate," alisema.

Alisema wananchi wanaiomba serikali kuonyesha mipaka ya shamba la Kafoi na kitongoji cha Esimbosi, kwa kuwa mwekezaji amevuka mipaka ya shamba lake na kuingia kwenye eneo la kitongoji na kusababisha wakazi wa kitongoji hicho kujenga na kuishi katika makazi yasiyopimwa.

Alisema kitongoji chao pia hakina eneo kwa ajili ya kujenga ofisi za kitongoji, uwanja wa michezo kwa ajili ya watoto na vijana eneo la kujenga soko la mifugo na chakula, maeneo ya wazi kwa ajili ya kupanda miti, mapumziko na mikutano ya hadhara.

"Hatuna eneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vidogo vya kuchakata maziwa kwa kuwa wakazi hao ni wakulima na wafugaji na kuiomba serikali kuingilia kati na kutatua mgogoro huo uliodumu kwa zaidi ya miaka 15 sasa," alisema.

Ili kumaliza mgogoro huo serikali haina budi kumwonyesha mipaka na kuweka alama za shamba la mwekezaji wa shamba la Kafoi Estate limited na wananchi wakiwamo vijana waweze kupata ardhi itakayopimwa kwa ajili ya makazi, biashara, kilimo, ufugaji, uwekezaji wa viwanda ili waweze kupata maendeleo.

"Mheshimiwa Katibu tunakuomba uingilie kati na kutatua mgogoro huu uliodumu kwa zaidi ya miaka tano sasa na tuna imani na serikali yetu ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli kuwa mgogoro huu utashughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi wake," alisema Danieli.

# Kodi yakwamisha chakula kutolewa bandarini

**Na Mary Mosha,** HAI

SHIRIKA la New Life Tanzania, limeiangukia serikali kuomba 'ahueni' ya kodi kwa ajili ya kukomboa chakula cha msaada kilichokwama Bandari ya Dar es Salaam kwa zaidi ya miezi sita sasa.

Chakula hicho, kiliingizwa nchini kwa ajili ya kusaidia makundi mbalimbali ya jamii, zikiwamo koo za wawindaji wa Kihadzabe na wafugaji wa kabila la Wasonji.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Askofu mstaafu wa Kanisa la TAG, Glorius Shoo, alieleza hayo jana, wakati wa kongamano la 11 la watoto ambalo limeshirikisha wadau kutoka nchi mbalimbali duniani.

"Kwa kweli nia yetu ni njema kwa sababu tunasaidia wahitaji hasa jamii inayoishi pembezoni. Sasa tunamwomba Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango na Rais Dk. John Magufuli, watazame namna ya kutusaidia kuingiza chakula cha msaada kwa ajili ya watoto wanaotoka katika jamii zilizo pembezoni.

"Kila mwaka tumekuwa tukipewa msamaha wa kodi tukiingiza vyakula vya msaada, lakini kwa mwaka huu tumetakiwa kulipa kodi ya takribani shilingi milioni nne ambayo tumeshaipata, isipokuwa hatuna pesa ya hifadhi ambayo kwa sasa tunadaiwa zaidi ya miezi sita," alisema.

Alisema taasisi hiyo iliamua kuwasaidia watoto wanaoachwa pembezoni hasa kutoka jamii za wawindaji wa kabila la Wahadzabe, Wasonji pamoja na watoto yatima ambao wanatoka katika mazingira magumu.

Awali, akisoma taarifa ya mwaka ya shirika hilo, Mwenyekiti wa bodi hiyo Mchungaji Isarael Ndalishao, alisema mbali ya changamoto wanazokabiliana nazo, lengo la kongamano hilo ni kuongea na watoto kujitambua na kuachana na maisha waliyopitia.

"Tupo hapa kwa ajili ya kujenga uelewa wa pamoja kwa jamii kuwajali na kuwapenda watu wenye mazingira magumu na kuwajenga watoto kuwa wakombozi wa taifa letu kwa kujenga watoto kwenye misingi bora na maadili," alisema Ndalishao.

Akifungua kongamano hilo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mgwhira, alisema ameshapokea ombi hilo kwa niaba ya serikali na atafuatilia madai hayo ili kujua taratibu ambazo hazikufuatwa na hivyo kukwamishwa chakula hicho cha msaada kuwafikia walengwa.

Nipashe
Spotika




BARCELONA YA GRIEZMANN, MESSI ITAKAVYOKUWA UK.18



## ISIKUPITE

MANCHESTER United itasitisha mchakato wa kumuuza kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba (26) baada ya dirisha la usajili la Ligi Kuu England litakapofungwa ifikapo Alhamisi Agosti 8 mwaka huu. Klabu hiyo imetaja thamani ya Pogba ambaye anawindwa na klabu za Juventus na Real Madrid kuwa ni pauni milioni 150.



MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Senegal, Idriss Gueye, ambaye amefunga mabao muhimu kwa nchi yake katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019) zinazoendelea Misri. Jana usiku Senegal ilikuwa ikiivaa Tunisia katika mchezo wa hatua ya nusu fainali ya kwanza ya michuano hiyo. Baadaye Algeria ilitarajiwa kucheza dhidi ya Nigeria. **PICHA: MTANDAO**

SOKA




# NJIA NNE ZA KUIREJESHA UTD KUWA TISHIO

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United kwa misimu ya hivi karibuni umwamba wake kwenye soka la England unaonekana kupungua kama sio kuporomoka kwa kasi ya ajabu.

**Mashetani wekundu hao walitawala soka la England kwa miongo miwili mfululizo, yaani miaka 20. Hata hivyo, tangu mwaka 2013, wamekuwa kwenye wakati mgumu na mbaya zaidi katika historia yao.**

Ingawa United wametumia kiasi cha pauni milioni 751.7 wamejikuta wakibadilisha makocha mara tano kwa kipindi cha miaka sita. Pamoja na hilo lakini klabu imeendelea kuwa na matatizo makubwa.

Hivyo basi, makala hii inakuchambulia namna gani United inaweza kurudi kwenye umwamba wake. Inaweza kuchukua muda, na hatua hii ikawa ngumu na ikachukua hadi miaka mitano, lakini hapa tunaangalia namna gani inawezekana, kwani hakuna kisichowezekana.

Haya twende:

**1) MMILIKI MPYA**

Familia ya Glazers ambao ndio wamiliki wa Manchester United wamekuwa wakiendelea na maisha yao, huku klabu ikionekana kuyumba.

Tangu mwaka 2005, Wamarekani hao wametumia kiasi cha pauni bilioni moja kwenye kuwekeza. Ukiangalia upande mwingine Sheikh Mansour ametumia kiasi cha pauni bilioni 1.3 pale Manchester City kwa uwekezaji tangu mwaka 2008 na ukiangalia hapo unaona kuna tofauti kubwa mno kati yao.

Msimu uliopita peke yake, City ilimaliza mbele kwa pointi 32 zaidi ya wapinzani wao hao wa jiji moja. Walifunga zaidi ya mabao 30 na kuruhusu nyavu zao kutikiswa mara 31 tu, na walishinda mataji yote ya nyumbani. Na kwa nyongeza, City waliwafunga kwa msimu wa tatu mfululizo. Takwimu haziongopi. Ukiangalia unaonekana kabisa klabu hizi zinautofauti mkubwa mno kwa wamiliki wake.

Bila ya United kutafuta bilionea mpya ambaye atawekeza fedha kwa faida ya klabu na kuweka mapenzi yake moyoni, basi pengo kati ya klabu hao majirani litabakia kuwa kubwa mno.

**2) OFISA MTENDAJI MPYA**

Licha ya kuwa mzuri zaidi katika biashara, Ed Woodward amekuwa katili kwa masuala ya soka na hakubali kubadilika. Ubishi wake kwenye suala la usajili na maamuzi yake yasiyokuwa na mpango wa kusajili wachezaji wapya wenye vipaji kwa fedha nyingi, kuna wafanya mashetani wekundu hao kuwa kwenye wakati mgumu zaidi kumsajili mchezaji wanayemtaka kwa wakati sahihi.

Woodward amekuwa katikati ya kushindwa kwa United kwenye suala la usajili, anatakiwa kuondolewa kwenye nafasi yake kama Makamu Mwenyekiti Mtendaji na kumpelekea kwenye masuala ya kibiashara tu. United inatakiwa kwenda Uholanzi kumchukua Edwin van der Sar ili awe Ofisa Mtendaji wao Mkuu. Amekuwa akifanya kazi nzuri mno pale katika Klabu ya Ajax.

Zaidi ni kwamba, anaijua vema United kama kiganja cha mkono wake baada ya kuichezea klabu hiyo kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2011 na kuwa mmoja wa magwiji wa wakati wote wa klabu hiyo. Hivyo akiwa amecheza wakati United ikiwa kwenye kilele cha mafanikio anajua mengi ya kuifanya klabu hiyo kurudi katika nafasi yake. Kile alichokifanya kule Ajax anaweza pia kukifanya akiwa pale United.

**3) MKURUGENZI WA SOKA**

Hii ni injini muhimu mno kwa klabu yoyote, huwa ndio kiungo cha ufundi kwa klabu hiyo. Kwa sasa moja ya sehemu ambayo klabu nyingi Ulaya wanaiangalia kwa makini zaidi ni hii. Angalia klabu zifuatavyo na wakurugenzi wake zilivyopata mafanikio: City (Txiki Begiristain), Liverpool (Michael Edwards), Atlético Madrid (Andrea Berta), Borussia Dortmund (Michael Zorc), Bayern Munich (Hasan Salihamidži ), Juventus (Fabio Paratici) na Ajax (Marc Overmars).

Ukiangalia unaona tofauti kubwa mno ya wakurugenzi wa klabu hizo na United. Kama mashetani hao wekundu wanataka kurudisha ushindani wao kwenye soka la Ulaya wanatakiwa kuleta mkurugenzi wa soka mpya ambaye anakuwa na maono ya kuipeleka mbali klabu hiyo.

Sio tu kuwachukua wachezaji wenye uzoefu kama Rio Ferdinand na Darren Fletcher, lakini wanaweza kumchukua mtu mwenye ufahamu mzuri zaidi wa soka la kibiashara la sasa na mwenye mtazamo wa ushindani.

**4)KUFUMUA KIKOSI**

Kuendelea kubakia na kikosi cha sasa cha United hakitakuwa na mabadiliko yoyote makubwa.

Kuna wachezaji wengi mno katika kikosi hicho ambao wanaonekana wazi kwamba hawawezi 'kufiti' kucheza kwenye kikosi hiki. Licha ya kutumia kiasi kikubwa cha fedha kwa siku za hivi karibuni, lakini ubora wa kikosi haupo kwenye kiwango cha kuridhisha.


Wachezaji kama Alexis Sánchez, Ashley Young, Phil Jones, Chris Smalling, Marcos Rojo, Matteo Darmian na Romelu Lukaku wote wangepaswa kuuzwa. Wachezaji hawa wameonyesha kwamba bado nafasi yao ya kuichezea klabu kama hiyo kuwa kubwa mno na wanaweza kurithishwa na wachezaji vijana na wenye vipaji, ambao wana njaa ya mafanikio.

Hadi sasa, United imesamjili Daniel James na Aaron Wan-Bissaka. Usajili mzuri? Ndio, haswa kwa kiwango chao cha fedha ambapo jumla yao ni pauni milioni 65. Hata hivyo, kwa ajili ya kuimarisha zaidi kikosi hicho, United sasa inatakiwa kuleta beki mpya wa kati, beki wa kushoto, viungo wawili na mshambuliaji mmoja.

Kwani hali ya sasa ya klabu inazungumza mengi, uboreshwa wake ni muhimu zaidi kwa kikosi hicho. Na ili kuweza kuweza kuleta ubora wake haina namna dhidi ya kukifumua kikosi chote.

Bila kufanya hivyo, United haitakuwa na maajabu makubwa kwako kwa sababu hakutakuwa na mabadiliko yoyote na wasipofanya hivyo, watajikuta hata nafasi ya sita waliyomaliza msimu uliopita wanaweza kuikosa.

**JE, WAJUA?**



MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Wales na Real Madrid, Gareth Bale, ambaye ana umri wa miaka 29, amekuwa akijituma kwenye kambi ya mazoezi ya klabu hiyo iliyoko Canada ili kumshawishi Kocha Zinedine Zidane, amjumuishe kwenye mipango ya vigogo hao wa Hispania.

# MICHEZO

## NJE YA UWANJA

# Neymar afunguka siku bora kwake

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Neymar, amesema kuwa wakati mzuri ambao hatausahau katika maisha yake ya soka ni pale alipokuwa na Barcelona na kupata ushindi wa mabao 6-1 dhidi ya timu yake ya sasa.

Tayari Mbrazil huyo ameshasema kuwa anataka kuondoka PSG katika kipindi cha dirisha la usajili la majira ya joto. Barca inatajwa ndio klabu ambayo Neymar anataka kurejea.





# USIYOYAJUA AZAM, KMC ZIKIKIPIGA KAGAME CUP

Na Adam Fungamwango

MASHINDANO ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame yanaendelea kutimua vumbi kwenye viwanja mbalimbali nchini Rwanda, huku Tanzania ikiwakilishwa na timu tatu za Azam FC, KMC FC kwa upande wa Bara na KMKM upande wa Visiwani.

**Hata hivyo, tayari timu za KMC na KMKM zimeshafungashiwa virago baada ya kutofanya vema kwenye michuano hiyo na kuiacha timu ya Azam ikiendelea kwenye hatua ya robo fainali.**

Azam imefanikiwa kusonga mbele kwa kukamata nafasi ya pili kwenye Kundi B, ikimaliza na pointi nne nyuma ya KCCA ya Uganda iliyomaliza mechi zake ikiwa na pointi saba.

Azam ilianza kwa kushinda bao 1-0 dhidi ya wenyeji Mukura Victory, ikachapwa bao 1-0 dhidi ya Waganda KCCA na kutoka sare ya bila kufungana dhidi ya Bandari ya Kenya.

KMC iliyokuwa kwenye Kundi A, pamoja na kuichapa Rayon Sport bao 1-0 Jumamosi, lakini imetoka kutokana na kufikisha pointi nne tu, huku TP Mazembe na Rayon zikisonga mbele zote zikiwa na pointi sita.

Wakati michuano hiyo ikiendelea kuna mambo mbalimbali yaliyojitokeza na mengine ni ya kihistoria ya michuano, pamoja na rekodi mbalimbali zilizowahi kuwekwa huko nyuma.

**1. MAAJABU MATATU MECHI YA TP MAZEMBE, KMC**

TIMU ya KMC Jumanne iliyopita iliingia kwenye rekodi ya kucheza Kombe la Kagame kwa mara ya kwanza kwenye historia ya klabu hiyo tangu ilipoanzishwa, huku kukiwa na mambo matatu makubwa yalijoyojitokeza kwenye mechi yao dhidi ya TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Katika mechi hiyo iliyofanyika Rwanda inakofanyika michuano hiyo, KMC iliangukia pua kwa kuchapwa bao 1-0, lililofungwa na Mondeko Zatu dakika ya 61.Mechi hiyo ilishuhudia kipa Juma Kaseja, kipa wa zamani wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba akikutana tena na TP Mazembe baada ya miaka minane.

Kipa huyo ndiye aliyekuwa kipa wa Simba na kusisimama golini mwaka 2011, wakati timu hiyo ikicheza na TP Mazembe kwenye mechi zote mbili za Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa Tanzania na nyingine mjini Lubumbashi.

Katika mechi hizo Simba ilifungwa zote, bao 3-1 ugenini na mabao 3-2 Tanzania. Kwa maana hiyo Kaseja amefungwa mechi zote tatu alizosimama langoni dhidi ya TP Mazembe.

Mohamed ambaye ni kaka wa Mbwana, alikuwa ni mmoja wa wachezaji wa KMC waliokuwa wakikipiga dhidi ya TP Mazembe.

Mdogo wake alikuwa mchezaji wa kutegemewa wa timu hiyo na alisajiliwa mwaka 2011, mara baada ya mechi ya Simba dhidi ya TP Mazembe. Kwa sasa Mbwana anaichezea Genk na Ubelgiji, huku Mohamed akiwa mchezaji mpya wa KMC baada ya kusajiliwa kutoka Mbeya City.

Kingine ni kwamba, Janvier Bokungu, beki Mkongomani aliyesajiliwa hivi karibuni akitokea nchini huko, alikuwa akicheza dhidi ya timu yake ya zamani TP Mazembe.

Bokungu alikuwa akiichezea KMC kwa mara ya kwanza baada ya kusajiliwa kutoka Groupe Bazano ya DRC.

Ikumbukwe kuwa Bokungu alishawahi kuichezа Simba msimu wa mwaka 2016/17 na kabla ya hapo alikuwa akiicheza TP Mazembe.

**2. REKODI YA SIMBA HAITOFIKIWA**

Kwenye michuano hiyo hakuna timu yoyote itayofikia rekodi ya klabu ya Simba iliyotwaa ubingwa huo mara sita.

Simba ndiyo timu inayoongoza kwa kutwaa ubingwa mara nyingi zaidi kwenye michuano hiyo ilifanya hivyo mwaka 1974, 1991, 1992, 1995, 1996 na 2002. Ni kwa sababu hakuna timu yoyote ile kati ya zinazoshiriki zilizotwaa ubingwa huo angalau mara tano.

Timu ambazo zingeweza kuifikia Simba kama zingeshiriki na kutwaa ubingwa ni Yanga, Tusker FC, na AFC Leopards ambazo kila moja zimetwaa mara tano.

**3. KENYA YAFUNIKA, TANZANIA YAFUATIA**

Kwa jumla ni kwamba Kenya kuchukua mara nyingi, baada ya timu zake kutwaa kombe la Kagame mara 15, huku Tanzania ikifuatia kwa kuchukua mara 13.

AFC Leopards na Tusker zimetwaa kila moja mara tano, Gor Mahia ikitwaa mara tatu na Luo Union ikichukua mara mbili.

Tanzania imechukua mara hizo kwa timu zake ya Simba kuchukua mara sita, Yanga mara tano, huku Azam ikitwaa kombe hilo mara mbili. Uganda na Rwanda, nchi hizo timu zake zimebeba kwa mara tano kila moja.

Extra Time



# MECHI 11 ZA 'KUFA MTU' LIGI KUU BARA

Na Adam Fungamwango

AGOSTI 23 ndiyo siku ya kuanza kwa pazia la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20 kwa mujibu wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF) kupitia Bodi ya Ligi.

**Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Bodi ya Ligi, ni kwamba Mabingwa wa Tanzania Bara, Simba watakuwa wageni wa JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.**

Ligi itaendelea tena Agosti 24 wakati Mbao FC itakapokuwa nyumbani dhidi ya Alliance, Mbeya City ikiikaribisha Prisons, Namungo kwa mara ya kwanza itacheza ligi ikiwa nyumbani dhidi ya Ndanda.

Polisi Tanzania, timu nyingine iliyopanda Ligi Kuu itakuwa nyumbani ikicheza dhidi ya Coastal Union, Biashara nayo itaikaribisha Kagera Sugar, Mwadui dhidi ya Singida United na Lipuli itaialika Mtibwa Sugar.

Agosti 28, Yanga itakuwa nyumbani Uwanja wa Taifa dhidi ya Ruvu Shooting na KMC itakuwa mwenyeji wa Azam Agosti 29.

Baada ya hapo mechi za Ligi Kuu zitakuwa zikiendelea kama kawaida. Hata hivyo, macho na masikio ya mashabiki wengi wa soka yataelekezwa kwenye baadhi ya mechi ambazo kwao hawatotaka ziwapite hivi hivi.

Hii ni kwa sababu ya kihistoria, rekodi za kuvutia, au za kushangaza zilipocheza huko nyuma au msimu uliopita na mengine yanayofanana na hayo.

Mwandishi wa makala haya ameorodhesha mechi 11 ambazo wengi wanazisubiri kwa hamu na hawataki kuzikosa ama kwenda uwanjani, kuangalia kwenye TV nyumbani au 'vibanda umiza' ama kusikiliza redio.

### 1. SIMBA VS MTIBWA SUGAR (SEPTEMBA 17, 2019)

Mechi hii itachezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini. Mara nyingi Simba hupata tabu inapocheza dhidi ya Mtibwa iwe Dar es Salaam au Morogoro. Inakuwa mechi ngumu na isiyotabirika.

Ingawa rekodi zinaibeba Simba hasa ikicheza Dar es Salaam, kuliko zile zinazochezwa Uwanja wa Jamhuri, lakini ikumbukwe kwa msimu wa 2017/18, ililazimika 'kuchomoa' goli 'usiku', dakika za nyongeza kwa faulo ya Emmanuel Okwi ambaye kwa sasa hayupo, ikaponea kwenye tundu la sindano kwa sare ya bao 1-1.

### 2. YANGA VS NDANDA FC (NOVEMBA 8, 2019)

Mechi kati ya Yanga dhidi ya Ndanda haijawahi kuwa nyepesi hata siku moja.

Kwa misimu yote ambayo Ndanda iko kwenye Ligi Kuu, Yanga imeifunga timu hiyo mara mbili tu. Msimu uliopita timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1 kwenye mechi zote za nyumbani na ugenini.

Ndiyo maana pamoja na Yanga kucheza nyumbani bado hakuwezi kuifanya mechi hiyo kuwa rahisi kutokana na rekodi za timu hizo mbili kila zinapokutana.

### 3. KAGERA SUGAR VS SIMBA (OKTOBA 3, 2019)

Itakuwa shughuli pevu kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, wakati Kagera Sugar itakapowakaribisha vibonde wake wa msimu uliopita, Simba.

Pamoja na kutwaa ubingwa, lakini Simba ilifungwa 'nje ndani' na Kagera Sugar.

Ilichapwa mabao 2-1 Bukoba, ikafungwa tena bao 1-0 waliporudiana kwenye Uwanja wa Taifa. Pia mechi kati ya timu hizo mbili haijawahi kuwa rahisi kwa Simba hata siku moja, hivyo mashabiki wanataka kuona siku hiyo, mambo yatakuwaje.

### 4. MBAO FC VS YANGA (OKTOBA 24, 2019)

Patashika nguo kuchanika itakuwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza wakati Mbao FC itakapoikaribisha Yanga.

Kila mtu anajua Yanga inapokutana na Mbao Kirumba shughuli inavyofanyika. Ni msimu uliopita tu ndipo Yanga ilipofanikiwa kuifunga Mbao kwenye uwanja huo.

Msimu huu mashabiki wengi wanataka kuona kama Yanga ilibahatisha msimu uliopita na kurudia uteja wake wa huko nyuma au la.

### 5. SIMBA VS AZAM FC (OKTOBA 23, 2019)

Ni moja kati ya mechi kubwa kwenye soka la Tanzania kwa sasa. Inapocheza Azam dhidi ya Simba au Yanga kwenye soka la Bongo inahesabiwa kuwa ni bonge la mechi kutokana na kuwa timu hiyo kwa sasa ina mzani sawa na timu hizo kongwe uwanjani, ikizizidi timu hizo kwenye miundombinu, lakini ikizidiwa tu na idadi ya mashabiki. Msimu uliopita Azam ilidondosha pointi nne kwa Simba, ikifungwa mabao 3-1 mzunguko wa kwanza na sare ya bila kufungana mzunguko wa pili.

### 6. SIMBA VS LIPULI (SEPTEMBA 22, 2019)

Simba itaikaribisha Lipuli kwenye Uwanja wa Taifa siku hiyo kwenye moja ya mechi inayotarajiwa kuwa bora. Mashabiki watataka kuona kama Lipuli iliyokuwa ikiikomalia Simba chini ya Selemani Matola ambaye kwa sasa yupo Polisi Tanzania itakuwa ni ile ile au itakuwa tofauti.

Lipuli, moja ya timu ambayo imeshaanza kuwa tishio kwenye Ligi Kuu, itataka kuonyesha kuwa pamoja na kuondokewa na kocha huyo, na baadhi ya wachezaji bado iko vizuri.

### 7. SIMBA VS KMC (OKTOBA 19, 2019)

Itachezwa Oktoba 19 kwenye Uwanja wa Taifa jijini. Mechi hii itakuwa inafuatiliwa na mashabiki wengi kwa sababu mechi ya moja ya msimu uliopita ilileta maneno mengi, kiasi cha mwamuzi wa mechi hiyo, Ibrahim Kambuzi alifungiwa.

Simba ilishinda mabao 2-1 na kupata penalti mbili, huku moja ikilalamikiwa kuwa haikuwa halali.

Hata hivyo msimu huu, KMC itakuwa ikiwa chini ya kocha mpya Mganda Joseph Mayanja baada ya Mrundi Etienne Ndayoragije kujiunga na Azam FC.

### 8. YANGA VS LIPULI (FEBRUARI 5, 2020)

Ni mechi ya mzunguko wa kwanza, lakini itacheza Februari mwakani. Ni mechi kali ambayo kila shabiki wa soka nchini hatotaka impite kwa sababu kama nilivyosema awali kuwa Lipuli kwa sasa ni moja kati ya timu tishio nchini.

Msimu uliopita ilikuwa ni moja kati ya timu chache iliyofifisha matumaini ya Yanga kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ilipoichapa bao 1-0 na kuidhohofisha kwenye mbio za kuikimbia Simba.

Lakini pia ndiyo iliyoifunga Yanga kwenye hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA, hivyo mashabiki watataka kuona kama nguvu hiyo na msimu huu ipo au?

### 9. MBAO FC VS SIMBA (JANUARI 15, 2020)

Mashabiki wengi wanakumbuka kuwa kipigo cha kwanza kwa Simba msimu uliopita kwenye Ligi Kuu kilikuwa ni dhidi ya Mbao FC kwenye Uwanja wa CCM Kirumba.

Ilifungwa bao 1-0 na kuzua tafrani kubwa kwa mashabiki kuwarushia mawe na chupa za maji wachezaji, benchi la ufundi pamoja na msemaji wa klabu hiyo, Haji Manara.

Baada ya kupoteza mechi hiyo, Simba ndipo ilipoanza kukaa vizuri na kuanza kushinda mechi nyingi. Safari hii inaweza kujirudia?

### 10. AZAM FC VS YANGA (JANUARI 22, 2020)

Ni mechi ya mzunguko wa kwanza ambayo Azam itakuwa mwenyeji. Kama nilivyosema kuwa mechi kati ya Azam dhidi ya timu hizi kubwa Simba na Yanga huhesabiwa kama ni kubwa na huwa na mvuto wake kuanzia mitaani hadi uwanjani kwenyewe.

Na hii ni kwa sababu nilizozieleza awali, lakini kwa nyongeza tu ni kwamba timu hizi tatu Simba, Yanga na Azam ndizo zinazoonekana kwa maneno na vitendo kuhitaji Ubingwa na Tanzania Bara, tofauti na timu nyingine.

### 11. SIMBA VS YANGA (JANUARI 4, 2020)

Mechi hii ya watani wa jadi, itachezwa siku tatu tu baada ya mwaka mpya. Ni mechi ambayo haihitaji maelezo mengi kwa shabiki yoyote wa soka nchini.

Hata hivyo, mashabiki wengi wanataka kuangalia kama Yanga inaweza kuuweza mtihani wa kuifunga Simba kwani tangu mwaka 2016 haijaweza kufanya hivyo.

Mara ya mwisho Yanga kuifunga Simba ilikuwa ni Februari 20, 2016 kwenye mechi ya Ligi Kuu kwa mabao 2-0, yaliyofungwa na Donald Ngoma na Amissi Tambwe. Kumbuka msimu huo wa 2015/16 Yanga iliifunga Simba mechi zote mbili kwa idadi hiyo hiyo ya magoli.

Kuanzia hapo Yanga imekuwa ikipata vipigo au kuambulia sare kwa misimu yote iliyofuata.

## Nukuu

"Sitaki kuwa mmoja wa wahusika katika rushwa ya aina hii, hatukutakiwa kuwa katika uonevu huu ambao tumekutana nao katika Copa America ya mwaka huu. Tulipaswa tufike mbali katika mashindano lakini tulizuiwa tusifike fainali, rushwa, waamuzi na vingine vingi vimewanyima watu uhondo wa kushuhudia kandanda safi."
"Mimi mara zote nasema ukweli na ni muwazi, ndicho kinachonifanya kuwa mtulivu hivi," **alisema Lionel Messi kufuatia timu yake ya Taifa ya Argentina kushindwa kufika fainali ya michuano hiyo.**




"Nimefurahi kuona nidhamu imeanza, asilimia 95 ya wachezaji wamejitahidi kuripoti kambini, nidhamu waliyoionyesha imenifurahisha, wameonyesha kutii amri ya uongozi wao," **Mwenyekiti wa Yanga, Mshindo Msolla alisema siku moja kabla ya timu yake haijaingia kambini kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.**



"Nina furaha kubwa kuendelea kuwa hapa na kusaini mkataba mpya wa miaka mitano. Ni sehemu ambayo nimekuwa nikicheza hapa, na sasa nina uhakika nitacheza hapa kwa muda mrefu zaidi," **alinukuliwa Ruben Loftus-Cheek na tovuti ya Klabu ya Chelsea.**



# BARCELONA YA GRIEZMANN, MESSI ITAKAVYOKUWA




**BARCELONA,** Hispania

KIPINDI hiki cha dirisha la usajili la majira ya joto kimekuwa cha kuvutia mno kwa soka la Ulaya, huku klabu zikifanya usajili wa wachezaji wapya kuimarisha timu zao.

**Barcelona inaonekana kuwajibu wapinzani wao wakubwa wa soka la Hispania, Real Madrid ambao wametumia kiasi cha euro milioni 300 kwa ajili ya usajili wa wachezaji wapya na wakiwa na nia kurudi vizuri zaidi kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Hispania, La Liga.**

Barça tayari wamemsajili kiungo mwenye umri wa miaka 22, Frenkie de Jong kutoka Ajax kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 86, golikipa Neto katika usaili uliomhusisha pia Jasper Cillissen kusepa, na sasa hatimaye wamemsajili Antoine Griezmann kwa euro milioni 120.

La Blaugrana hao baada ya katolewa hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita na pia wakilikosa Kombe la Copa del Rey baada ya kufungwa kwenye fainali, kocha, Ernesto Valverde amekuwa na presha kubwa kuhusu kikosi chake msimu unaokuja.

Wakati Griezmann ameshatua na pia kukiwa na uwezekano mkubwa wa kumsajili nyota wa Inter, Lautaro Martinez na Neymar, safu ya ushambuliaji ya Barça inaweza kuwa ndio bora zaidi kwa msimu ujao kwenye Ligi Kuu Hispania na hata Ulaya.

Makala hii hapa inaangalia faida na hasara namna ya fowadi hiyo itakavyokuwa msimu ujao.

4-2-3-1 (Griezmann - Messi - Dembélé - Suarez)

**FAIDA**

Ni wazi inaweza kuwa changamoto kubwa kwa Barça kumtumia Griezmann kwenye timu, lakini kwa mfumo huu itakuwa njia nzuri kwa kocha Valverde kufanya mambo yaende sawa bila kuharibu chochote.

Kucheza kwa mfumo wa 4-2-3-1 kunaweza kuwezesha Lionel Messi kuutawala mchezo na kutengeneza mashambulizi mengi akiwa akicheza kama namba 10, huku Dembélé na Griezmann wakiwa na nafasi kubwa ya kutiririka pembeni. Mshindi huyo wa Kombe la Dunia ataweza kuwa na nafasi kubwa ya kuwatumia mabeki wa pembeni Jordi Alba na Nelson Semedo (pengine) kupata nafasi nzuri ya kupanda na kushuka.

Sasa unaweza kujionea namna gani safu ya ushambuliaji yenye wachezaji kama inavyoweza kutisha dimbani.

**HASARA**

Griezmann alikuwa akicheza kama mshambuliaji wa kati kule Atletico, mara kwa mara akicheza kama mshambuliaji pekee. Kama atafanya hivyo pale Camp Nou, kwa uhakika mkubwa hatakuwa na nafasi kwenye kikosi.

4-4-2 (Messi - Griezmann)

**FAIDA**

Valverde mara nyingi amekuwa akitumia mfumo wa 4-4-2, na kuna uwezekano akaendelea kuutumia kwa msimu ujao.

Huku Luis Suarez kwa sasa akiwa na umri wa miaka 32, kufunga mabao umekuwa mzigo mzito mabegani mwake na sasa nafasi hiyo ataweza kuachia Griezmann acheza na Messi.

Raia huyo wa Uruguay alifunga mara moja tu katika kipindi cha mwisho cha msimu, ingawa aliweza kufikisha mabao 21 kwenye La Liga. Kama ukitumika mfumo huo, maana yake ni kwamba, maisha ya Philippe Coutinho pale Barcelona yatafikia mwisho.

**HASARA**

Griezmann amekuwa akicheza kama mshambuliaji pekee wa kati, hivyo kwa staili yake itakuwa ngumu pale Barca.

Alifunga mabao 15 kwenye La Liga msimu uliopita, lakini kucheza kwa pamoja na Messi itakuwa ngumu kwake kuweza kubakia kama mshambuliaji pekee.

4-3-3 (Messi - Griezmann - Coutinho)

**FAIDA**

Kama Coutinho ataendelea kubakia pale Barcelona mfumo huu unaweza kuwa na maana kubwa zaidi kwa kikosi hicho kuweza kuwaweka mbele washambuliaji watatu. Messi na Griezmann wanaweza kuwa upande wa kushoto na kulia, na kumwacha katikati Coutinho.

Mshambuliaji wa kati atacheza kwa uhuru kwa kupokea mipira kutoka kushoto na kulia, huku wakitengeneza mfumo ambao utaifanya safu ya ulinzi ya timu pinzani kuwa kwenye wakati mgumu zaidi.

Katika nafasi ya kiungo watakuwa Arthur, Busquets na De Jong, na hivyo kuwa na faida kubwa mno ya kusukumiza mashambulizi mbele na kuwapa Barça uimara zaidi kwenye kiungo na ushambuliaji.

**HASARA**

Mfumo huu kwa namna nyingine hautakuwa na ubunifu, ingawa mabao yanaweza kuwa mengi tu. Kuwachukua Messi na Griezmann na kuwaweka kwenye winga, maana yake kutakuwa na kitu kinachokosekana pale katikati.

**NAJUA WAJUA**



BEKI wa zamani wa Azam FC, Gadiel Michael, tayari ametangazwa kujiunga na mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara akitokea Yanga.

# FELIX ATAJWA KUVAA VIATU VYA RONALDO




**MADRID,** Hispania

KINDA Joao Felix ameingiza kwenye orodha ya kuwa mmoja wa wachezaji ghali zaidi mwenye umri mdogo duniani baada ya kujiunga na Atletico Madrid kutoka Benfica kwa dau la pauni milioni 113.

**'Dogo' huyu mwenye umri wa miaka 19 alianza kuichezea Benfica mwanzoni mwa msimu wa 2018-19, lakini alifunga ma goli 15 na kutoa pasi tisa zilizozaa magoli katika ligi hiyo, huku klabu yake ikishinda taji la ligi.**

Alifunga 'hat-trik' dhidi ya klabu ya Ujerumani ya Eintracht Frankfurt katika Ligi ya Europa Aprili mwaka huu.

Na hilo likamfanya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi katika klabu ya Benfica na Ureno kufunga magoli matatu kwenye mchezo mmoja katika mashindano ya Ulaya.

Kipaji chake kilimfanya kuitwa katika Timu ya Taifa ya Ureno na akaanza kuhusishwa na uhamisho wa klabu kama vile Manchester United na Manchester City kabla ya Atletico Madrid kumnunua kwa donge nono na kumfanya kuwa mchezaji ghali zaidi baada ya mshambuliaji wa PSG, Kylian Mbappe.

Felix alianza kusakata soka katika timu ya vijana ya klabu ya Porto, lakini aliondoka mwaka 2015, kwa madai ya kuwa ni mwembamba na akajiunga na wapinzani wao.

Akiwa Benfica na umri wa miaka 16 alifanikiwa kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi miongoni mwa wachezaji wa ziada kuwahi kuichezea klabu hiyo wakati alipoanzishwa Septemba 2016.

Lakini katika msimu wa 2018/19 alianza kucheza rasmi na mnamo Novemba mwaka jana alipewa mkataba uliokuwa na kipengele cha kumuuza kwa euro milioni 120 ambao Atletico waliweza kulipa.

Mechi yake ya kwanza ilikuwa dhidi ya Boavista Agosti na katika mechi ya pili alifunga goli lake la kwanza dhidi ya wapinzani wao Sporting Lisbon kwa kichwa.

Chini ya kocha, Rui Vitoria hakupata nafasi nyingi za kucheza, lakini alichezeshwa mara kwa mara chini ya kocha, Bruno Lage ambaye alichukua nafasi klabuni hapo Januari na alifunga mara mbili katika mechi ya kwanza ya ligi na kumaliza msimu akiwa na magoli 20 kutoka mechi 43 katika mashindano yote.

Miongoni mwa vijana katika Ligi Kuu barani Ulaya - Uingereza, Itali, Hispania, Ujerumani, Ufaransa, Ureno na Uholanzi, Felix alikuwa wa pili katika ufungaji wa magoli nyuma ya kiungo wa kati wa Bayer Leverkusen na raia wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 19, Kai Havertz.

Na yuko nyuma ya winga wa Timu ya Taifa ya England na Borussia Dortmund, Jadon Sancho kwa upande wa magoli aliyochangia.

Mabadiliko ya kuwa mchezaji wa kulipwa sio rahisi, lakini kwake ilikuwa rahisi. Wakati unapokutana naye nje ya uwanja, kuzungumza naye, mtazame akizungumza katika vyombo vya habari utagundua mvulana mwenye furaha.

Shinikizo ya kutaka kushinda ni kitu anachokabiliana nacho vizuri kila siku. Jose Delgado, Naibu Mkurugenzi katika gazeti la A Bola la Ureno anammiminia sifa chungu nzima kijana huyu.

"Tangu Ronaldo hatujawahi kuwa na mchezaji anayechangamshana kijana kama huyu," alisema Delgado wakati wa mahojiano yake na BBC Sport.

Felix atalinganishwa na mchezaji bora Ureno kwa sasa, mshindi mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or Ronaldo. "Tayari wamemuita mrithi wangu wa Ronaldo."

Ni mchezaji mwenye mchanganyiko wa kucheza namba 9 na 10, anacheza kama mshambuliaji wa pili. Ni mchezaji mwenye vichwa vizuri hata iwapo sio mchezaji mwenye maungo makubwa.

Ni mchezaji anayejua kutafuta nafasi katika safu ya ulinzi ya upinzani, na ndio sababu yeye hufunga zaidi na hupiga mpira kwa kutumia miguu yote miwili.

Ni mchezaji mzuri mwenye ufundi. Kile kinachomfanya kuwa tofauti ni mshambuliaji anapowasili katika lango la upinzani na anafunga magoli.Lakini pia ni mchezaji mzuri katika wingi katika kusaidia na kutoa pasi.

NDANI YA 18




KOCHA mpya wa Chelsea, Frank Lampard, ameanza kwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Bohemian katika mechi ya kirafiki iliyochezwa Jumatano iliyopita. Lampard ametua katika timu yake hiyo ya zamani kuchukua mikoba ya Maurizio Sarri.



MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Neymar, amesema kuwa wakati mzuri ambao hatausahau katika maisha yake ya soka ni pale alipokuwa na Barcelona na kupata ushindi wa mabao 6-1 dhidi ya timu yake ya sasa.

Uk. 15



# UMUHIMU WA KOSCIELNY UNAVYOITESA ARSENAL

**LONDON,** England

KUNA maneno machache unayoweza kuielezea safu ya ulinzi ya Arsenal kwa kipindi cha muongo mmoja uliopita.

Hata hivyo kwa misimu ya hivi karibuni, katikati ya mafanikio yao yanaangukia kwa nahodha, beki wa kati na kiongozi wa klabu, Laurent Koscielny.

Klabu hiyo hivi sasa inaonekana kwamba haipo kwenye mahusiano mazuri na mchezaji huyo. Koscielny ambaye ameonekana kuwa kinara wa uongozi wa Arsenal pale kwenye dimba la Emirates ameanzisha mgomo.

Mapema wiki iliyopita, Koscielny alikataa kusafiri na Arsenal kwenye maandalizi ya msimu mpya wa ligi Kuu England kwenda nchini Marekani. Majaliwa ya Koscielny ndani ya Arsenal yameripotiwa kuwa shakani baada ya kuingia kwenye mwaka wake wa mwisho wa mkataba wake, na kukiwa hakuna ishara ya kusaini mkataba mpya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 amekuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kurudi nchini Ufaransa katika Klabu ya Bordeaux.

Koscielny, ambaye alijiunga na Arsenal akitoka kwa miamba wa Ufaransa, Lorient mwaka 2010, amecheza mechi 350 kwa klabu hiyo.

Mkataba wake aliosaini mwaka 2017, unamalizika msimu wa 2019-20. Beki huyo wa kati aliumia goti wakati wa mchezo dhidi ya Atletico Madrid Mei mwaka 2018, na kumfanya ashindwe kucheza Kombe la Dunia nchini Urusi ambapo Ufaransa waliibuka kuwa mabingwa.

Hata hivyo, hili sio jambo rahisi kwa Arsenal kumwachia mchezaji huyo aondoke klabuni hapo.

Kila kundi la wachezaji lenye mafanikio kunakuwa na nguzo yake na ni wazi kwamba, pale Arsenal kwa hali ilivyo mchezaji huyu bado anaonekana kuwa kiungo muhimu zaidi.

Na ni wazi kwamba, klabu hiyo haitakuwa tayari kuingia mkenge wa kukubali kumwachia mchezaji huyu.

Kuondoka kwa Aaron Ramsey kwa uhamisho huru kwenda Juventus kipindi cha majira ya joto, kumemuacha Mfaransa huyo kuwa ndiye nguzo pekee ya klabu hiyo kwa sasa.

Kwa sasa hali ya Arsenal inamhitaji zaidi Koscielny na hata mmiliki wa klabu hiyo, Stan Kroenke analijua hilo vizuri.

Hata hivyo, kama hakuna mchezaji atakayeachwa kwenye kikosi cha klabu hiyo ambaye haijui vizuri falsafa ya Arsenal, kwa njia nyingi ile Arsenal halisi itaanza kukumbuka zama za kina Tony Adams na Patrick Viera, kuliko kuangalia upande gani wa kwenda.

Koscielny amecheza mechi 350 hapo Arsenal tangu aliposajiliwa mwaka 2010 kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 8.45 na amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia kwenye himaya yake. Pia alionyesha umuhimu wake wakati alipofunga kwenye fainali ya Kombe la FA mwaka 2014, ambapo alifunga bao la kusawazisha dhidi ya Hull City.

Uzoefu wake kwenye safu ya ulinzi ya Arsenal unamfanya kuwa mchezaji pekee kwenye kikosi hicho ambaye mwenye uzoefu wa kushinda mataji. Inaeleweka kwamba, kocha, Emery Unai anajaribu kujenga himaya yake kwa miamba hao wa London Kaskazini baada ya kuchukua mikoba ya Arsene Wenger ambaye alikuwa na imani kubwa na wachezaji vijana.

Falsafa ya kuwatumia zaidi wachezaji vijana pale kwenye dimba la Emirates kuendelea, baada ya kutangazwa kwa usajili wa kinda mwenye umri wa miaka 18, Gabriel Martinelli kutoka klabu ya nchini Brazil ya Ituano kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 6.

Falsafa hiyo ya kuwatumia wachezaji vijana pia inaendelea huku wakiwa kwenye harakati za kutaka kumsajili beki wa kati, William Saliba kutoka Saint-Etienne.

Usajili wa makinda haya na kuwapandisha wachezaji kama Reiss Nelson, Joe Willock, na Emile Smith Rowe bado kuna umuhimu wa kuwa na viongozi wenye uzoefu kama Koscielny. Kama Emery ataendelea kutaka kutumia mfumo wa msimu uliopita wa kuwategemea Shkodran Mustafi na Konstantinos Mavropanos, bado safu ya ulinzi ya Arsenal haitakuwa imara.

Kumpoteza beki kama Koscielny kwenye kundi la Arsenal linaweza kuwa pigo kubwa zaidi kwa kikosi hicho msimu ujao.

Harakati zao za kutafuta nafasi ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya zinaweza zisifanikiwe. Ukweli ni kwamba Koscielny bado ni mchezaji, kiongozi na beki muhimu zaidi kwa Arsenal.

## USILOLIJUA

MARA ya mwisho kwa Timu ya Taifa ya Nigeria (Super Eagles) kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika ilikuwa ni mwaka 2013. Mwaka huo pia vigogo hao wa Afrika Magharibi walishinda taji hilo.





## HABARI MBEYA

# H'shauri zatakiwa kutatua migogoro

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amezitaka halmashauri zote mkoani humo kutatua migogoro baina ya viongozi na kuweka nguvu ya pamoja katika ukusanyaji mapato ili kuziwezesha kujiendesha zenyewe badala ya kutegemea Serikali Kuu.

Chalamila alitoa kauli hiyo juzi wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani cha Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, kilicholenga kupokea na kujadili hoja za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2018/2019.

Alisema ili halmashauri ifikie lengo la ukusanyaji mapato lazima umoja na ushirikiano uimarishwe baina ya viongozi wakiwamo madiwani, mkurugenzi na wakuu wa idara badala ya kuendekeza migogoro isiyo na tija inayosababisha halmashauri kupata hati ya mashaka.

"Mara kwa mara nimekuwa nikitatua migogoro kwa viongozi wangu huku wilayani sijajua hasa sababu inayosababisha wakagombana, nawaomba kuanzia sasa acheni hayo mambo chapeni kazi kwa ushirikiano na upendo nyie ni ndugu na yeyote atakayeleta kiburi naomba nipewe jina lake ili nimshughulikie," alisema Chalamila.

Alishauri kuwa ili halmashauri ziweze kujiendesha, lazima zijifunze kujitegemea kwa kutumia vyanzo vyake vya mapato vya ndani badala ya kutegemea msaada.

Aliitaka Halmashauri ya Rungwe kuwa wabunifu kwa kutafuta vyanzo mbalimbali vya mapato kwa kuwashirikisha wadau ili kuiondoa hati chafu walioipata.

Akitoa taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali mbele ya baraza hilo, Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Nje Kanda ya Mbeya, Mohamed Bakari, alisema kwa miaka mitatu mfululizo Halmashauri ya Rungwe imepata hati safi, lakini kwa mwaka wa fedha 2017/18 imepata hati ya mashaka.

Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja, aliwataka wataalamu wilayani Rungwe kushirikiana na Mkurugenzi ili kuondoa doa la kupata hati chafu na kuahidi kuwachukulia hatua wote watakaokaidi agizo la serikali.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Rungwe, Loema Peter, alieleza kusikitishwa halmashauri yake kupata hati isiyoridhisha na kuahidi kusimamia maagizo yote yaliyotolewa kwa maslahi mapana ya wananchi.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), January Makamba (kushoto), akizungumza na wahandisi wa mradi wakati wa ziara yake ya siku moja katika Bonde la Mto Rufiji ambapo ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa maji unafanyika, lengo ikiwa ni kutembelea vyanzo vyote vya maji vinavyoelekea kwenye Mto Rufiji. (Katikati) ni Mhandisi John Masiko kutoka TECU, (kulia ) ni Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TCRA yabaini wasajili laini za simu hawana vibali

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Nyanda ya Juu Kusini, imefanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye vituo ambavyo vinasajili laini za simu jijini Mbeya, nakubaini wanaotoa huduma hiyo hawana vibali kutoka kwenye kampuni za simu na wengine wanawezesha uhalifu kufanyika kwa kusajili laini bila kitambulisho chochote.

Maofisa wa TCRA mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wakishirikiana na Mkuu wa TCRA Kanda, Mhandisi Asajile John, walitembelea vituo mbalimbali vinavyosajili laini ili kuhakikisha wanaofanya shughuli za usajili wa laini za simu ni watu ambao wamethibitishwa na kampuni za simu pamoja na kuwa na vibali vya kampuni husika.

Mhandisi John alisema kwenye ukaguzi huo walibaini uwepo wa mawakala ambao wanatoa huduma ya kusajili laini kutokuwa na sifa ya kufanya kazi hiyo kwa sababu hawana uthibitisho kutoka kwenye kampuni za simu ambazo wanasajili laini.

Alisema walibaini baadhi yao kusajili laini bila kitambulisho cha aina yoyote hali ambayo alidai inaweza kuchochea kufanyika kwa vitendo vya uhalifu kupitia mitandao ya simu.

Kutokana na hali hiyo alizitaka kampuni za simu nchini kuhakikisha zinatoa usajili kwa mawakala wao wanaosajili laini ili kuepuka ukiukwaji wa sheria na mtu yeyote anayefanya kazi ya kusajili laini bila utambulisho wa kampuni husika anaweza kutozwa faini ya shilingi milioni saba au kifungo cha miaka miwili jela ama vyote kwa pamoja.

Baadhi ya mawakala wanaosajili laini waliomba kujua kama inatakiwa kuwa na utambulisho kwa kampuni zote ambazo wanasajili laini zao au kampuni moja na kujibiwa kuwa utambulisho wa kampuni zote ambazo zinafanya usajili wa laini zake.

# Watafiti A/ Mashariki wajadili utafiti endelevu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATAFITI na wahasibu kutoka vyuo vikuu vya nchi za Kenya, Uganda na Tanzania na Chuo Kikuu cha Kassel, kilichopo nchini Ujerumani, wamekutana jijini hapa kujadili na kuwa na uelewa wa pamoja namna ya kutumia fedha za utafiti ili kuboresha utafiti unaofanyika na kuwa na tija na endelevu.


Akizungumza na Nipashe juzi, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Profesa Aloyce Mvuma, alisema kikao kazi hicho kimeshirikisha wahasibu na watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kassel kilichopo nchini Ujerumani, Chuo Kikuu cha Jomo Kenyatta nchini Kenya, Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda pamoja na vyuo vikuu kutoka mikoa ya Morogoro, Mbeya na Iringa, na Tanzania kwa ujumla.

Alisema lengo la kikao kazi hicho ni kuwa karibu kati ya wahasibu na watafiti ili utafiti unaofanyika uweze kuwa na ufanisi na kiwango kilichokusudiwa.

Aliongeza kuwa kikao hicho kinalenga kujengeana uwezo wa kiutendaji hususani kwa watafiti ambao bado hawana uwezo zaidi, lakini pia kupeana mbinu kwa watafiti wabobezi ili malengo ya kiutafiti yaweze kufikiwa na hatimaye kuleta matokeo chanya.

Mhadhiri Mwandamizi Idara ya Ujenzi Mazingira kutoka MUST, Dk. Zakaria Katambala, alisema kikao kazi hicho kitaongeza ufanisi katika utafutaji wa miradi na utekelezaji wake huku Dk. Erick Ronoh, kutoka Chuo Kikuu cha Jomo Kenyatta akisema kikao hicho kitaleta tija kwenye utafiti katika nchi hizo.

Kikao kazi hicho ambacho kinashirikisha wahasibu na watafiti wa vyuo vikuu kutoka baadhi ya nchi za Afrika Mashariki kilifanyika kwa siku mbili katika Chuo Kikuu cha MUST.





# Watakiwa kutumia vyema fedha wanazokopa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WANACHAMA waliopo kwenye vikundi vya hiari vya akiba na mikopo (SACCOS), wameshauriwa kutumia fedha wanazokopa kwa ajili ya maendeleo.

Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo KKKT Arusha Road Saccos Ltd, Ibrahim Sumbe, alitoa wito huo alipokuwa akisoma taarifa kwenye mkutano mkuu wa mwaka 2019.

Sumbe alisema Saccos nyingi zinakumbana na changamoto mbalimbali ikiwamo wanachama wake wanapokopa fedha wanashindwa kurejesha kutokana na kutofanya vitu vya maendeleo ambavyo vingewawezesha kurejesha kwa wakati.

Alisema wamekuwa wakisababisha kuwapo kwa usumbufu kulazimika kutumia nguvu kubwa kuwafuatili, hivyo ni vyema wanapokopa wakafanyia vitu ambavyo vitawaletea maendeleo na si vinginevyo.

Alisema kuwa licha ya saccos hiyo kufanya vizuri kwa kufuata miongozo ya uendeshaji bado inakabiliwa na changamoto ya ucheleweshwaji wa marejesho ya mikopo.

"Chama chetu kina wanachama wachache wanaochelewesha marejesho yao ya mikopo, tunawaomba wanachama wote mjitahidi kuwa waaminifu na mrejeshe mikopo yenu kwa wakati, kwani kwa kutorejesha mikopo hiyo mnakiletea chama hasara, na kitashindwa hata kuwalipa nauli za mikutano wanachama ambao wanachelewesha marejesho yao," alisema Sumbe.

Sumbe alisema ukaguzi wa hesabu za chama hicho hufanyika kila mwaka na wakaguzi kutoka Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika(COASCO).

Mkaguzi wa COASCO Mkoa wa Dodoma, Dorah Meta, alisema shirika hilo limekuwa likifanya kazi zake vizuri kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji wa shughuli za vyama vya ushirika.

Aidha, alisema pamoja na kuwa na utendaji mzuri wa Saccos hiyo bado kuna changamoto kubwa katika kipengele cha mikataba kati ya Saccos hiyo na watumishi, jambo ambalo bado linatakiwa kufanyiwa kazi.

Aliwataka wanachama kuhakikisha wanalipa madeni kwa wakati ili kuepukana na usumbufu unaoweza kujitokeza na kusababisha Saccos kufanya vibaya.

Mwenyekiti wa mkutano huo, Witness Msuya, aliutaka uongozi kuhakikisha unafuatilia madeni na kuwataka wanachama wote kuwa waaminifu na kuwafuatilia wale waliokopa.

# Wenye ulemavu watakiwa kuchangamkia fursa sasa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewataka watu wenye ulemavu kuchangamkia fursa za mikopo ya asilimia mbili inayotolewa katika halmashauri nchini ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani, Meja Jenerali Jacob Kingu, wakati wa kongamano la kitaifa la lugha ya alama kwa vyombo vinavyosimamia haki, ulinzi na usalama jijini Dodoma.

Kingu alisema kundi hilo linapaswa kuchangamkia fursa hizo kwa sababu mikopo hiyo ipo na inatolewa kulingana na taratibu na sheria zilizokuwapo kwa lengo la kuwainua kiuchumi katika shughuli mbalimbali wanazofanya.

Alisema wanapaswa kuifikia mikopo hiyo ambayo ni haki yao kuipata na itamwezesha kila mmoja kufanya jambo la msingi ikiwamo biashara.

Alifafanua kuwa hakuna sababu ya wao kurudi nyuma kwa sababu taifa linawatambua kinachotakiwa ni kuangalia fursa inayowafaa na kuanza kuifanyia kazi ambapo itawasaidia kujikwamua kiuchumi ikiwamo kujiongezea kipato.

"Serikali inatambua mchango unaotolewa na walemavu ndio maana unaona iko mstari wa mbele kuwakumbuka katika shughuli za kijamii na nyie msisite kutoa ushirikiano," alisema Kingu.

Alisisitiza serikali itaendelea kulinda na kutetea haki za msingi za kundi hilo ili kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Amina Mpatu, alisema wamefanikiwa kutambua walemavu zaidi ya 300,000 katika mwaka 2017/18 wakiwamo viziwi jambo ambalo litawasaidia kupanga mpango mkakati wa kuwasaidia.

Alisema pia watoto wenye ulemavu zaidi ya 16,000 wametambuliwa na wengi wao wamefanikiwa kuwaunganisha katika matibabu waliostahili ikiwamo kuwapa ushauri.

Aliiomba jamii kuacha kuwaficha watu wenye ulemavu kwa kuwa serikali ipo mstari wa mbele kuhakikisha wanapata haki zao za msingi ikiwamo elimu, ili waweze kutoa michango ya maendeleo katika jamii.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akihakiki deni la kodi ya pango la ardhi la kampuni ya Birchard Oil Limited pamoja na Meneja Uhusiano wa kampuni hiyo, Arshad Jetha (kushoto), wakati wa operesheni za kuwatembelea wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi katika mkoa wa Mwanza mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Kodi wizarani, Denis Masami. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# CCM yajipanga kushinda kwa kishindo S/Mitaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya Dodoma Mjini kimejipanga kuhakikisha kinapata ushindi mkubwa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka huu kwa kutatua kero na changamoto za wananchi.

Hayo yalielezwa jana na Mwenyekiti wa CCM Wilaya hiyo, Robert Mwinje, wakati wa hafla ya kukabidhi vifaa vya uenezi(spika) na bendera kwa kata zote 41 vilivyotolewa na Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu.

Alisema watahakikisha CCM inashinda mitaa yote ya wilaya hiyo kwa kuwa wamekuwa wakitatua na wanaendelea kutatua changamoto zinazowakabili wananchi. "Ili kuweza kushinda lazima tujipange, tutapiga hesabu mezani tunashindaje huu uchaguzi, rai yangu kwenye kata hakikisheni tunapata wagombea wenye sifa, sitakubali kubeba gunia la mchanga," alisisitiza.

Aliwataka viongozi wote waliopo serikalini na wawakilishi wa wananchi wanapaswa kuhakikisha wanatatua matatizo ya wananchi kuanzia ngazi ya chini ili kutengeneza uhalali kwa wananchi watakapoomba ridhaa kwenye chaguzi zijazo.

Kwa upande wake, Mavunde ambaye pia ni Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, alisema matatizo ya wananchi wa Dodoma ndio yaliyomsukuma kuomba kuwatumikia na kusisitiza kuwa ataendelea kuwa mtumishi wao.

"Sisi viongozi tuliyopewa dhamana na chama heshima yetu sio kupendeza na mashati ya kijani wala sio kuimba sana, bali ni kuhakikisha tunatatua kero za wananchi na hiyo ndio heshima ya CCM, hata tupendeze vipi kama wananchi wetu wana shida hatujatimiza wajibu wetu," alisema.

Alibainisha vifaa alivyotoa vina thamani ya Sh. milioni 19.5 ikiwa ni maandalizi ya kampeni ya kisayansi ambayo amepanga kuifanya katika Jimbo la Dodoma ili kuhakikisha CCM inashinda kwa kishindo.

Alisisitiza amejipanga kuhakikisha anaendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi na kutoa kura nyingi katika uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani mwaka 2020.

"Lazima chama kiendelee kutatua kero za wananchi kwa kuwa wananchi wamerudisha imani kwenye ofisi za chama wanapeleka matatizo yao, kuanzia ngazi ya kata tuyafanye haya, tukitatua changamoto zao hatuhitaji kutumia nguvu kwenye uchaguzi kwa kuwa tone moja la asali linavutia nyuki kwenye dumu la pombe," alisema.





Wanafunzi wa Shule ya Msingi Shishinulu iliyoko Kata ya Isaka katika Halmashauri ya Msalala, wakielekezwa namna ya ufugaji wa nyuki na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, George Charles. **PICHA NA SHABAN NJIA**

# ZBS yatakiwa kuzingatia viwango

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Kamati za Kitaalamu za Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), wametakiwa kuwa makini kwa kuzingatia sheria, kanuni na viwango ili kuendelea kuifanya Zanzibar kubaki salama katika masuala ya viwango vya ubora wa bidhaa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya ZBBS, Profesa Ali Seif Mshimba, alisema hayo wakati akifungua mafunzo kwa wajumbe hao kuhusu ubora wa viwango yaliyofanyika, mjini hapa. Alisema kamati hizo zinajukumu muhimu la kuwalinda watumiaji wa bidhaa, hivyo wanapaswa kuzingatia utaalamu wao na weledi ili kufanya kazi hiyo kwa ufanisi.

Alisema dhamana waliyonayo kwa jamii ni kubwa hivyo ufanyaji wa kazi wa pamoja na ushirikiano miongoni mwa wajumbe kutaiweka nchi katika mazingira salama na kuwa na bidhaa zenye viwango.

Kaimu Mkurugenzi wa ZBS, Haji Abdulhamid, alisema taasisi hiyo imetimiza wajibu wake wa kuwalinda wananchi dhidi ya bidhaa zisizo na viwango zinazozalishwa nchini.

Alieleza kuwa tayari bidhaa 191 zimepitishwa baada ya kukidhi viwango na nyingine 103 zimo katika mchakato wa kufanyiwa tathmini ya ubora wa viwango.

Washiriki wa mkutano huo walisema kuwa wanataka kuona kuwa ZBS inafanya kazi za kukagua ubora wa bidhaa hadi katika soko la Afrika Mashariki badala ya kuonekana uwezo wao wa kufanya kazi hiyo unaishia Chumbe.

Vile vile, wameshauri kuwapo kwa ushirikiano baina ya TBS na ZBS ili kuweza kufanya kazi kwa pamoja.

# Wataalamu wa kigeni majengo watakiwa kujisajili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MRAJISI wa Bodi ya Wahandisi, Wasanifu na Wakadiriaji majengo, Injinia Hawa Mzee Khamis, amesema wataalamu wa kigeni katika majengo mbalimbali hawajajisajili katika bodi hiyo jambo ambalo ni kinyume na sheria.

Akizungumza baada ya kutembelea na kukagua majengo manne ya serikali yanayojengwa katika Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, alisema kufuatia ziara hiyo wamegundua kuwapo kwa wataalamu wa ujenzi wanaofanya kazi hizo bila kusajiliwa na bodi.

Alisema pia wataalamu hao baadhi yao wamekuwa wakifanya kazi ambazo hawana utaalamu nazo hali inayoweza kusababisha athari katika majengo hayo.

"Wapo wataalamu ambao wanafanya kazi sio zao ambazo hawajasomea hivyo kufanya kazi ambazo sio fani yako kunaweza kukasababisha athari nyingi ikiwamo kufeli kwa majengo," alisema.

Aliwataka wataalamu hao kujisajili katika bodi hiyo ili kuepukana na matatizo mbalimbali. Naye Msaidizi wa Mrajis wa bodi hiyo, Injini Mansor Rashid, alisema baadhi ya wajenzi wanaosimamia majengo hawajasajiliwa hivyo ni vyema kusajiliwa ili kuwa na majengo sanifu na salama.

"Mikakati ya bodi hii ni kuwafuatilia watalamu hao na kuona kwamba wanasajiliwa na bodi," alisema.

Pia alisema katika kazi za ujenzi wa majengo yanayoendelea, msimamizi mkuu wa majengo hayo ni wataalamu kutoka nje wakati wazalendo wenye taaluma hiyo wapo, lakini wanakosa fursa hiyo.

"Wataalamu wazawa wapo hivyo tunawaomba hao waje kujisajili katika bodi ili kupata fursa mbalimbali za ujenzi na usimamiaji wa majengo," alisema. Kwa upande wao wasimamizi na wasanifu wa majengo hayo walieleza kuwa miongoni mwa vikwazo vinavyowakabili katika utendaji wa kazi zao ni pamoja na tatizo la upatikanaji wa mchanga kwa wakati na ucheleweshaji wa kushusha vifaa vya ujenzi katika Bandari ya Malindi.

"Kumekuwa kukichukua muda mrefu wa ushushaji wa vifaa bandarini hali ambayo inasababisha kutomalizika kwa wakati uliopangwa kwa majengo," alisema.

Bodi hiyo ilitembelea na kukagua ujenzi wa jengo la Mamlaka ya Usimamizi wa Maji na Nishati Zanzibar (Zura), ujenzi wa jengo la biashara, Michenzani, ujenzi wa jengo la maduka Kisonge na ujenzi wa hoteli iliyopo uwanja wa ndege ili kutambua kasoro zinazojitokeza ikiwamo uhalali wa wasimamizi wa majengo pamoja na kuwapa maelekezo wataalamu wanaosimamia majengo hayo.

# Wanawake watakiwa kudai urithi kuepuka dhuluma

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISA Ardhi kutoka Kamisheni ya Ardhi, Haji Mrisho, amewataka wanawake wanaofiwa na waume zao kudai urithi wao mapema ili kuepuka kudhulumiwa.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Matendwe, katika mkutano wa umiliki wa ardhi kwa wanawake, alisema wanawake wengi Zanzibar wanaofiwa na waume zao huwa hawadai haki yao ya urithi hata kama mume aliacha mali ikiwamo nyumba au viwanja.

Alisema kukaa kwao kimya kunatoa mwanya kwa watu ambao sio waaminifu kuwadhulumu mali hizo.

"Wengi wa wanawake wakishafiwa huondoka katika familia ya mume na huenda katika familia zao hata kama mume aliacha nyumba," alisema.

Vile vile, aliwataka wanawake wa kijiji hicho na maeneo mengine kuhakikisha kuwa mali walizoacha marehemu waume zao wanapewa urithi na endapo watadhulumiwa kutokaa kimya, waende katika vyombo vya sheria.

Pia alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, miongoni mwa sehemu ya mikakati yake ni kuwataka wananchi kutafuta hatimiliki ya ardhi kwa ajili ya kuitumia kwa shughuli za kiuchumi na uwekezaji.

Alisema migogoro mingi inayojitokeza moja ya chanzo chake kikubwa ni kukosekana kwa hatimiliki ya ardhi zaidi vijijini.

"Serikali imeanzisha utaratibu mpya wa kuwataka wananchi wake kutafuta hatimiliki ya ardhi ikiwamo mashamba kwa ajili ya kuepuka migogoro," alisema.

Sheha wa Shehia ya Matemwe Kaskazini, Denge Khamis Silima, alisema wanawake wengi wa vijijini hawajahamasika kuomba hatimiliki kwa ajili ya kumiliki ardhi kihalali.

Alisema thamani ya ardhi imeongezeka hivi sasa kutokana na matumizi ya kiuchumi na uwekezaji kwa hivyo njia pekee ya kuepuka migogoro ni kutafuta hatimiliki ya ardhi.

"Hakuna vikwazo kwa wanawake kupata hatimiliki ambayo itawawezesha kumiliki ardhi kihalali na kuitumia kwa shughuli za kiuchumi na uwekezaji...tatizo wanawake hawajahamasika hadi sasa," alisema.

Wakizungumza katika mkutano huo kuhusu umiliki wa ardhi, Tatu Muhidin Mussa, mkazi wa kijiji hicho, alisema ameomba hati ya kumiliki ardhi ya sehemu ya shamba lake na huu ni mwaka wa pili hajafanikiwa kuipata.

Alisema baadhi ya wananchi wamekuwa na malalamiko makubwa ya kuwapo kwa urasimu wa kupata hatimiliki ambao unawavunja moyo.

"Tunaiomba serikali kuondoa urasimu wa hatimiliki ya ardhi ili wananchi wajitokeze na kuwasilisha maombi mengi zaidi," alisema.

## Wananchi kusahau kero maji Septemba

**Na Magreth Magosso,** KIGOMA

NAIBU Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, amewatoa hofu wakazi wa Mji Mdogo wa Mwandiga mkoani Kigoma juu ya changamoto ya ukosefu wa maji iliyodumu kwa zaidi ya miongo mitano.

Alitoa ahadi hiyo kwenye mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Mbunge wa Kigoma Kaskazini, Peter Serukamba, kwa lengo la kuelezea utekelezaji wa ahadi zake kwa wananchi wa mji huo, ikiwamo kuondoa kero ya maji.

"Wizara yetu ni ya maji sio ya ukame, mbunge wenu ametubana tunasema, ifikapo Agosti mwaka huu fedha zimeongezwa kwa ajili ya kuchimba mitaro na kutandaza mabomba ambapo Septemba mwaka huu mtasahau kero ya maji," alifafanua Aweso.

"Sindano ndogo ndio inayoshona makoti, Rais John Magufuli anahitaji wananchi waondokane na kero ya maji na ondoeni hofu kwa kuwa wakazi wa Mwandiga wataunganishwa na mtandao wa maji kutoka chanzo cha Ziwa Tanganyika na wakazi wa Kiganza wataendelea na matumizi ya maji katika chanzo cha Mkongoro One."

"Wali wa kushiba huonekana mezani, mbunge wenu anachapa kazi na mbunge anayewajibika ndiye anatakiwa na jamii yake, lakini kazi ya jamii haikosi fitina," alisema Naibu Waziri na kuongeza:

"Ondoeni shaka juu ya kero ya maji, siwezi kudanganya, fedha ipo na maji mtapata na shukuruni neema mnayopatiwa na Serikali ya Awamu ya Tano ya Rais Magufuli."

Aweso aliongeza kwa kusema sababu ya Mji Mdogo wa Mwandiga kutumia chanzo cha maji kutoka Manispaa ya Kigoma Ujiji ni kutokana na mradi mkubwa wa maji wenye fedha zaidi ya Sh. bilioni 42 ambao utaongeza kasi ya ujazo.

Serukamba alisema mpaka sasa usanifu umefanyika na Agosti utekelezaji wa mtandao wa kuchimba mitaro na kusambaza mabomba utaanza na ifikapo Septemba wakazi wa mji mdogo watasahau kero hiyo iliyodumu zaidi ya miongo mitano.

# Marufuku wanunuzi dengu kununua kwa wakulima

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI imepiga marufuku wafanyabiashara wa zao la dengu mkoani Shinyanga kwenda kununua kiholela moja kwa moja kwa mkulima.

Kwa mujibu wa utaratibu, kwa sasa wanapaswa kulinunua kupitia kwenye vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS), na atakayebainika kwenda kinyume, atachukuliwa hatua kali na kutaifishwa mzigo wake.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Ushirika Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika kutoka makao makuu, Benjamin Mwangwala, kwenye kikao cha wadau wa zao la dengu mkoani Shinyanga, wakati akitoa maelekezo ya serikali kuwa zao hilo litanunuliwa kwa njia ya mnada kupitia AMCOS.

Alisema serikali imedhamiria kumnufaisha mkulima na kumuinua kiuchumi, ndio maana imetoa mwongozo kuwa marufuku mfanyabiashara kwenda kununua dengu kwa mkulima moja kwa moja, badala yake anapaswa akalinunue zao hilo kupitia AMCOS ambapo wao ndio watanunua kutoka kwa mkulima.

"Naomba wafanyabiashara wote ambao huwa mnanunua zao hili la dengu mtii maagizo haya ya serikali tofauti na hapo tusije kulaumiana baadaye," alisema na kuongeza:

"Dhamira yetu ni kumnufaisha mkulima, pamoja na nyie muweze kupata bidhaa yenye ubora kwa sababu AMCOS zitakuwa zinanunua bidhaa safi."

"Zao hili pia litakuwa linauzwa na vyama vya msingi vya ushirika kwa njia ya mnada ambapo wafanyabiashara waliopitishwa na serikali kuwa wanunuzi wa dengu mara baada ya kukidhi vigezo na masharti, ndio watakuwa wanashindana, na mshindi atapewa kibali cha kulipa pesa na kukabidhiwa bidhaa yake," aliongeza. Aidha, alisema baada ya mshindi kulipa pesa na kukabidhiwa bidhaa yake, ndipo AMCOS nacho kitaanda malipo ya kila mkulima (stakabadhi gharani) na kumpatia pesa yake bila ya kupunjwa bei.

Mmoja wa wafanyabiashara wa dengu, Hassani Mboje, alidai kutokubaliana na maagizo hayo ya serikali kwa maelezo imekuwa ghafla sana, ni bora wangepewa zaidi kwa kuwa walishakopa fedha benki kwa ajili ya kununua dengu kwa mkulima na kubainisha wataingia hasara.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Shinyanga (SHIRECU), Richard Luhende, alisema msimu wa ununuzi wa dengu mkoani humo unaanza leo na kubainisha bei elekezi ni shilingi 800 kwa kilo moja, na kwamba siku ya mnada ikifika wafanyabiashara watakuwa wanatangaziwa.



Wafanyakazi wa Benki ya Exim Tanzania wakimuhudumia mmoja wa wateja waliotembelea banda la huduma za benki hiyo, kwenye Mkutano Mkuu wa Kimataifa wa wadau wa korosho mkoani Mtwara mwishoni mwa wiki. Benki hiyo ni miongoni mwa wadau wakubwa wa zao la korosho nchini, na imekuwa ikitoa huduma za kifedha kwa wakulima na wafanyabiashara wa zao hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kasi ujenzi hospitali yamkera Jafo

**Na Idda Mushi,** GAIRO

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Seleman Jafo, ameeleza kutoridhishwa na kasi ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Gairo mkoani Morogoro.

Kutokana na kusuasua huko, amesema mradi huo ni kichefuchefu kwa kuwa kila mara anapokwenda kukagua, sababu kubwa wanayoitoa ni changamoto ya maji ambayo huahidi kuifanyia kazi bila utekelezaji.

Jafo alisema hayo baada ya kuwasili mkoani Morogoro kwa lengo la kukagua utekelezaji wa ujenzi huo, akabainisha kuwa licha ya kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ndani ya muda wa miezi 18 aliotoa, kukamilishwa kwa ujenzi wa hospitali 67 za wilaya na vituo 352 vya afya, amebaini ujenzi huo umekamilika kwa asilimia 90 isipokuwa baadhi ya maeneo.

Alisema katika baadhi ya wilaya kwenye mikoa ambako amepita, hajaridhishwa kabisa na kasi inayoendelea ikiwamo mkoa wa Mtwara katika Hospitali ya Nanguruwe ambako wako nyuma na kushindwa kuanza ujenzi kutokana na uzembe wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo na kutaka viongozi na watendaji kubadilika na kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

"Gairo ni kichefuchefu kwa sababu sijaridhika kabisa, sitaki kuwa mnafiki, wajitathmini wajirekebishe. Imani yangu ni kuwa watajirekebisha hadi Julai 30 watakuwa wamemaliza. "Wakati naondoka wanasema wamechelewa kwa kwa shida ya maji na wanalifanyia kazi. Wanasahau mara ya mwisho mwezi wa pili nilipopita walisema tatizo lilikuwa maji na wameshavuta hakuna tatizo. Sasa ninarudi tena wanasema shida ni maji," alisema.

Alipongeza baadhi ya wilaya zikiwamo Mvomero na Singida ambazo alielezea kuridhishwa na kasi ya ujenzi unaoendelea na kutoa ahadi Julai 30 kwenye maeneo walikokwama kukamilisha ujenzi huo.

Waziri Jafo alibainisha viongozi katika maeneo husika hawana chochote cha kusingizia kukwamisha ujenzi huo, kwani serikali iko makini kwenye utekelezaji wa miradi yake ya maendeleo.

Alisema serikali ilitoa Sh. bilioni 105 kufanikisha ujenzi huo na kila mkoa ulishakabidhiwa Sh. bilioni 1.5 kukamilisha hospitali hizo.

Jafo pia alisema fedha zaidi zimeongezwa ili kujenga hospitali mpya zingine 27 za wilaya na kufanya jumla ya hospitali mpya kufikia 94 ndani ya kipindi cha miaka miwili, jambo ambalo lilikuwa nadra kwa kufanikisha ujenzi huo ndani ya kipindi kifupi tangu kabla ya Uhuru. Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Stephen Kebwe, alisema wataongeza kasi ya ufuatiliaji na usimamizi ili maeneo yenye changamoto ikiwamo Gairo, yakamilishe ujenzi huo na kwamba ana imani tatizo la maji likitatuliwa, shida hiyo itakuwa imepatiwa ufumbuzi.

HABARI KIMATAIFA

## Macron aupa umuhimu ushirikiano kijeshi Ulaya

**PARIS,** Ufaransa

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, kwa mara nyingine amelipa umuhimu mkubwa suala la ushirikiano wa kijeshi barani Ulaya kwenye gwaride la siku kuu ya kitaifa ya Ufaransa, huku kukiongezeka wasiwasi na Marekani.

Mahusiano ya karibu ya kijeshi baina ya mataifa ya Ulaya limekuwa miongoni mwa sera za nje ambazo Macron anazipa kipaumbele, na hajaonyesha kutetereka licha ya kuongezeka kwa mvutano na Ujerumani na Uingereza kujitoa Umoja wa Ulaya.

Hii ni mara ya pili Macron anatoa mwito huu, baada ya mwaka jana kuzungumzia mbele ya Rais Donald Trump wa Marekani hatua iliyovuruga mahusiano baina yao hadi sasa.

Viongozi wakuu wa Umoja wa Ulaya ikiwa ni pamoja na kansela wa Ujerumani, Angela Merkel na Waziri Mkuu wa Uholanzi, Mark Rutte, wameungana na Macron kutazama gwaride hilo la kila mwaka karibu na Ikulu ya Champs Elysees katika kuadhimisha kumbukumbu ya uvamizi wa ngome ya Bastille mjini Paris wakati wa mapinduzi ya Ufaransa. **VOA**

## Watu 33 wauawa katika mlipuko Somalia

**MOGADISHU,** Somalia

WATU 33 wakiwamo wageni wameuawa katika shambulizi la bomu la kujitoa muhanga katika hoteli ya maarufu ya Medina mjini Kismayo, Somalia.

Wanamgambo wa al-Shabaab wanadai kuhusika na shambulizi hilo.

Vyanzo rasmi vya habari vimesema ofisa wa ngazi ya juu kimkoa amesema Jumamosi mshambuliaji wa kujitoa muhanga aliligonga gari lililokuwa na milipuko katika hoteli ya Medina Ijumaa.

Ameeleza kuwa watu kadhaa wenye silaha nzito walilazimisha kuingia ndani ya hoteli hiyo huku wakirusha risasi. Hoteli hiyo ilikuwa imezingirwa kwa takriban saa 12 na mapigano kati ya majeshi ya nchi hiyo na washambuliaji hao yalimalizika alfajiri ya Jumamosi.

Taarifa kutoka kwa Rais wa Jimbo, Ahmed Mohamed, zinasema kuwa Wakenya watatu, Watanzania watatu, Wamarekani wawili, Muingereza mmoja na raia mmoja wa Canada ni kati ya watu 26 waliouawa.

Pia taarifa hiyo imeeleza kuwa kuna pia raia wawili wa China waliokuwa wamejeruhiwa.

Naye ofisa wa usalama wa jimbo hilo Mohamed Abdiweli amesema majeshi ya usalama yamefanikiwa kuudhibiti mji huo na gaidi wa mwisho alipigwa risasi na kufariki. **VOA**

# Safari muhimu za kisayansi zazinduliwa nchini Urusi

**RUSSIA,** Urusi

MOJA ya safari muhimu zaidi za kisayansi nchini Urusi kuwahi kushuhudiwa baada ya utawala wa Kisovieti imezinduliwa kutoka eneo la Baikonur.

Spektr-RG telescope, ni kifaa chenye darubini ya anga za mbali ni uvumbuzi uliokamilika kwa ushirikiano na Ujerumani ambayo inatarajia kupima nishati ya joto kote angani na kutoa taarifa.

Watafiti wanasema taarifa hii itasaidia kupata muundo wa dunia kwa upana zaidi, matumaini ni kwamba Spektr-RG kitaweza kutoa mtizamo mpya juu ya upana zaidi.

**Wakati gesi inapoanguka katika mashimo hayo, huwa na joto kali na kumeguka na kugeuka kuwa joto kali.**

Kinatarajiwa pia kutambua idadi mpya ya vyanzo vya nishati, kama vile mashimo makubwa meusi yaliyopo katikati mwa nyota nyingi.

Wakati gesi inapoanguka katika mashimo hayo, huwa na joto kali na kumeguka na kugeuka kuwa joto kali. Mionzi yake hatimaye husababisha hali mbaya ya joto kinatarajiwa pia kutambua idadi mpya ya vyanzo vya nishati, kama vile mashimo makubwa meusi yaliyopo katikati mwa nyota nyingi.

Wakati gesi inapoanguka katika mashimo hayo, huwa na joto kali na kumeguka na kugeuka kuwa joto kali.

Mionzi yake hatimaye husababisha hali mbaya ya joto kwa dunia. Darubini ya Spektr-RG inatarajiwa kugundua takribani mashimo milioni tatu makubwa sana meusi angani wakati itakapokuwa angani hadi mwisho wa maisha yake. **BBC**



Waziri wa Mambo ya Nje wa Iraq, Mohamed Alhakim (kulia), akiwa na Mkuu wa Sera ya Mambo ya Nje wa Umoja wa Ulaya, Federica Mogherini, baada ya mazungumzo katika Wizara ya Mambo ya Nje jijini Baghdad, juzi. **PICHA: AP**

# Mapya ya Kim Darroch dhidi ya Trump

**NEW YORK,** Marekani

RAIS Donald Trump ameachana na mkataba wa nyuklia wa Iran ili kumkera Barack Obama, kwa mujibu wa barua ya siri iliyovuja kutoka kwa aliyekuwa balozi wa Uingereza nchini Marekani.

Sir Kim Darroch alielezea hatua ya Trump kuvunja mkataba huo kama "ubadhirifu wa kidiplomasia" kwa mujibu wa gazeti la Mail on Sunday.

Gazeti hilo linadai kuwa barua hiyo iliandikwa baada ya aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza, Borris Johnson, kuidai Marekani mwaka 2018 kusalia ndani ya makubaliano hayo.

Barua hii mpya inavuja katika kipindi ambacho polisi nchini Uingereza wameonya juu ya uchapishwaji wa barua hizo.

Barua ya kwanza kutoka kwa balozi huyo ambayo ilikuwa inakosoa utawala wa Trump ilivuja wiki moja iliyopita na kusababisha majibizano ya hasira baina ya Uingereza na Marekani.

Majibizano hayo yamesababisha Sir Kim kujiengua kwenye wadhifa wake licha ya serikali ya Uingereza kupitia Waziri Mkuu Theresa May kueleza kuwa inamuunga mkono. **BBC**

## Shehena mfumo silaha yawasili

**ANKARA,** Uturuki

WIZARA ya Ulinzi ya Uturuki imetangaza kuwasili kwa sehemu ya kwanza ya shehena ya mfumo wa silaha za ulinzi wa anga aina ya S-400, kutoka Russia.

Ndege ya mizigo ya Russia, iliwasili ikiwa imebeba shehena ya mfumo wa silaha hizo katika uwanja wa ndege wa kijeshi wa Murted, Ankara.

Silaha hizo kutoka Russia, za kwanza kuuzwa kwa mwanachama wa Umoja wa Kujihami wa Ulaya (Nato), imesababisha wasiwasi kwamba Uturuki inakaribia ushawishi wa Moscow.

Uturuki ilikuwa imekataa kuzingatia masharti ya Marekani kujiondoa kwenye mkataba huo, ulioripotiwa kugharimu zaidi ya dola bilioni 2. **VOA**

# Majaliwa awapa matumaini wakulima wa tumbaku soko

**Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali inaendelea kutafuta masoko kwa ajili ya zao la tumbaku nchini ili kuwawezesha wakulima kuzalisha kwa wingi na kuinua kipato.

Ameyasema hayo jana wakati akizungumza na wadau wa zao la tumbaku kutoka mikoa mbalimbali. Mkutano huo umefanyika mjini Tabora.

Waziri Mkuu alisema tayari serikali imeshafanya mazungumzo na nchi mbalimbali zikiwamo za Vietnam na Misri ambayo imeahidi kuisaidia Tanzania kupata wanunuzi.

Kadhalika, Waziri Mkuu amesema kuwa serikali inaendelea na mazungumzo na kampuni zinazonunua tumbaku nchini ili zingeze kiwango cha ununuzi ili kuwawezesha wakulima kuzalisha zaidi.

"Wakulima wanahitaji kuzalisha zaidi lakini wanakwamishwa na kiwango wanachowekewa (ukomo wa uzalishaji) na wanunuzi ambacho ni kidogo ukilinganisha uwezo wa wakulima katika kuzalisha zao hilo."

Hata hivyo, Waziri Mkuu alisema serikali inaendelea na mazungumzo na kampuni ya ununuzi wa tumbaku ya Tanzania Leaf Tobacco Company (TLTC) ili iendelee na ununuzi wa zao hilo.

Amesema awali kampuni ya TLTC ambayo ilikuwa ni miongoni mwa wanunuzi wa tumbaku nchini ilitoa kusudio la kutaka kuacha kununua zao hilo.

Pia, Waziri Mkuu alisema serikali inashirikiana na Malawi katika utafutaji wa masoko ya zao hilo na tayari kampuni za Malawi zimeahidi kununua tumbaku nchini.

Kwa mujibu wa Majaliwa, hayo ni miongoni mwa mafanikio ya ziara aliyoifanya Rais John Magufuli hivi karibuni nchini Malawi.

Waziri Mkuu aliwataka wakulima waendelee kuwa na subira.



Wateja wa Vodacom Tanzania wakipata maelezo kuhusu shughuli zinazofanywa na Vodacom Tanzania Foundation kutoka kwa watoa huduma wa kampuni hiyo katika Maonyesho ya 43 ya Biashara za Kimataifa Sabasaba, jijini Dar es Salaam juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Shirika lataka asilimia saba kutengewa mkaa endelevu

**Na Christina Haule,** MOROGORO

VIJIJI vinavyotekeleza mradi wa kuleta mageuzi katika sekta ya mkaa Tanzania (TTCS) vimetakiwa kuona umuhimu wa kutenga asilimia saba ya mapato yake ili kumlipa mtaalamu atakayewasaidia na kufanya mradi uwe endelevu licha ya ufadhili wake kukoma Novemba mwaka huu.

Hayo yalisemwa jana na Ofisa Biashara wa Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Hamza Nkumulwa, kwenye kikao cha madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ambapo alisema ikiwa watakuwa na mtaalamu mmoja kutoka Mjumita, itawasaidia kuendeleza shughuli zao za mkaa endelevu.

Alisema TTCS imeona uwapo wa mtaalamu mmoja kwa kila kijiji kilichokuwa na mradi tangu mwanzo utakaowasaidia wanavijiji hao kufuatia kuwa hata mradi huo utakaporudi kwa awamu ya tatu, vijiji vya zamani havitaendelea kupewa ufadhili.

Alivitaja vijiji hivyo ni Matuli, Mlilingwa Lulongwe, Diguzi na Tununguo ambapo alisema vijiji hivyo vimeanza kunufaika kwa kupata mapato ya mkaa endelevu hivyo si vibaya vikatenga kiasi cha pesa kwa ajili ya kuweka usimamizi utakaosimamiwa na uongozi wa halmashauri.

Naye Diwani wa Kolelo, Elidius Mbena, alivitaka vijiji vinavyonufaika na mradi kuwa na mkataba utakaowabana wataalamu watakaowachagua na kuwalipia ili kusiwe na mkanganyiko.

Aidha, alisema, kufuatia mpango mzuri ulioandaliwa na TTCS wao kama madiwani hawana nafasi ya kuupinga bali alisema, makubaliano yoyote yatakayofanyika yafuate misingi ya kisheria ili kuwasaidia wazalishaji wa mkaa na kuzidi kuleta ushawishi kwa wanavijiji wengine waliovutika na mradi huo.

Akizungumzia hilo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Kibena Kingo, alisema, suala hilo litapewa kipaumbele cha usimamizi wa halmashauri endapo wanavijiji vya mradi watakaridhia wao wenyewe.

Hivyo Mwenyekiti huyo ambaye pia ni Diwani wa Ngerengere aliwataka wataalamu wa halmashauri kushirikiana vyema na wataalamu kutoka TFCG kwenda vijijini kuwasikiliza wanavijiji waliopo kwenye mradi na kupata maoni yao kabla ya suala hilo kufikishwa kwenye baraza.

Naye Meneja Mradi wa TTCS, Charles Leonard, alisema, mradi huo umefanikiwa kuingiza zaidi ya Sh. milioni 800 kwa kipindi cha miaka miwili na nusu na kwamba ni wajibu wa wanavijiji kuona umuhimu wa kuangalia njia za kuendeleza mradi huo ili waendelee kuvuna mapato zaidi ya hayo.

## Wajasiriamali walivyowezeshwa na Tigo miaka 5

**Na Romana Mallya**

KAMPUNI ya mawasiliano Tigo Tanzania katika kipindi cha miaka mitano imewawezesha wajasiriamali kufanya mabadiliko kupitia shindano la 'Tigo Digital Change makers'.

Shindano hilo lililenga kuibua na kuwasaidia wajasiriamali ambao wanatumia programu na teknolojia katika kuboresha jamii na kuleta mabadiliko kwa vizazi vijavyo. Meneja Mkuu wa Tigo, Diego Gutierrez alisema kuwa, katika miaka mitano wamegusa maisha ya watoto zaidi 250,000 Tanzania.

"Tunaamini tutaleta mabadiliko katika maisha ya watoto wengi zaidi na kusaidia kuifanya Tanzania kuwa sehemu nzuri kwa vizazi vyetu vijavyo," alisema.

Gutierrez alisema kama nembo ya maisha ya kidijitali Tigo inatoa msukumo kwa mawazo na miradi inayoendeshwa na teknolojia ambayo inaleta mabadiliko endelevu.

"Teknolojia ya kidijitali siyo tu inabadilisha namna ambavyo tunafanya biashara ndani ya Afrika, inaleta mapinduzi kwa njia tofauti na kutatua masuala ya maendeleo ya jamii," alisema.

Alisema kutokana na heshima hiyo kubwa, Tigo inaunda fursa kwa mawazo hayo kutambuliwa, kuungwa mkono na kubadilisha hadi kiwango cha juu cha matokeo ya kijamii na kiuchumi.

"Shindano hili limewatambua waleta mabadiliko ya kidigitali kwa muda wa miaka mitano ambapo Tigo na Reach for Change inawatambulisha kwa jamii," alisema. Alisema washindi ambao walichaguliwa kuingia fainali hutokana na kundi la mamia ya wajasiriamali jamii ni wale waliotumia programu za kiteknolojia kupata suluhisho kwa matatizo yanayoikabili jamii.

"Tumeshasaidia jumla ya waleta mabadiliko ya kidijitali jamii tisa na tunatarajia kuwasaidia wengine kila mwaka ili harakati hizi zisonge mbele," alisema.

Anawataja waliowahi kushinda ni Nancy Sumari na Sophia Mbega ambao waliibuka kuwa washindi wa tano katika shindano hilo.

Alisema Tigo Tanzania kwa kushirikiana na asasi isiyo ya kiserikali ya Reach for Change iliwazawadia kila mmoja dola za Marekani 20,000.

Alisema Sophia aliwavutia majaji kupitia mkakati wake mkubwa wa kidijitali ambao umejielekeza katika kuvisaidia vikundi binafsi vya wanawake maarufu kama VICOBA.

"Ameibuka na programu ya simu ambayo inaunda jukwaa la ushirikiano linalotumia programu zilizopo kwa usimamizi wa kifedha na majukumu katika njia ambayo inaendana na mazingira ya Kiafrika."

Alisema Nancy alishinda kupitia mkakati wa 'KIDS JENGA HUB' ambao unaangalia msingi wa uelewa wa watoto kwa kufundisha programu za kompyuta, matumizi ya kiroboti na stadi za kuweka namba kwa wanafunzi wa shule ya msingi.

Alisema mshindi mwingine alikuwa ni Faraja Nyalandu ambaye anaendesha ujasiriamali jamii kidijitali unaofahamika 'Shule Direct'.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

### VIWANJA/MASHAMBA

**VIWANJA VINAUZWA,** Viwanja Vinauzwa Kibaha Visiga, ukubwa ni mita 20 kwa 20 bei ni millioni moja tuu(1,000,000/=) unaweza kulipa kwa awamu ndani ya miezi mitatu. Huduma zote zipo. Mawasiliano: 0714 090008 au 0767 090008

### KUPOTELEWA NA CHETI NA RESULT SLIP



**LINA COLBERT MUSHI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0284/0045** kilichotolewa na RoNeCa Girls Secondary School mwaka 2016 pamoja na karatasi ya matokeo (Result Slip). Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/STA/RB/106066/2019.**

115322802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DODOMA**
**SHAURI LA JINAI RUFAA NA. 02/2019**
**SENGA SUNZULA……………………………MRUFANI**
**DHIDI YA**
**MAKALA NYEMBE……………………MFUFANIWA**

**KWA: MAKALA NYEMBE – POPOTE PALE ULIPO**

**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA JINAI NA. 02/2019**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

**MNAFAHAMISHWA KWAMBA:** Shauri tajwa hapo juu litatajwa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dodoma mbele ya Mhe. Jaji L. Mansoor Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma saa tatu (3:00) kamili asubuhi siku ya Jumanne tarehe 16/07/2019.

**HIVYO:** Unatakiwa ufike wewe mwenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

**NA ENDEPO:** Hutafika wewe mwenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au Wakili wako kuwepo.

**HATI HII IMETOLEWA:** Kwa mkono wangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 10/07/2019.

115322702


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# GRIEZMANN: NATAKA KUIPAISHA ZAIDI BARCA

**BARCELONA,** Hispania

ANTOINE Griezmann mara baada ya kukamilisha usajili wake na Barcelona amesisitiza kuwa anataka kuwafanya miamba hao wa Katalunya kuwa bora zaidi.

**Mshambuliaji huyo alikamilisha usajili wa pauni milioni 108 kutoka kwa wapinzani wao wa La Liga, Atletico Madrid Ijumaa kabla ya kupanda ndege na kupaa kwenda Barcelona, ambako alifanya ziara ya kwenye klabu hiyo na kukuta jezi zake zipo tayari.**

"Nina furaha kubwa," alisema. "Nasubiria kukutana na wachezaji wenzangu wapya.

"Ni changamoto mpya, pia nikiwa na malengo mapya kabisa. Natumaini nitafanya vizuri na nilivyokuwa nafanya katika klabu nyingine na nchi yangu.

"La Liga, Copa del Rey, Ligi ya Mabingwa Ulaya haya ndio malengo yangu na ya klabu na nina matumaini makubwa ya kushinda hapa."

Griezmann pia alisema kwamba anajisikia fahari kubwa sasa atacheza sambamba na Lionel Messi.

Aliendelea kusema: "Nasubiria kuona jinsi anavyokuwa siku hadi siku kwenye mazoezi. Kucheza naye litakuwa jambo kubwa ninalolisubiria kwa hamu kubwa na ni furaha kwangu.

"Nilikuwa natamani kuja hapa na familia yangu ipo nyuma yangu, hii ni klabu kubwa na nina matumaini makubwa ya kufanya mengi hapa na nina imani kubwa zaidi.

"Hakika nasubiri kuwa na wachezaji wangu wapya pamoja na kocha Ernesto Valverde, na kucheza kwenye dimba la Nou Camp ni jambo nzuri zaidi kwa upande wangu na nina hamu kubwa."

# *Arsenal yarudi na dau nono Kieran*

**LONDON,** England

ARSENAL imerudi kwa mara ya pili na ofa ya thamani ya pauni milioni 25 kwa ajili ya nyota wa klabu ya Celtic, Kieran Tierney.

Celtic ilikataa ofa ya kwanza ya pauni milioni 15 mwezi uliopita na sasa wameamua kuongeza kwa kuamini safari hii watakubaliwa.

Napoli bado imebakia kuwa klabu pekee inayomwania Tierney, lakini bado hawajatoa ofa kwa sababu hawajamuuza beki wao wa kushoto, Mario Rui ili kupata fedha.

Kocha Carlo Ancelotti ametajwa kuwa anavutiwa zaidi na mchezaji huyo raia wa Scotland na ana matumaini ya kuipiku Arsenal kupata saini ya mchezaji huyo.

Unai Emery anataka kuimarisha safu yake ya ulinzi na Arsenal ina matumaini kwamba ofa yao ya sasa inatosha kutoa ushawishi wa kumsajili mchezaji huyo.

Tierney, kwa sasa anauguza majeraha ya kuumia mfupa wa kiuno anatajwa kwamba ndio beki anayekuja juu zaidi nchini Scotland kwa sasa.




# Inter Milan yamrudisha nyumbani Icardi



**MILAN,** Italia

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Mauro Icardi amerudi nyumbani na imethibitishwa kwamba hatakuwa na timu hiyo kwenye ziara ya maandalizi ya msimu mpya barani Asia, klabu hiyo imetangaza.

Klabu hiyo ipo kwenye mazoezi yake nchini Uswisi kabla ya kusafiri kwa ajili ya mechi za kirafiki dhidi ya Manchester United, Juventus, Paris Saint-Germain, Tottenham na Valencia.

Kuondoka kwa nahodha huyo wa zamani wa klabu hiyo, Icardi kunaweza kuwa ndio mwisho wa siku zake pale Nerazzurri.

Alinyang'anywa unahodha katikati ya msimu wa 2018-19 kabla ya kusimamishwa na klabu hiyo kwa utovu wa nidhamu.

Kwenye ukurasa wa Twitter klabu ya Inter Milan ilisema uamuzi wa kumrudisha Icardi umekuja kwa makubaliano ya pande zote mbili.

Inter Milan imekuwa ikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili nyota wa Manchester United, Romelu Lukaku, ambaye hakuchezeshwa kwenye mchezo wa maandalizi ya msimu dhidi ya Perth Glory Jumamosi.

## HABARI MICHEZO

# Coutinho: Nipo tayari kurudi Liverpool

**BARCELONA,** Hispania

PHILIPPE Coutinho sasa amebainisha kwamba, milango iko wazi ya kurudi kwenye klabu yake ya zamani Liverpool kama itamfuata na kutaka huduma kipindi hiki cha majira ya joto, kwa mujibu wa ESPN FC.

Raia huyo wa Brazil ameweka wazi mpango wake wa kuachana na maisha ya pale Camp Nou baada ya kushindwa kuwa kwenye kiwango bora.

Coutinho aliigharimu Barcelona pauni milioni 142 kutoka Liverpool Januari mwaka jana na mabingwa hao wa La Liga wanataka kumuuza haraka iwezekanavyo ili kurudisha fedha ya kusajili wachezaji wengine.

Kocha Jurgen Klopp ameambiwa aende kuinasa huduma ya kiungo huyo na kumrudisha Anfield kama kweli anataka kikosi chake kiwe na nguvu ya ziada na kushinda ubingwa wa Ligi Kuu England msimu wa 2019/20.

Kinachoelezwa ni kwamba Liverpool itamsajili Coutinho kwa bei ya chini, lakini saini yake haitapatikana kirahisi kutokana na Paris Saint-Germain nayo kumhitaji.

Taarifa za kutoka Nou Camp zinadai Coutinho safari inamhusu baada ya Antoine Griezmann kukamilisha usajili wake wa kutua pale Barcelona.




# BAYERN WAONGEZA DAU KWA HUDSON-ODOI




**MUNICH,** Ujerumani

BAYERN Munich haijakata tamaa na mpango wake wa kumsajili nyota wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi, baada ya kujiandaa kutoa ofa ya pauni milioni 45 wiki hii.

Kiwango hicho cha fedha kimeongezeka kwa pauni milioni 10 kutoka ofa waliyoitoa Januari siku ya mwisho ya kufungwa dirisha dogo la usajili.

Mkurugenzi wa soka wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic, alithibitisha mpango wa kutaka kumsajili mchezaji huyo wiki iliyopita kwenye gazeti moja la Ujerumani na akasisitiza kuwa mabingwa hao wa Bundesliga wanafanya kila njia kumsajili.

Hata hivyo, kocha mpya wa Chelsea, Frank Lampard amebainisha wazi kwamba, ana mipango na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 na hataki aondoke klabuni hapo.

Bayern wanahaha kutaka kumsajili Hudson-Odoi kama mrithi wa muda mrefu wa wachezaji wakongwe, Arjen Robben na Franck Ribery ambao wameondoka klabuni hapo.

Hudson-Odoi yupo kwenye mazoezi pale kambi ya Cobham huku akiendelea kupona taratibu, wakati wachezaji wenzake wiki iliyopita walikuwa jijini Dublin nchini Ireland na wiki hii wanatarajia kusafiri kwenda Japan kwa ziara ya mandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu England.

Lampard alibainisha wiki iliyopita kwamba, atakaa chini na Hudson-Odoi kuzungumza nae ili aweze kubakia klabuni hapo kwani ana mipango naye ya muda mrefu.

# *Madrid wampa likizo Zidane*

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid imethibitisha kifo cha Farid, ambaye ni kaka wa kocha wa klabu hiyo, Zinedine Zidane.

Uongozi wa klabu hiyo umeeleza kuwa Zidane amepewa likizo fupi. Imeelezwa kuwa kaka yake alifariki akiwa na umri wa miaka 54 kutokana na ugonjwa uliokuwa unamsumbua kwa muda mrefu ambao haukutajwa.

Mtoto wa Zidane, Luca, ambaye ni mlinda mlango wa klabu hiyo pia aliambatana na baba yake Ijumaa, Julai 12, 2019 kutokana na kupokea taarifa hiyo ya msiba.

Real Madrid ilithibitisha kifo cha Farid kupitia tovuti yake huku ikitangaza kuwa katika mazoezi yanayoendelea ya klabu hiyo kutakuwa na wakati wa ukimya kwa ajili ya kumkumbuka na kumwombea marehemu huyo.

"Wachezaji wetu wote walikuwa na wakati wa ukimya kuelekea katika kambi ya mazoezi, Montreal kufuatia kifo cha Farid Zidane, kaka wa kocha wetu mkuu, Zinedine Zidane," imeeleza taarifa hiyo.

Kocha Msaidizi, David Bettoni ataiongoza timu hiyo katika mazoezi hadi Zidane atakaporejea. Wawili hao ni marafiki wa karibu. Walikutana kwa mara ya kwanza walipokuwa wanacheza katika timu ya vijana nchini Ufaransa.



## DONDOO SOKA
MAGAZETI Y AYA




# UNITED KUMPA JUKUMU POGBA

●●● Ni kitambaa cha unahodha wa timu hiyo na uamuzi rasmi utatangazwa...

**PERTH,** Australia

KOCHA Ole Gunnar Solskjaer amethibitisha kwamba anamfikiria Paul Pogba kuwa nahodha mpya ajae wa Manchester United licha ya kiungo huyo kusema anataka kuondoka klabuni hapo.

**Solskjaer anatafuta nahodha mpya baada ya kuondoka kwa nahodha wa zamani, Antonio Valencia mwishoni mwa msimu uliopita.**

Ashley Young na Juan Mata walivaa kitambaa cha unahodha kwenye ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Perth Glory juzi Jumamosi, lakini bosi huyo wa United amesema Pogba, ambaye ameshatamka hadharani kwamba anataka kwenda kupata changamoto mpya kipindi hiki cha majira ya joto, anaweza kuwa nahodha wao, uamuzi ambao bado haujafikiwa kabla ya kuanza msimu mpya.

"Kuna uwezekano kabla ya kuanza kwa msimu mpya tutatangaza nahodha mpya," alisema Solskjaer katika mkutano wake na waandishi wa habari kwenye uwanja wa Optus.

"Tuna wakati mzuri wa kuchambua na kuangalia jinsi maendeleo ya kikosi yanavyokwenda. Lakini kama ulivyoona, Ashley atavaa kitambaa cha unahodha wakati akicheza hadi tutakapoamua nani achukue mikoba hiyo."

Alipoulizwa moja kwa moja kama Pogba ni moja ya jina linalofikiriwa, Solskjaer alijibu: "Yaap."

Wakati akiondoka uwanjani, Pogba alikataa kulizungumzia hilo alipoulizwa na waandishi wa habari na akajibu: "Nani anataka kuzungumza? Hakuna haja." Romelu Lukaku, ni mchezaji mwingine anayataka kuondoka Old Trafford kipindi hiki cha majira ya joto, aliukosa mchezo huo wa hapa Perth kutokana na kuwa majeruhi.

Raia huyo wa Ubelgiji ambaye alisema 'mtajua kitu fulani wiki ijayo' anawaniwa na Inter Milan na Solskjaer alikataa kuthibitisha kama mshambuliaji huyo atabakia kwenye kikosi hicho katika msimu ujao.

"Ngoja tuone wakati msimu utakapoanza," alisema Solskjaer, ambaye aliongeza kusema hakutakuwa na wachezaji wengine watakaokuja kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili.

"Hatuna ofa yoyote tunayoifikiria. Majadiliano yangu yote yatakuwa ya siri, hicho ndio kipaumbele changu."

Solskjaer, ambaye alishuhudia kwenye mchezo huo mabao yake yakifungwa na Marcus Rashford na James Garner alithibitisha kwamba, Luke Shaw alitolewa nje kwa sababu aliumia misuli ya nyama za paja.

Kocha huyo raia wa Norway pia alibainisha kuwa, Kocha Msaidizi, Mark Dempsey, ambaye alirudishwa hoteli Alhamisi anaondoka kurudi England.

"Mark aliumia wakati wa mazoezi na sasa anarudishwa England kwa kujitazamia zaidi," alisema Solskjaer.

## ZISIKUPITE

### COUTINHO KUREJEA LIVERPOOL

KIUNGO wa Barcelona, Philippe Coutinho anatarajia kukataa ofa ya kujiunga na Manchester United, hata hivyo ameweka wazi kwamba upo uwezekano wa kurejea Liverpool. Mbrazil huyo (27), anatajwa kama anaweza pia kujiunga na Paris St-Germain. ***(Express)***

### BARCA YAWEKA NGUMU

BARCELONA imemweleza wakala wa Coutinho kuwa hawana mpango wowote wa kumuuza mchezaji huyo, lakini amewaeleza kwamba mteja wake amepata ofa kutoka katika klabu mbalimbali ambazo zinachuana na vigogo hao wa Hispania. ***(Sky Sports)***

### YAMGANDA HUDSON-ODOI

BAYERN Munich bado haijakata tamaa ya kuwania saini ya mshambuliaji wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Callum Hudson-Odoi, ambaye ana umri wa miaka 18, kwa kujiandaa kuwasilisha ofa mpya ya pauni milioni 45 wiki hii.***(Mail)***

### UNITED WAITEGA MADRID

MANCHESTER United haitakuwa tayari kumuuza kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba (26) endapo Real Madrid haitawasilisha ofa ya kutaka kumsajili nyota huyo kabla ya dirisha la usajili la Ligi Kuu England litakapofungwa Agosti 8 mwaka huu. ***(Mirror)***

### MAGUIRE AIPASHA LEICESTER

BEKI wa Leicester na Timu ya Taifa ya England, Harry Maguire (26), ambaye anahusishwa kujiunga na Manchester United kwa dau la pauni milioni 75, ameiambia klabu yake maarufu Foxes kwamba anataka kuondoka. Pia ameilalamikia klabu yake kwa kupandisha dau. ***(Mail)***

### NEYMAR ASISITIZA KUONDOKA

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Brazil, Neymar (27), ameendelea kuilazimisha klabu yake ya Paris St-Germain ikubali arejee Barcelona huku akieleza kwamba ushindi wa mabao 6-1 walioupata mwaka 2017 akiwa na Barca dhidi ya mabingwa hao wa Ufaransa ndio kumbukumbu nzuri zaidi anayoikumbuka katika maisha yake ya mpira. ***(Mail)***

### CHALOV AGOMBEWA EPL

LIVERPOOL imeingia katika vita ya kuwania saini ya straika wa CSKA Moscow, Fedor Chalov kwa dau la pauni milioni 20. Arsenal, Manchester City, Tottenham, Chelsea na Manchester United zimetajwa kumwania mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(Mirror)***

### CELSO AKARIBIA SPURS

TOTTENHAM imeweka wazi nia yake ya kuwania saini ya kiungo wa Real Betis na Timu ya Taifa ya Argentina, Giovani lo Celso (23), huku klabu hiyo ya Hispania ikitajwa kumwania kiungo wa Lyon na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Nabil Fekir, 25. ***(Football.London)***

### STURRIDGE ANUKIA BOLOGNA

NYOTA Daniel Sturridge anatakiwa kusajiliwa na klabu ya Bologna ya Italia baada ya straika huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya England, ambaye ana umri wa miaka 29, kuondoka Liverpool. ***(Express)***

### MAEHLE ATAKIWA BUNLEY

MABOSI wa Burnley wanajiandaa kumsajili beki wa kulia wa Genk ambaye ni raia wa Denmark, Joakim Maehle (22), kwa dau la pauni milioni 7. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

## Bwenda mshindi Tigo Soka Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya Kampuni ya Mawasiliano ya Tigo, kufanikisha ndoto za wateja wake kwenda kushuhudia mechi za Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) nchini Misri, mwishoni mwa wiki kampuni hiyo imetangaza mshindi wa kitita cha Sh. milioni 10 kupitia promosheni hiyo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Meneja Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael, alimtaja mshindi huyo wa mwezi kuwa ni mfanyabiashara, Omar Bwenda (27).

Shisael alisema kuwa kupitia promosheni hiyo iliyoandaliwa na Tigo kwa ajili ya kuwashukuru wateja kwa kuendelea kuiunga mkono kwa kununua bidhaa na kutumia huduma zake, imewawezesha pia wateja wengine 28 kujishindia fedha taslimu Sh. 100,000/- kila siku na wateja wanne kujishindia Sh. milioni moja kila mwezi.

Alisema kuwa promosheni hiyo itakayodumu kwa kipindi cha miezi mitatu, washiriki wataendelea kujishindia zawadi za fedha na ili kushiriki, mteja atatakiwa kutuma neno SOKA kwenda namba 15670 au tembelea tovuti ya www.tigosports.co.tz na kujibu maswali kuhusiana na michuano ya Afcon inayoendelea.

"Natoa wito kwa watumiaji wa mtandao wa Tigo kuendelea kuchangamkia na kushiriki promosheni hii ya SOKA la AFRIKA, ili waweze kujishindia zawadi, na kadri wanatavyoshiriki na kujibu maswali ndivyo watakavyokuwa na nafasi kubwa zaidi ya kupata ushindi.

## Kipanga waichapa Zimamoto Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU iliyopanda daraja ya Kipanga imefanikiwa kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Zimamoto katika mechi ya kirafiki iliyochezwa juzi kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar unaotarajiwa kufanyika kuanzia Agosti 25 mwaka huu.

Bao pekee katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Ngome uliopo Fuoni lilifungwa na Mohamed Masoud dakika ya 25.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Kipanga, Bakari Hussein Bori, alisema kuwa wamefurahishwa na matokeo hayo na timu yake inatarajia kucheza mechi nyingine na timu za Ligi Kuu pamoja na Ligi za Kanda ili kuwajenga zaidi wachezaji wao.

Bori alisema wanataka kabla ya kuanza kwa msimu mpya, wachezaji wao wawe wameimarika na kuwa tayari kukabiliana na ushindani kwenye ligi hiyo ya juu visiwani hapa.

Naye Katibu Mkuu wa Zimamoto, Ali Jongo, aliliambia gazeti hili kuwa kikosi chake kinaendelea kurekebisha makosa waliyoyabaini msimu uliopita na kupelekea kushindwa kutwaa ubingwa katika dakika za lala salama, ili msimu huu waweze kutimiza ndoto zao.

# NDAYIRAGIJE HESABU KALI AKIWAVAA TP MAZEMBE

**Na Shufaa Lyimo**

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Kombe la Kagame, Azam FC wameahidi kufanya vema katika mchezo wao wa robo fainali dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) utakaochezwa kesho jijini Kigali, Rwanda.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Azam FC, Etienne Ndayiragije, alisema kikosi chake kiko tayari kuwakabili mabingwa hao wa zamani wa Afrika na wamejipanga kwa kuongeza umakini katika mchezo huo.**

Ndayiragije alisema kuwa ili waweze kusonga mbele katika mashindano hayo, watatakiwa kucheza kwa nguvu kwa sababu wanakutana na wachezaji wenye uzoefu wa mechi za mtoano.

"Tunashukuru tunaendelea vizuri na mazoezi, tunajua TP Mazembe ni wazoefu, tutajiandaa kuivaa Mazembe kutokana na timu hiyo ilivyo, kwanza tulikuwa na mpango wa kucheza na Rayon, lakini sasa tutajipanga kucheza na Mazembe, hii ni mechi ya dakika 90, ni mtoano, tunahitaji kujiandaa kufanye nini na kwa wakati gani, tuko tayari," alisema Ndayiragije.

Alisema kuwa kikosi chake kinaundwa na wachezaji mchanganyiko, hivyo anaamini watajituma kuhakikisha wanafanya vema hasa wakijua wao ndio mabingwa watetezi wa michuano hiyo.

"Tunaomba mashabiki wetu pamoja na Watanzania wazidi kutusapoti na kutuombea ili tuweze kurudi nyumbani na kombe letu, tumeziangalia timu zote zinazoshiriki mashindano haya kuanzia hatua ya kwanza, tutajipanga kuhakikisha tunaendelea kufanya vema na kutetea ubingwa," Ndayiragije alisema.

Aliongeza kuwa mashindano ya msimu huu yana ushindani zaidi tofauti na misimu iliyopita kwa sababu timu zote zilijiandaa kuwania kombe hilo kuanzia hatua ya makundi.

Alieleza kuwa TP Mazembe ni moja kati ya timu bora barani Afrika, hivyo ni lazima unapokutana nayo, ucheze kwa heshima.




Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara (katikati), akiwa na mchezaji mpya wa mabingwa hao, Francis Kahata (kushoto) na Meddie Kagere kwenye kambi ya timu hiyo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SIMBA**

## *Waogeleaji wanne majaribuni Korea*

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAOGELEAJI wa Tanzania wanatarajia kuondoka nchini kesho kuelekea Korea Kusini kwa ajili ya kwenda kushiriki mashindano ya dunia ya mchezo huo, imeelezwa.

Safari hiyo itajumuisha waogeleaji wanne ambao ni pamoja na Hilal Hemed, Collins Saliboko ambao watashindana kwa upande wa wanaume na wanawake ni Sylvia Caloiaro na Shivan Bhatt.

Katika kuhakikisha wanafanya vema katika mashindano hayo, Kampuni ya Motisun ya jijini Dar es Salaam, imewakabidhi kiasi cha Dola za Marekani 2,000 (sawa na Sh. milioni 4.4 ) ili ziwasaidie katika mahitaji mbalimbali.

Meneja Mkuu wa kampuni hiyo, Nitin Menon, aliwataka waogeleaji hao wakapeperushe vizuri bendera ya nchi kwa sababu Watanzania zaidi ya milioni 45 wanawategemea kuona wanapata matokeo mazuri katika mashindano hayo.

Menon alisema kuwa licha ya ushindani uliopo, anaamini maandalizi waliyofanya, yatawasaidia kurejea nchini na medali.

"Naomba mkafanye vizuri katika mshindano haya na kuendelea kuleta hamasa kwa wanamichezo nchini, tupo pamoja nanyi katika kuendeleza gurudumu la maendeleo ya michezo Tanzania," alisema Menon.

Alisema kuwa hiyo si mara ya kwanza kwa kampuni yao kusaidia wanamichezo, na kueleza hivi karibuni walishiriki katika maandalizi ya Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) iliyokuwa inajiandaa na fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) pamoja na kudhamini mashindano ya vijana ya umri chini ya miaka 17 (Afcon U-17) yaliyofanyika mapema Aprili mwaka huu hapa nchini.

Naye Katibu Mkuu wa Chama cha Kuogelea nchini (TSA), Inviolata Itatiro, alisema aliipongeza kampuni hiyo kwa kuwapa hamasa waogeleaji hao ambao chama pia kinaamini wataenda kufanya vema katika mashindano hayo ya dunia.

# Michezo

Jumatatu Julai 15, 2019

Nipashe



United kumpa jukumu Pogba

UKURASA 30



Wachezaji wa Simba wakifuatilia kwa umakini maelekezo kutoka kwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Patrick Aussems (picha ndogo), ikiwa ni sehemu ya kwanza ya maandalizi ya msimu mpya wa 2019/20. **PICHA: SIMBA SC**

# MAGORI: SIMBA TUMEJIPANGA

## ●●● Kundi la kwanza kuondoka leo kuelekea kambini Rustenburg, Afrika Kusini...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI kikosi cha mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kikitarajia kuondoka nchini leo kuelekea Afrika Kusini ili kujiandaa na msimu mpya wa mwaka 2019/20, uongozi wa timu hiyo umesema wao sasa wako "levo" nyingine.

**Simba inayonolewa na Mbelgiji Patrick Aussems, na ilitwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya pili mfululizo, inatarajia kuweka kambi zaidi ya mbili katika mji wa Rustenburg.**

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, alisema kuwa uamuzi wa kwenda Afrika Kusini unalenga kuendelea kuwajenga wachezaji wao na kuwaweka tayari kushindana katika ngazi za kimataifa.

Magori alisema kuwa baada ya kuwasili kambini, walianza na zoezi la utambulisho na kushiriki semina elekezi kutoka kwa wataalamu mbalimbali walioandaliwa na klabu hiyo ambayo ilikuwa na lengo la kuwaongezea uelewa na kujiandaa kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Alisema kuwa wanatarajia watakuwa na msimu wenye mafanikio zaidi, kutokana na hali ya wachezaji waliowasajili kuonekana wana "kiu" ya kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali watakayoshiriki.

"Tunashukuru Mungu wachezaji wetu wote wamefika kwa wakati, tumeanza kwa darasa maalumu au unaweza kuiita semina elekezi, kwa kifupi Simba tunasema tumejipanga," alisema Magori.

Alisema kuwa kundi la kwanza litakaloondoka leo litakuwa na watu 33 na watakaobakia wataondoka kesho, na hii inatokana na taratibu za visa za baadhi ya wachezaji wao wa kigeni kutokamilika kwa wakati.

"Msafara utakaoondoka kesho (leo), utakuwa ni wa watu 33, wengine wataondoka keshokutwa (kesho), na kambi yetu inatarajia kuwa ya zaidi ya wiki mbili na tumeamua kukaa nje kidogo ya mji (Rustenburg), na baadaye tutarudi kwa ajili ya Simba Day," alisema Magori.

Aliongeza kuwa Aussems amehitaji mechi tatu za kirafiki wakiwa huko Afrika Kusini na tayari wako katika hatua za mwisho za mazungumzo na klabu za huko ili waweze kutimiza mahitaji ya kocha wao.

Mbali na maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambapo itafungua pazia dhidi ya "Maafande" wa JKT Tanzania, Simba pia itashiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Pia Simba itashuka kucheza mechi ya kuwania Ngao ya Jamii dhidi ya mabingwa wa Kombe la FA, Azam FC itakayochezwa Agosti 17 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

# Yanga ushindani wazidi kukolea

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA wanaingia wiki ya pili tangu kuanza mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara, hali ya ushindani wa kuwania namba katika kikosi cha Yanga umeonekana ni wa kiwango cha juu, imefahamika.

Yanga inafanya mazoezi yake kwenye Uwanja wa Chuo cha Biblia, kilichoko eneo la Bigwa mkoani Morogoro chini ya Kocha Msaidizi Mzambia...

Mratibu wa timu hiyo, Hafidh Saleh, aliiambia gazeti hili kuwa kila mchezaji ana morali na hii inaonyesha kwamba hakuna ambaye ana uhakika wa kuwapo kwenye kikosi cha kwanza. Saleh alisema kwamba "vita" hiyo ya kuwania namba inasaidia kukuza viwango vya wachezaji hao na muda wa kuanza msimu mpya utakapofika, watakuwa imara kukabiliana na ushindani.

Wachezaji wapya waliosajiliwa Yanga ni Ally Ally kutoka (KMC), Ally Mtoni 'Sonso' (Lipuli), Lamine Moro ( Liberty Academy-Ghana), Mustapha Suleiman (Burundi), Abdulaziz Makame (Mafunzo FC), Mapinduzi Balama (Alliance), Issa Bigirimana, Patrick Sibomana (Rwanda), Juma Balinya (Uganda), Maybin Kalengo (Zambia), Mwalimi Salum (Singida United), Farouk Shikhalo (Bandari) na Sadney Urikhob (Namibia).

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002